ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu - Tarehe 24 Septemba, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani hati ya Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora kuhusiana na mambo hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Marekebisho mbali mbali na kuweka masharti yaliyo bora kuhusiana na mambo hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 93

Maslahi ya Walinzi katika Visima vya Maji

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Aliuliza:-

Katika kijiji cha Makoba kilicho katika Shehia ya Mafufuni kuna kisima kimoja ambacho kimekuwa kikifanya vizuri hadi sasa. Hata hivyo, katika kisima hicho kumekuwa na walinzi ambao wamekuwa wakifanya kazi ya kujenga taifa kwa muda wa miaka kumi na sita (16) sasa.

(a) Je, wizara yako ina mpango gani juu ya hatma ya walinzi hao katika kuwafikiria kuwapatia maslahi yoyote.

(b) Wizara yako itakuwa tayari kuwaajiri walinzi hao ambao wamekuwa wakijitolea kufanya kazi hiyo muhimu kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza kabisa wizara yangu inapenda kuwapongeza walinzi walioelezwa na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini kwa kujitolea kwao na kushirikiana na serekali katika kazi ya kujenga taifa na kuwahudumia wananchi wa jimbo husika.

Mhe. Spika, lakini napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba, katika vituo vya maji kuna wafanyakazi wa kujitolea ambao wamegawika kwa utaratibu mbali mbali katika maeneo husika, ikiwemo utekelezaji na undelezaji wa miradi ya *TASAF* ambapo wananchi wenyewe walichukua ahadi ya kulinda na kuienzi miradi hiyo kwa njia ya kujitolea. Kuna miradi inayoendelezwa na Uongozi wa Majimbo ama kupitia Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi ambapo Waheshimiwa hao huwateuwa watu wanaowaamini katika jamii husika kwa ajili ya kulinda miradi hiyo kwa makubaliano baina yao na viongozi niliowataja awali. Pia, baadhi ya maeneo ya uwekezaji huanzishwa miradi ya maji na kuweka ulinzi wao wenyewe unaopelekea katika maeneo mengi ya Mijini na Vijijini kuwa na walinzi wa kujitolea ikiwemo Jimbo la Bumbwini.

(b) Kwa kuwa walinzi hao ni wengi kutokana na makubaliano walioyafanya awali, serikali imo katika hatua ya kuangalia utaratibu wa ajira zao kulingana na sifa na hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa vile amesema serikali inaweza kuangalia watumishi hawa, lakini ukiangalia kwamba wengine tayari umri unazidi kuwapita.

Je, imewafikiria nini kuweza kuwapatia haki zao hawa ambao umri umeshawapita wa kuajiriwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kuwa hawa sio waajiriwa, kawaida sisi huwa tunawapa posho ndogo ndogo kama kifuta jasho, kwa sababu waliingia makubaliano na wahusika wengine ambao sio waajiriwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, hakuna utaratibu wa kuwapa maslahi kama wafanyakazi wengine.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na kazi nyeti wanazofanya walinzi hawa katika vyanzo vya maji na kama tunavyojua kwamba vyanzo vya maji ni taasisi nyeti ambayo ikitokea uharibifu wa mara moja unaweza kuhatarisha usalama wa afya au hata maisha ya wananchi wa Zanzibari.

Je, serikali haioni kwamba kuna sababu maalum kutafuta waajiriwa rasmi ambao wamepitia mafunzo kwa ajili ya usalama wa vyanzo vile vya maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kweli serikali inaona umuhimu na ndio maana pamoja na kuwepo wale wa kujitolea ambao walikubaliana na waanzilishi, lakini pia kuna wafanyakazi wanaokagua visima hivyo mara kwa mara; matengenezo yote yako chini ya serikali, lakini pia kuna wahudumu wetu ambao wanakuweko katika maeneo hayo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza kwa ruhusa yako napenda nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia naomba kuuliza swali la nyongeza. Visima hivi ambavyo vinalindwa na watu ambao hawajaajiriwa na serikali ni vingi na viko katika majimbo mengi sana. Lakini kuna baadhi ya maeneo hata wale waliokuwa wameajiriwa na serikali wanalinda na pia wanapiga *pump*. Wananchi wengi wanalalamikia hawa wapiga *pump* kwamba wanafunga maji kwa makusudi.

Je, wizara yake imejiandaa vipi kukomesha tatizo hili ambalo linalalamikiwa sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo ambalo alilolizungumza walilileta wakati wa Kikao cha Kwanza cha Baraza na tumelipokea kulifanyia kazi kuliangalia ukweli wake. Kusema kweli mara nyingi maji yanafungwa kutokana na tatizo la umeme mkubwa, kwa sababu mahitaji yanakuwa mengi, lakini baada ya kuzungumza na wahusika wakatueleza kwamba zile *units* wanazopewa wakazipiga moja kwa moja zinakuwa hazitoshi na ulipaji wa maji umekuwa mdogo. Mhe. Spika, ndio maana hamasa kubwa sasa hivi tunawaambia Wawakilishi hata kile kikao kilichopita watusaidie kuhamasisha kwa maeneo ambayo maji yanatoka na yapo, basi wananchi waweze kulipa ili na sisi tuweze kufidia gharama kubwa za umeme ambazo Mamlaka zinawakabili.

Nam. 120

Kuletwa kwa Sera ya Gesi na Mafuta

Mhe. Simai Mohamed Said – Aliuliza:-

Ni lini serikali italeta Sera ya Gesi na Mafuta ili Wawakilishi wapate kuielewa vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 120 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Serikali tayari imekamilisha Sera ya Mafuta na Gesi Asilia tokea mwaka 2015. Sera hiyo imeidhinishwa na Baraza la Mapinduzi kama utaratibu unavyotaka, kufuatia kukamilika kwa sera hiyo ndipo hatua za kutayarisha Mswada wa Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia zitafuata. Aidha, sera hiyo ndio dira iliyoongoza sheria itakayowasilishwa Barazani. Sera hiyo imewasilishwa kwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi na baadae itasambazwa kwa wadau wote kupitia utaratibu maalum utakaoandaliwa.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Spika, na mimi ningependa niulize swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa nchi nyingi ambazo zilipata neema hii ya mafuta na gesi, ziko nchi nyengine duniani zilitokea kwamba wananchi walivunjika moyo katika masuala ya nguvu kazi na kuelekeza akili zao zote katika neema ya mafuta na gesi.

(a) Je, wizara husika imejipanga na mikakati gani katika kuhakikisha kutoa elimu kwa umma ili kuhakikisha Wazanzibari wote wanaendelea na shughuli zao za kila siku kama kawaida na ili wananchi waweze kufanikiwa.

(b) Katika kutunga hii sheria, ni utaratibu gani umetumika katika kujenga mahusiano na wenzetu wa *TPDC* katika upande wa Tanzania Bara. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kama Naibu wangu alivyojibu swali la msingi kwamba, utaratibu maalumu unaandaliwa wa kusambaza na kutoa elimu kwa sababu ya sera, lakini pia na sheria baada ya kuipitisha ndani ya Baraza la Wawakilishi. Utaratibu huo ukishakuandaliwa basi fursa kubwa kwa wananchi wa Zanzibar wataipata ili

kufahamu na kuelewa lengo la serikali katika sheria hii, lakini na kuweza kuifahamu sheria yenyewe.

La pili, ni kwamba sikulisikia vizuri, lakini nafikiri *in relation* na sheria za nchi nyengine si ndio ee? Swali la pili sikulisikia vizuri.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Spika, swali la (b) niliuliza kwamba, ni utaratibu gani umetumika wa kisheria na katika kujenga mahusiano kupitisha sheria hii, tumejenga mazingira bora kwa upande wetu na Tanzania Bara kwa Shirika la *TPDC*.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, utaratibu uliotumika nafikiri ni utaratibu wa kawaida ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unaotumika, kwamba wataalamu wakishirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika utekelezaji na utungaji wa sheria. Lakini pia kawaida wanapotunga sheria huwa wanaangalia na sheria zile *related* ambazo zina manufaa kwa watu wao. Pia, wameweza kufanya *comparison* na nchi jirani ambazo wana *oil and gas* katika kutunga sheria hii.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar chini ya kifungu cha 18(2) inampa haki kila raia kuwa na haki ya kupata taarifa pale ambapo anaitaka na hasa taarifa hiyo inapohusiana na maisha na shughuli za wananchi.

Naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba, kwa muda mrefu sasa Waheshimiwa Wawakilishi, wamekuwa wakiomba kupatiwa sera hii kutoka serikalini. Mhe. Waziri, atwambie je, ni lini atatupatia nakala ya sera hiyo ili na sisi tuwe na haki ya kupata taarifa kama ilivyoelezwa kwenye Katiba kifungu cha 18(1) na (2).

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, nafahamu kwamba haki ya kupata taarifa ni ya kila mmoja, lakini kwa bahati mbaya sana mimi sijapokea maombi ambayo rasmi ya kupatiwa hiyo sera. Sera ipo na sisi Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kama Naibu Waziri alivyosema walipatiwa sera hiyo na hata sasa hivi akitoka Mhe. Mjumbe, kwa sababu sera imo ndani ya Baraza la Wawakilishi basi mtu yeyote atakayeitaka sera hiyo itapatikana. Sera ni mali yetu sote na ni muongozo muhimu katika kuleta maendeleo ya taifa hili.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsane sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Katika nchi mbali mbali ulimwenguni kuna matatizo kwenye sehemu ya mafuta, na mafuta huwa ni chanzo cha ghasia na uhasama katika nchi mbali mbali, kwa kuwa hili tunalitarajia Mwenyezi Mungu akitujaalia tutachimba mafuta hapa kwetu.

Je, wanasiasa ni chanzo cha mwanzo wanaoleta vurugu katika kuwashawishi watu kwa mambo mengine, hili limeangaliwa vipi katika sheria hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa uzoefu alionao utatusaidia na Wajumbe waliokuwemo humu ni wanasiasa ndio watusaidie kuiweka hii hali vile ambavyo tunaitegemea, isije ikawa tofauti na hivyo. Ahsante sana.

Nam. 139

Tatizo la Uingiaji Kiholela kwa Wageni nchini

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:-

Kutokana na sheria zinazotumika ndani ya nchi ni kwamba sheria ya mgeni wa aina yeyote anaeingia ndani ya nchi hii ni lazima akaguliwe na awe na vitambulisho maalumu vinavyoonesha kwamba yeye ni nani na anatoka wapi, lakini tunaona kwamba suala hili liko tofauti kwa sasa. Maana kuna bandari ambazo zinatumika kwa kuingiza watu hao wa aina tofauti na wanaingia na mambo tofauti ambayo yako kinyume na maadili ya nchi yetu. Kwa kupitia ulinzi na sheria.

a) Je, serikali inalichukuliaje suala hili la uingiaji wa wageni bila udhibiti kwa usalama wa nchi yetu.

b) Na vipi watadhibiti uingiaji huu haramu katika nchi yetu na kusababisha matokeo tofauti na mabaya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 139 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba ieleweke kwamba, utaratibu wa ukaguzi wa wageni wanaoingia na kutoka nchini kupitia vituo vilivyopo katika mipaka yetu ni wa

kisheria chini ya Kanuni ya 19(1) na (2) ya Kanuni za Uhamiaji Sura ya 54, Marejeo ya mwaka 2002; ambapo mgeni akienda kinyume na utaratibu huo atakuwa amevunja sheria na hatua kali za kisheria zitatakiwa kuchukuliwa dhidi yake.

Mhe. Spika, serikali kupitia Idara ya Uhamiaji imekua ikichukuwa hatua mbali mbali za kukubaliana na wimbi la wageni wanaoingia nchini kwa njia zisizo rasmi kinyume na sheria za uhamiaji (wahamiaji haramu).

(a) Kwa kushirikiana na Vikosi vyengine vya Ulinzi na Usalama, Idara ya Uhamiaji imekuwa ikiimarisha ulinzi na usalama katika mipaka yetu ili kudhibiti tatizo la wahamiaji haramu nchini.

(b) Vile vile, Idara ya Uhamiaji imekuwa ikiendelea na misako na doria katika sehemu mbali mbali nchini mwetu, ili kuwabaini wageni waliokiuka taratibu na sheria za nchi yetu na kuwachukulia hatua kali za kisheria wageni wote wanaobainika kuvunja sheria za kiuhamiaji nchini ikiwemo kuwalipisha faini na kuwafikisha Mahakamani au kuwaondoa nchini.

Mhe. Spika, suala la ulinzi na usalama wa nchi yetu ni jukumu letu sote, hivyo serikali inatoa wito kwa wananchi wote kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama au kwa viongozi wa Shehia wanapobaini au kumtilia mashaka mtu yeyote anaishi katika maeneo yao ambaye uhamiaji wake haukufuata taratibu za kisheria.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika, Kwa kuzingatia majibu mazuri ambayo amenipa Mhe. Wazkiri. Lakini pia naomba kumuuliza suala moja.

Kweli majibu tumeyasikia vizuri na serikali tunajua kwamba inajitahidi kuimarisha ulinzi na usalama katika nchi yetu kwa ambao wanaingia ndani ya nchi kwa kupitia njia zote.

Lakini je, unatuthibitishia vipi na je, utatoa mashirikiano gani kwa Masheha wa Wilaya na Wakuu wa Wilaya na Halmashauri kwa kushirikiana kuimarisha huu ulinzi kwa kuwatafuta wale wote ambao wameingia ndani ya nchi kwa njia ambazo wanazijua wenyewe hususan katika kijiji cha Nungwi, Mkokotoni na Tumbatu pia. Naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nataka kumuhakikishia kwamba mashirikiano yapo kati ya Jeshi la Polisi na

uongozi na ndio maana Jeshi la Polisi katika kila ngazi lina uwakilishi wake na utendaji mzima wa shughuli za Kimikoa, Wilaya na sasa hivi hata Shehia basi Jeshi la Polisi lipo pale. Nia na madhumuni ni kushirikiana na uongozi ili kuhakikisha hali ya ulinzi katika maeneo husika yanakuwepo. Hata hivyo, serikali imeanzisha mpango maalum wa Polisi Jamii ili kuzidi kuimarisha ulinzi katika maeneo yetu.

Lakini naomba nitanabahishe Mhe. Spika, kwamba sote Watanzania ndio walinzi wa nchi yetu. Kwa hiyo, pale tunapoona jambo lolote la kuvunjwa utaratibu wa kisheria hasa wanapoingia hawa wageni wasiofata taratibu za kiuhamiaji, basi jambo la msingi ni kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika baada ya kuwafuga wahamiaji hao haramu.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba, tutaendelea kushirikiana na uongozi katika ngazi zote pamoja na wananchi ili kupambana na tatizo hili la wahamiaji haramu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, Zanzibar katika usafiri wetu tunatumia usafiri wa maji pamoja na usafiri wa Anga. Lakini naona tumejikita sana katika kuimarisha ulinzi wa upande wa Anga, upande wa maji hasa upande wa bandarini mpaka leo tunatumia kama kushikana shikana katika kupekuwa.

Ni lini tutatumia vyombo vya kisasa ambavyo vitaweza kutusaidia kiulinzi kuliko kuangaliana kwa mikono.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli upo umuhimu sana wa kuwa na boti za kisasa katika suala zima la kuimairisha ulinzi katika maeneo mbali mbali ya majini katika nchi yetu. Serikali imeliona hilo na licha ya jitihada zinazochukuliwa na Jeshi la Polisi, lakini kikosi chetu cha KMKM kimejipanga vyema katika kuimarisha ulinzi huo, hivi sasa kuna mpango mkubwa wa kikosi hichi kukiwezesha kuwa na boti za kisasa katika kufanya ulinzi wa sehemu mbali mbali.

Hata hivyo, hivi sasa Mhe. Suleiman Sarahan Said, ni shahidi anapoona vijana wetu hapa wanavyopambana na magendo ya karafuu.

Kwa hivyo, nichukuwe nafasi hii kuwapongeza sana sana wana-KMKM kwa kazi nzuri wanayoifanya katika ulinzi wa majini na hususan katika bandari zetu. Lakini nataka nimuhakikishia kwamba nia ya serikali ni kuimarisha boti za ziada kwa ajili ya ulinzi na majini na katika maeneo yote nchini.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, nchi yetu ni kisiwa na tumeshuhudia dunia nzima nchi nyengine zinapambana na uingiaji haramu kwa sababu hazitaki watu ndani ya nchi zao.

Mhe. Spika, nchi yetu tumeshuhudia uingiaji haramu umekuwa mwingi sana, kuna watu wanaishi nchi hii kutoka nchi nyengine kinyume na utaratibu, kinyume na sheria.

(a) Je, serikali lini itaanza mkakati ya kuwatafuta na wakuwatoa watu wote wa nchi nyengine wanaoishi nchi hii kinyume na sheria?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika suala langu la msingi kwamba hivi sasa upo mpango maalum ulioanzishwa na wenzetu wa uhakiaji kwa nia ya kufanya misako na doria ili kuwabaini wahamiaji haramu. Lakini inaonekana bado Wajumbe wa Baraza hili tukufu wanahitaji tufanye juhudi za ziada katika misako hiyo.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tunalipokea shauri hili tujipange vizuri zaidi ili misako na doria mbali mbali ziendeleze. Hata hivyo, kama nilivyotoa wito wangu wa awali kwamba kama viongozi katika ngazi mbali mbali za Majimbo, Shehia na kadhalika, tuna wajibu pia wa kushirikiana ili kuhakikisha kwamba wale ambao wanaishi kinyume na taratibu na kwa vyovyote vile jamii ndio wanaishi nao kwa njia moja au nyengine watakuwa wanaelewa.

Kwa hiyo, nitowe wito kwa viongozi sote tushirikiane ili kuwabaini watu hao. Hata hivyo, jitihda zitaongezwa ili doria iwepo na wale wote ambao wameingia nchini kinyume na utaratibu wa kisheria hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

Nam. 125

Kupatiwa nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Aliuliza:-

Watu wenye ulemavu hukosa ajira wanapofanya usaili na wakati sifa na Shahada zinazohitajika wanazo na uwezo wa kufanya kazi wanao.

a) Je, Wizara ina mpango gani katika kuwasaidia watu wenye ulemavu ili waweze kupata ajira.

b) Je, Wizara, Idara, Taasisi za Serikali huwafikiria vipi walemavu katika kuwaajiri kutokana na hali.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Zaina Abdallah Omar, swala lake Nam. 125 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kwanza kutoa maelezo mafupi kama yafuatayo:-

Mhe. Spika, Utaratibu wa ajira katika Taasisi za Umma umeeleza wazi katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011, kifungu cha 57, 58(2) na 59(1), ikisomwa kwa pamoja na Sheria ya Marekebisho Nam. 5 ya mwaka 2012, kuwa fursa za ajira zitazingatia kiwango cha elimu na sifa kulingana na nafasi ya kazi inayohitajika.

Mhe. Spika, Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake kama ifutavyo:-

a) Mhe. Spika, Pamoja na kwamba serikali inatoa fursa sawa za ajira kwa vijana wote wakiwemo watu wenye ulemavu hata hivyo, ili kuwasaidia watu wenye ulemavu wizara ina mpango wa kutoa kipaumbele kwa kuwaajiri vijana wenye ulemevu ambao watakuwa na viwango vya elimu, ujuzi na uwezo kwa mujibu wa nafasi iliyopo kama ilivyoelekezwa katika kanuni za 28(1) na Kanuni ya (30) ya Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2014.

Mhe. Spika, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinatoa mazingatio ya hali ya juu katika ajira za watu wenye ulemavu. Kutokana na hayo na kutambua na kuthamini misingi muhimu ya haki za binaadamu, taasisi hizi zinaamini:-

i. Kwamba watu wenye ulemavu wana uwezo wa kufanya kazi na kujipatia kipato kwa kufanya kazi

ii. Kwamba haki ya kufanya kazi ni ya msingi isiyoweza kutenganishwa na haki zengine za kibinadamu ambayo kila mtu anapaswa kuipata na kunufaika nayo kwa usawa nchini.

iii. Kwamba usawa wa fursa katika ajira umejengwa juu ya msingi kwamba wafanyakazi wote wenye ulemavu na wasio na ulemavu wana thamani na umuhimu ulio sawa, na

iv. Kwamba usawa wa fursa za ajira ni kanuni ya msingi inayopaswa kutambulika katika soko la ajira.

Mhe. Spika, Kutokana na imani hiyo, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinahakikisha kusimamia kwa karibu sana haki zifuatazo:-

i. Kufanya kazi halali kwa watu wenye ulemavu ambayo ameichagua kwa imani yake na itakayomuwezesha kuishi.

ii. Kuhakikisha kunakuwa na malipo sawa kwa kazi zenye thamani sawa bila ya ubaguzi wa aina yoyote kwa waajiri wote.

iii. Kuhakikisha watu wenye ulemavu wanafanya kazi katika mazingira mazuri ya kufanyia kazi yanayokidhi haja ya wafanyakazi wote.

iv. Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wana haki ya kupata vitendea kazi na kufanya kazi katika mazingira salama.

v. Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanastahiki mshahara kwa mujibu wa kazi wanayofanya, na

vi. Kuhakikisha kwamba mfanyakazi yeyote ambaye amepata ulemavu akiwa kazini anarejeshwa na kubakishwa kazini.

Mhe. Spika, Kutokana na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kuwa na mtizamo huu, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba, serikali imeweza kuajiri na inaendelea kuwaajiri watu wenye ulemavu katika Wizara na Idara za Serikali wenye viwango tofauti vya elimu ikiwemo Shahada ya Kwanza, Stashahada, Cheti na Elimu ya Sekondari. Ahsante.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Spika, ili watu wenye ulemavu wafaidike na vipao mbele ambavyo alivyovizungumzia Mhe. Rais, pale ambapo alipozungumzia nanukuu kuwa;

> "Atahakikisha kwamba kwa watu wenye ulemavu wanaondokana na mambo ambayo yanawabagua."

Je, haya mengine yako ndani ya wizara yako Mhe. Waziri, umejipanga vipi katika kuhamasisha Mawizara, Idara, Mashirika na Taasisi husika kuona kwamba wanaweza kuwaajiri watu wenye ulemavu wakati wa ajira unapofika? (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa kuwa katika suala langu mama nimesema kwamba ajira zinazotolewa zinatolewa kwa usawa bila ya kujali mtu mwenye ulemavu au asiekuwa na ulemavu. Kwa hivyo, kwa kuwa ajira zinatolewa bila ya ubaguzi serikali kupitia Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma inachukuwa jitihada mbali mbali kuhakikisha kwamba zile wizara nyengine ambazo huwa wanapelekewa wale watumishi kuwa wanajali watumishi wa aina zote wanapowapatia haki sawa watumishi wa aina zote bila ya kujali ulemavu wao, bila ya kujali sura zao, bila ya kujali jinsia yao. Ahsante.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara hii ya Katiba na Sheria inatakiwa iwe mfano katika kuwaajiri watu wenye ulemavu.

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi hadi sasa wameajiriwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, idadi halisi ya watu wenye ulemavu walioajiriwa katika serikali yetu kwa hivi sasa ni vigumu kumtolea idadi hiyo, lakini niseme kwamba nitajibu suala hili kwa njia ya maandishi. Sambamba na hilo, Mhe. Spika, naomba kuwaeleza Waheshimiwa Wawakilishi kwamba, serikali imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanaajiriwa kwa wingi na ushahidi ulivyo sasa hivi ni vigumu kwenda wizara kukutaka kwamba katika miongoni mwa wafanyakazi hamna mfanyakazi aliekuwa na ulemavu. Utakapotembelea wizara mbali mbali hili utaliona kwamba wafanyakazi wenye ulemavu na wasiokuwa na ulemavu wanaajiriwa katika taasisi zetu mbali mbali. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, kwa kuwa serikali inajitahidi sana kuwaajiri watu wenye ulmavu.

(a) Je, watu wenye ulemavu walioajiriwa wote mmewapa kipaumbele gani kuhakikisha kwamba wote wana Bima ya Afya?

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, serikali itakapoanza utaratibu wa kutoa Bima haitojali mtu ambaye ana ulemavu au hana ulemavu. Kwa maana hiyo ni kwamba, utaratibu huo utakapofikia watu wote bila ya kujali ulemavu wao na itikadi zao watapatiwa hiyo Bima ya Afya.

Nam. 44

Juhudi za kuwasaidia vijana na dawa za kulevya

Mhe. Zulfa Mmaka Omar (Kny. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis):- Aliuliza:-

Vijana ndio uti wa mgongo wa Taifa letu, lakini vile vile ndio nguvu kazi na Taifa lolote hutegemea sana vijana katika kuleta maendeleo. Hata hivyo, sasa kumekuwepo na wimbi kubwa la utumiaji wa dawa za kulevya ambapo vijana wengi hupoteza muelekeo na taifa kupoteza nguvu kazi.

(a) Je, Serikali inachukuwa juhudi gani kuwanusuru vijana hao.

(b) Katika kuwarekebisha tabia vijana ambao wameshaathirika na madawa ya kulevya, Serikali imeshaanzisha nyumba ngapiza kurekebisha tabia (*Sober House*) ambazo zinamilikiwa na Serikali kupitia Wizara husika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri, hayupo muhusika na hakutoa taarifa, naomba suala lake liondolewe na tuendelee.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, majibu nafikiri serikali inayo hapo mezani. Nafikiri ungekuwa ukasaidia kujibu huku.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swala lake Namba 44 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala la dawa za kulevya kisheria na kisera ni suala ambalo la kitaifa na linasimamiwa na serikali kwa ujumla wake. Na kwa kweli Mhe. Spika, ni kwamba vijana ndio uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa letu. Hata hivyo, kumekuwepo na wimbi kubwa la utumiaji wa dawa za kulevya ambapo vijana wengi hupoteza mwelekeo na taifa kupoteza nguvu kazi.

Hivyo, Serikali itaendelea kuchukua juhudi mbali mbali za kuwanusuru vijana hao kwa kuandaa mikakati mbali mbali ya kuwawezesha kuepukana na jambo hilo ikiwemo mikakati ifuatayo:-

1. Kutoa elimu za athari za dawa ya kulevya kwa kutumia mbinu tofauti kwa jamii ikiwemo kuchapisha vitabu na mabango ya kuelimisha dhidi ya dawa za kulevya. Wizara yangu na Wizara inayoshughulikia masuala ya vijana SMT tumekubaliana kufanya ujumbe wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya kuwa agenda ya kudumu ya kila mwaka katika ujumbe wa mbio za mwenge wa Uhuru. Kutokana na makubaliano hayo kauli mbiu hizo za mwaka 2015 zinazohusu "Uteja wa dawa za kulevya unaozuulika na kutibika, chukua hatua", na kauli ya mbiu ya mwaka 2016 inasema "Tujenge jamii na Utu wetu bila ya dawa za kulevya".

2. Wizara kwa kushirikiana na *UNFPA* kutoa mafunzo *study* ya maisha kupitia mkusanyiko wa vijana. Mafunzo yanatolewa kwa kupitia makongamano mbali mbali ambayo yanahusu taasisi zote za vijana ikiwemo zisizo za Kiserikali Unguja na Pemba. Vijana hao wamepewa mafunzo mbali mbali ikiwemo ushauri nasaha wa kutunza afya zao kwa ujumla. Mwaka 2015 jumla ya vijana 5000 (Unguja 3000 na Pemba 2000) walipatiwa mafunzo hayo.

3. Vile vile, Wizara inawahamasisha vijana kujiunga katika vikundi mbali mbali vya ushirika ili kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na fursa zilizopo zikiwemo za mikopo nafuu ili kupata mitaji ya kuanzisha na kuimarisha shughuli zao za uzalishaji ili kujipatia ajira.

4. Wizara imeandaa Sera ya maendeleo ya mwaka 2005 na kuifanyia mapitio mwaka 2015 ili iendane na wakati. Sera imebainisha majukumu ya vijana wenyewe, jamii, taasisi za kiserikali, sekta binafsi na washirika wa maendeleo katika kunusuru na kumuelimisha kijana.

5. Wizara imeandaa Sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana kwa lengo la kuwashirikisha vijana katika kupanga, kutekeleza mipango mbali mbali ya maendeleo.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye vitoto (a) na (b).

a) Mhe. Spika, ni kesi ngapi za madawa ya kulevya zimeshatolewa hukumu katika Mahakama hususan *cocaine* na *heroin*.

b) Serikali ina mpango gani wa kuanzisha *sober houses* katika Kisiwa cha Pemba na tukiangalia kwamba watoto wengi sana wamejihusisha na madawa ya kulevya, lakini uwezo wao ni mdogo wa kujiunga nyumba hizi za

kuacha madawa ya kulevya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha nyumba hizo Pemba.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa swali la (a) ni la kitakwimu na Mhe. Waziri, anayejibu hapa si Waziri wa ile wizara inayohusika, lakini swali (b) linajibika. Mhe. Waziri, naomba umjibu swali la (b).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waiziri wa Kazi, Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri muhusika naomba kujibu swali kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la takwimu kama ulivyokwishalieleza nitaomba nimjibu kwa maandishi Mheshimiwa, ili kumpa takiwmu halisi za kesi ambazo zimefikishwa Mahakamani.

Hata hivyo, kuhusu suala la *sober houses.* Mhe. Spika, mpaka sasa Sera ya Serikali ni kuzisaidia *sober houses* ili ziweze kufanya wajibu wake. Na tumejenga kituo kikubwa chenye sifa za hizi *sober houses* hapa Unguja. Ushauri wake wa kufikiria kujenga na kituo kama hicho kwa upande wa Pemba ni mzuri na tutaufikiria. Lakini kwa sasa tutachukua kila jitihada kuhakikisha kwamba zile *sober houses* ambazo zipo Pemba na Unguja tunazisaidia ili ziweze kutoa huduma bora.

Ninakubali kwamba vijana wetu wanapata tabu sana kiuwezo katika kupata suala zima la kupata mafunzo katika *sober houses* kutokana na uwezo wao wa kifedha. Lakini niombe kwa viongozi wa majimbo na viongozi wengine wote walione jambo hili ni la jamii, ni sehemu yetu sote tushirikiane namna ya kuwasaidia hao na Serikali kwa upande wake itafanya kila bidii kuona inasaidia ili vijana wetu wapate mafunzo hayo na waepukane na tatizo kubwa hili la madawa ya kulevya.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nikupongeze Mhe. Spika, kwa kuikumbusha Serikali kwamba wana wajibu wa kuwajibika kwa pamoja. Lakini swali langu la nyongeza nilikuwa ninamuomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba, katika kipindi kilichopita cha Serikali hii kulikuwa kuna mpango wa kujenga kituo cha *sober house* chini ya Wizara ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais kaondoka peke yake katuachia afisi yetu, ninataka kujua kutoka kwa

Serikali kwamba kituo kile kimefikia wapi na je, kinajengwa na ufadhili wa Serikali ama kuna wafadhili ambao wanatujengea kituo kile.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Wanu, kama ifuatavyo.

Tumejenga kituo kikubwa sana kitakachoweza kutoa mafunzo mbali mbali kwa ajili ya kuwanusu watoto wetu kwa madawa ya kulevya. Siyo kama *sober house,* lakini ni *centre* kubwa ambayo licha ya kutoa mafunzo itatoa matibabu na mambo mengine ambayo yanahitajika kwa ajili ya kuwarekebisha watoto wetu kuepukana na madawa ya kulevya. Kituo kipo tayari na karibuni kitazinduliwa rasmi ili kiweze kuanza kazi ya kutoa huduma kwa watoto wetu.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Nassor Salim Ali, kwa swali la mwisho la nyongeza kwa wizara hii.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, Wakati Mhe. Waziri, anajibu swali mama alisema kwamba Wizara inajishughulisha sana kuwashajihisha vijana kujiunga vijana kujiunga ushirika na kuwapatia mikopo ili kuweza kujiendeleza katika vikundi vyao. Je, ni kiasi gani cha fedha zilizotengwa kuwapatia vijana hao na mpaka sasa ni pesa ngapi ambazo zimeshatumika kuwapatia mikopo vijana wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waiziri wa Kazi Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Nassor Salim Ali, kama ifuatavyo kwa pamoja.

Mhe. Spika, kutokana na *microphones* zetu hizi sikuweza kumsikia vizuri sana, lakini ninadhani nimelielewa suala lake, naomba nimjibu kutokana na vile nilivyoelewa.

Mhe. Spika, ni Sera ya Serikali na imeanzisha wizara maalum kusimamia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi chini ya Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Nia na madhumuni ni kuwawezesha

vijana wetu ili waweze kujitegemea na kuanzisha miradi mbali mbali ya maendeleo kwa maisha yao na kwa maslahi ya taifa.

Ni vijana wengi siwezi kumpa takwimu ambazo tayari wameshapewa pesa hizo na bado Serikali inapanga bajeti kila mwaka kusaidia jambo hili. Na imeanzisha Kamati Maalum kwa wafadhili na wahisani mbali mbali kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia vijana wetu hawa ili wapate uwezo wa kujiendeleza. Hata hivyo, Serikali imeanzisha Vyuo vya Amali ili licha kupata fedha hizi kuwafundisha vijana wetu waweze kusomea taaluma zao ili waweze kujiajiri na kuweza kufanya vizuri maisha yao.

Kwa hivyo, licha kutoa mikopo pia wanapewa taaluma na taaluma hizo wakati mwengine pia husaidia vifaa kwa ajili ya kujiendeleza na kupata manufaa makubwa ya uendelezaji ili kupambana na ukosefu wa ajira nchini, lakini wakati huo huo kuhakikisha kwamba vijana wetu wanajijengea uwezo waweze kujitegemea katika maisha yao.

Nam. 86

Utekelezaji wa Mtaala wa TEHAMA

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Zanzibar imeanza kutekeleza Mitaala ya Sayansi kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kutumia Kompyuta kwa wanafunzi wa Skuli za Msingi na Sekondari.

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wamenufaika mpaka sasa.

(b) Je, ni Kompyuta ngapi zinahitajika ili wanafunzi katika skuli zote Unguja na Pemba (Msingi na Sekondari) ili waweze kuwa na darasa la mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kutumia Kompyuta.

(c) Je, Wizara imechukua hatua gani kwa Skuli zilizokuwa hazina huduma ya umeme ili ziweze kunufaika na mitaala hiyo badala ya wanafunzi wengine kufundishwa na wengine kutokufundishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-
Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake namba 86, lenye sehemu (a), (b) na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Teknologia ya Habari na Mawasiliano au kifupi TEHAMA ni dhana pana sana ambayo inajumuisha matumizi ya vifaa mbali mbali vya habari na mawasiliano ikiwemo; redio, simu, televisheni, *MP3* na kompyuta. Teknologia ya Habari na Mawasilianoa ina umuhimu mkubwa katika kurahisisha kujifunza na kufundishia. Kutokana na umuhimu wake mtaala wa somo hilo umeandaliwa na unafundishwa katika ngazi ya msingi yaani darasa la tano na sita. Kuanzia mwaka 2015 somo hilo la TEHAMA limeanza kufundishwa kwa wanafunzi wote wa darasa la tano na la sita katika skuli za Serikali.

Pia, kupitia mradi wa TZ 21 uliotekelezwa kwa pamoja baina ya Wizara na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (*USAID*), skuli za msingi 246 na vituo 10 vya walimu vilipatiwa kompyuta kwa wastani wa kompyuta mbili kwa kila skuli. Kompyuta hizo zilitumika kwa kufundishia na kuhifadhia kumbukumbu mbali mbali za skuli kwa njia ya kielektroniki. Katika ngazi ya Elimu ya Sekondari, somo la TEHAMA linafundishwa kupitia skuli zenye mchepuo wa kompyuta ambazo ni Skuli ya Biashara Mombasa, Skuli ya Sekondari ya Kiembesamaki na Skuli ya Sekondari ya Utaani Pemba. Pia, zipo baadhi ya skuli za msingi na sekondari zenye kompyuta ambazo zinatumiwa kama ni visaidizi vya kufundishia au kwa kuweka taarifa mbali mbali za elimu na kwa matumizi ya kawaida ya skuli.

Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Jumla ya Wanafunzi 1,268 wa skuli za sekondari wamefaidika kwa kusoma TEHAMA tokea kuanzishwa kwa mchepuo huo katika skuli mbili.

b) Jumla ya kompyuta 8,360 zitahitajika, kwa wastani wa kila skuli kupata kompyuta 20 ikiwa skuli zote 418 ziwe na darasa la kufundishia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Mbali ya kompyuta, skuli zitahitaji kuwa na walimu waliobobea katika fani hiyo kwa wastani wa walimu sita kwa kila skuli. Juhudi ya kuzipatia vifaa vya TEHAMA skuli zetu zinafanyika kwa kushirikiana na wahisani mbali mbali. Kwa mfano Skuli ya Sekondari ya Kiembesamaki imepata msaada wa kompyuta 50 kutoka kampuni ya *ZTE* ya China.

Shirika la Simu la *ZANTEL* limiepatia msaada wa kompyuta 21 kwa ajili ya Skuli ya Sekondari Chasasa, kituo cha Walimu, Michakaeni kwa upande wa Pemba na Skuli ya Sekondari ya Biashara, Kituo cha Walimu cha Dunga, Kituo cha Walimu Mkwajuni na Kituo cha Walimu Kembasamaki na kituo cha Taifa cha Walimu kilichoko Beit el Ras. Pia, Taasisi 10 za elimu za

Pemba zimepata msaada wa kila skuli kompyuta 10 kutoka Shirika lisilo la kiserikali Ireland. Skuli hizo ni skuli ya Uweleni, Kiwani, Mauwani, Shamiani, Fidel Castro, Vitongoji, kituo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji, Chasasa, Utaani, Konde na Chuo cha Kiislamu Kiuyu. Wizara inayapongeza mashirika mbali mbali yanayosaidia juhudi zetu katika kuzipatia skuli zetu vifaa vya TEHAMA.

c) Kwa hivi sasa, Wizara haina uwezo wa kuzipatia huduma za umeme kwa skuli zote kutokana na gharama kubwa ya umeme. Hata hivyo, Wizara kwa kushirikana na Shirika lisilo la Kiserikali la *Powering pontial* la Marekani limetoa msaada wa vifaa vya TEHAMA kwa skuli 16 za maeneo ya vijijiini vinavyotumia nishati ya jua. Skuli hizo ni Uzi, Kidoti, Kandwi, Pwani Mchangani, Tumbatu, Jongowe,Ukongoroni, Charawe, Kijini, Michamvi na Mbuyutende kwa Unguja na kwa Pemba ni Kisiwa Panza, Makongwe, Shungi na Fundo.

Wizara inaendelea na mazungumzo na Shirika hilo ili kupata vifaa vyengine vya TEHAMA vinavyotumia umeme wa jua kwa skuli nyengine 40 zilizoko vijijini. Napenda kutoa wito kwa walimu na wanafunzi kuvitunza vifaa hivyo ili viweze kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kwa muda mrefu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijampa Mhe. Ali Suleiman Ali, kuuliza swali la nyongeza, punguzeni kidogo sauti, kwa sababu nimeletewa karatasi kutoka kwa *crews* wetu wa *TV* kwamba sauti zenu zinatawala zaidi kwenye matangazo ambayo yanakwenda nje. Kwa hivyo, punguzeni kidogo.

Mhe. Ali Suleiman Ali kwa swali la nyongeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza ninaipongeza Serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba vijana wetu au watoto wetu wanapata elimu kutokana na wakati tuliokuwa nao. Lakini pili Mhe. Spika, niseme tu kwamba nawapongeza Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri na wizara kwa jumla kwa ghafla ya jana ambayo ni muhimu katika historia ya nchi yetu kutimia miaka 52 tumeona mengi na mafanikio yameyaona. (*Makofi*)

Swali langu lipo hapa. Kwa kuwa vijana wetu tunawategemea msingi na sekondari kupata mafunzo haya ya teknoloji ya TEHAMA, lakini tunaamini kwamba na kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, kwenye jibu lake, alisema kuwa wizara haina mpango wa kuziwekea umeme zile skuli ambazo hazina umeme kwa sasa hivi kutokana na hali ya kifedha, sina tatizo nalo. Swali langu ni hivi.

Je, kwa kuwa mkonga wa taifa tuliokuwa nao wa mawasiliano ambao Mhe. Simai Mohamed Said, mara nyingi huupigia ukelele kwamba utumike ili kuleta manufaa ya rahisi katika matumizi haya ya teknolojia tuliokuwa nayo. Wizara ina mpango gani kuutumia mkonga huu ili kuhakikisha kwamba matumizi yetu yanakwenda rahisi kuliko tunavyotegemea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa ruhusa ya Mhe. Waziri, ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Hivi sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeshaanza kuutumia mkonga huo wa taifa kwa kuunganisha baadhi ya Vyuo na Skuli. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mafupi aliyotoa kwenye swala lililopita. Mimi nilikuwa na swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, suala la mkonga huu *fiber optic* umekuwa ukizungumziwa sana na katika majibu mama aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, ni katika eneo ambalo litakuwa ni muhimu sana kutumika ili Wazanzibari kwenye maeneo tofauti waweze kufaidika. Ni lini mkonga huu utaweza kuunganishwa katika Vyuo Vikuu viliopo katika Jimbo langu la Tunguu hasa katika *State University* ya Zanzibar ambacho ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar pamoja na *Zanzibar University*. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri, ninapenda kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said, swali kama ifuatavyo.

Tumesema kwamba mkonga huu umeshaunganishwa katika *campus* ya Beil el Ras kama ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, lakini pia umeshaunganishwa pia na *campus* nyengine ya Tunguu. Kwa hivyo, ninadhani kwamba kazi ya kuunganisha na sehemu nyengine ya taasisi za elimu itafanyika wakati wowote pale hali itakaporuhusu. (*Makofi*)

Nam. 100

Kubadilika kwa Taaluma ya Ualimu

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa Ualimu ni taaluma inayokuwa na kubadilika kutokana na wakati, na mafunzo ya Uwalimu ni lazima yajengewe hulka ya kukubali mabadiliko na kujifunza. Kwa kuwa walimu wanapaswa kupata mafunzo ya kutosha ya awali na mafunzo endelevu, ili waweze kutekeleza vizuri kazi zao.

(a) Je, Wizara ina mipango gani wa kuimarisha mafunzo ya walimu na kuwapatia nyenzo za kutosha walimu wetu.

(b) Je, Wizara imejipanga vipi kuimarisha mifumo mbali mbali ya kitaalamu kwa ukaguzi na ushauri, pamoja na mifumo itakayosimamia uwajibikaji wa walimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 100, lenye sehemu (a) na (b). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa taaluma ya ualimu inabadilika badilika kutokana na mabadiliko ya maendeleo ya ulimwengu, na walimu wanahitajiwa kupatiwa mafunzo ya ualimu kazini na mafunzo endelevu, ili waweze kwenda sambamba na maendeleo ya taaluma yao.Wizara yangu inalifahamu hilo na imechukuwa juhudi kubwa katika kuwaendeleza walimu wakiwa kazini kwa kupitia vituo vya walimu 11, vilivyoenea katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Vituo hivyo vimefanya kazi kubwa ya kuimarisha uwezo wa walimu wetu ili waweze kutoa elimu bora.

Baada ya maelezo hayo sasa, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Katika mwaka 2015/2016, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Swiden imekamilisha ujenzi wa madarasa, maabara na kumbi za mikuatano katika vituo 8 vya walimu. Kukamilika kwa upanuzi wa vituo hivi vya walimu kumesaidia sana katika kuongeza

upatikanaji wa nafasi za kuendesha mafunzo ya ualimu kazini kupitia vituo vya walimu.

Pia, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kwa kupitia mradi wa "*Zanzibar Improving Students Project (ZISP),"* inakusudia kuendesha mafunzo makubwa ya walimu kazini, kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hesabati na Kiingereza katika madarasa ya msingi na sekondari. Kupitia mradi huu, vituo vya walimu vitakuwa na kazi kubwa sana ya kuendesha mafunzo ya ualimu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Aidha, wizara kwa kushirikiana na Shirika la "*Global Partnership for Education" (GPE)* na *"Madrasa Early Childhood Programme"* itaendeleza mafunzo ya walimu kazini, kwa walimu wa skuli za maandalizi, ili waweze kuongeza ujuzi wao na hatimae kutunukiwa vyeti vya kuhitimu mafunzo ya cheti cha walimu wa maandalizi.

b) Wizara kwa kupitia mradi wa *ZIPS,* inakusudia kufanya mageuzi ya mfumo wa ukaguzi, ambapo wizara inakusudia kuanzisha ofisi za ukaguzi wa kikanda, badala ya ofisi za ukaguzi kuwepo katika ngazi ya kitaifa tu. Hivi sasa, wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, imeandaa hadidu rejea za Mshauri Elekezi atakaetoa ushauri wa namna ya kufanyika mageuzi katika mfumo wa ukaguzi wetu, utakaoweza kuwafanya walimu wakuu na walimu kuwajibika zaidi katika utoaji wa elimu bora. Aidha, wizara inakusudia kuandaa Rasimu ya mswada ya kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Ahsante, *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b). Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa majibu mazuri ya kiualimu.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri, alisema kwamba, wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Global Partnership for Education* pamoja na *Madrasa Early Childhood Programme*, wanaandaa mafunzo ya wakuwapatia walimu hawa wa maandalizi waweze kuongeza ujuzi ili kuweza kupata vyeti vyao. Mbali na mafunzo hayo,

(a) Je, kwa kushirikiana na wahisani hawa au programu hizi, kuna mafunzo mengine ya ziada ambayo yanatolewa kwa walimu hawa?

(b) Wizara inakusudia kuleta mswada ili kuweza kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Je, mswada huu unategemea kuja lini katika Baraza lako tukufu?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika.

(a) Wizara itaendelea kutoa mafunzo, mbali na juhudi za wahisani. Lakini pia kutakuwa najuhudi maalum za wizara, nayo pia kujipiga ili kuweza kutoa mafunzo ya viwango mbali mbali katika tathnia ya ualimu.

Mhe. Spika, zaidi tutasisitiza katika mafunzo yanayohusiana, tunaita kwa Kiingereza *Instructional Leadership*, kwamba sasa mtizamo wetu hasa katika mafunzo ya uongozi wa walimu na walimu wakuu, ni namna bora wa kusimamia usomeshaji moja kwa moja. Sasa mafunzo haya tutayafanya sisi kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, mbali na juhudi za wahisani.

(b) Sasa hivi mswada upo katika hatua za wizara, watalamu wa wizara wanauchambua, hatimae tutawashirikisha wadau mbali mbali kutoa maoni yao, baada ya wadau utafuata katika hatua nyengine za serikali, kwa Makatibu Wakuu, Baraza la Mapinduzi.Kwa hivyo, hatuwezi kusema lini, lakini wakati hatua hizi zitakapokamilishwa basi mswada huo utakuja Barazani.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, na mimi napenda kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Waziri, serikali imetangaza elimu mjumuisho kuhusiana na watu wenye ulemavu, ili wajumuishwe. Lakini kuna baadhi ya walimu wachache ambao wanachukuliwa na wizara wanafundishwa na kupewa mafunzo ya kwenda kutoa elimu mjumuisho kwa watu wenye ulemavu, lakini baada ya kupata mafunzo walimu wale, wanakuwa hawataki kufuata au kusomesha elimu mjumuisho na hatimayake wanaomba uhamisho ili wapate kuhamishwa na kwenda skuli nyengine.

Je, wizara inawafikiria vipi walimu hao ambao wanafanya hivyo, au wizara inawapangia nini watu hao katika kuwawajibisha, ili waweze kufuata kazi ambayo waliokwenda kupewa mafunzo?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika. Kuanzia sasa mwalimu atasomesha somo alilosomea, hakutakuwa na uhamisho wa aina yoyote ambao utaruhusiwa. *(Makofi)*

Suala hili tumeshalisema kabla ya kuingia katika Baraza kwenye kufunga mafunzo, tulisema kwamba kuanzia sasa mwalimu atapimwa kwa somo alilolisomea, hata katika mafunzo madogo madogo ambayo tunatoa. Kwa mfano, kama haya ya elimu mjumuisho. Tutamfuatilia mwalimu huyo na tutamkagua mwalimu huyo kwa lile alilosomea. Kwa hivyo, napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wawakilishi sasa, walimu wa aina hiyo tutawatafuta na tutawarejesha katika skuli walizopangiwa na kusomesha fani walizosomea. *(Makofi)*

Nam. 59

Kituo cha Afya Chumbuni Kutumika Kama Kambi ya Wagonjwa wa Kipindupindu

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:-

Ahsante Mhe. Spika. Kwanza naomba kurekebisha jina langu ni Saada Ramadhan Mwendwa, sio Mwenda kama walivyoandika hapa kwenye orodha wa shughuli za leo. Naomba kuuliza swali langu namba 59. *(Makofi)*

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nne ya Mhe. Rais Idrissa Abdulwakil ilijenga kituo cha afya Chumbuni na kituo hicho ambacho kimeimarishwa kwa nyakati mbali mbali na viongozi wa Jimbo la Chumbuni kinahudumia wananchi wa Majimbo ya Chumbuni, Shaurimoyo na Jimbo la Mtopepo na pia kina huduma za kinamama na watoto hali ambayo inatoa faraja kwa wananchi wa maeneo hayo hasa kina mama. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni kituo hicho kimegeuzwa kambi ya kipindupindu kila kunapokuwa na mripuko wa maradhi hayo.

(a) Hivi Serikali kukifanya kituo hicho kuwa kambi ya kipindupindu haioni kwamba inaondoa dhana ya awali ya kuwapatia huduma bora wananchi wa maeneo hayo.

(b) Kwa vile maradhi ya kipindupindu yamekuwa yakiibuka mara kwa mara hapa Zanzibar, Serikali haioni kuna haja ya kutafuta eneo la kudumu la kujenga kambi ya kipindupindu.

(c) Je, Wizara yako ina mpango wowote wa kuwakinga wananchi jirani wa kituo hicho ili wasipate kipindupindu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Kituo cha Afya Chumbuni, kwa sasa ndio kituo kikuu kinachotumika kuhudumia wagonjwa wa kipindupindu, hasa kwa Mkoa wa Mjini na Magharibi. Fikra ya kukifanya Kituo cha Chumbuni kuwa kambi ya kipindupindu, ilipatikana baada ya kuona matokeo mengi ya wagonjwa wa kipindupindu, katika mkoa huu, yakitokea katika ukanda huo unaojumuisha maeneo ya Chumbuni, Shaurimoyo, Mtopepo, Karakana, Daraja Bovu na Mtoni Kidatu.

Mhe. Spika, taratibu za matibabu kwa wagonjwa hawa, zinakataza mgonjwa kusafirishwa masara marefu, ili kupunguza uwezekano wa kuambukiza watu wengine pamoja na uwezekano wa kupoteza maisha ya mgonjwa wakati akiwa safarini.Uamuzi huu pia umezingatia uwepo wa miundombinu sahihi kwa matibabu ya kipindupindu pamoja na uwepo wa vituo vyengine jirani, ambavyo wanachi wa maeneo haya wanaweza kupata huduma kama kawaida, zikiwemo za maradhi ya kawaida na zile za wanawake na watoto. Vituo vinavyozunguka eneo hilo ambavyo wananchi wanaweza kuvitumia, ni pamoja na Kituo cha Shaurimoyo, Sebleni, KMKM, Magogoni na Kituo cha Afya Kinuni.

(b) Mhe. Spika, wakati ilipoamuliwa kutumia kituo hicho kuwa ni kambi ya kipindupindu, matumizi ya kituo hiki yalikusudiwa yawe ya muda mfupi tu, wakati serikali ikiendelela na utaratibu wa kutafuta eneo jengine kwa ajili ya matibabu haya na mengine ya maradhi ya miripuko. Hii inatokana na ukweli kuwa eneo hilo sasa limekua finyu, hasa kutokana na eneo lake kubwa kuvamiwa na makazi ya watu. Mchakato huu bado unaendelea, na wizara itaacha kukitumia Kituo cha Chumbuni kwa matibabu ya kipindupindu, mara tu baada ya kukamilisha mipango ya ujenzi muafaka zaidi kwa matibabu hayo.

(c) Mhe. Spika, kwanza napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wote kuwa, kutokana na utaratibu uliowekwa na wizara, tahadhari kubwa zinazochukuliwa ili wananchi wa Chumbuni wasiwe katika hatari ya maambukizo ya kipindupindu, kutoka na uwepo wa kambi hiyo katika eneo hilo. Hii inatokana na ukweli kuwa wakati kambi ya kipindupindu ikiendelea, hakuna mwananchi wa kawaida anaeruhusiwa kuingia katika eneo hilo bure

bure, na kwa sasa eneo hilo limezungushiwa ukuta wa matofali kuhakikisha stara na udhibiti wa eneo hilo.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kinga ya maradhi ya kipindupindu kwa wananchi, wizara imekuwa ikiendelea na utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi wote juu ya kinga dhidi ya mripuko wa maradhi ya kipindupindu, ikiwemo kukosha mikono kabla ya kula, mara tu baada ya kutoka chooni, kuchemsha maji ya kunywa au kutia dawa ya *water guards*, usafi wa mazingira pamoja na kujenga na kutumia vyoo kwa haja zote. Elimu hii imekuwa ikitolewa kwa wananchi wote kupitia mikutano ya hadhara, skuli, vyuo vya qur-ani, taasisi za kijamii, vyombo mbali mbali vya habari na vipeperushi vinavyotolewa katika mikusanyiko mbali mbali ya kijamii.

Mhe. Spika, nyumba zote zinazotoa wagonjwa wa kipindupindu, hufuatiliwa kwa umakini zaidi, kuangaliwa mazingira wanayoishi, pamoja na kupatiwa elimu stahiki ili kuweza kujikinga na maambukizo hayo ya kipindupindu. Serikali ina tahadhari kubwa juu ya maisha ya wananchi wake na inawaomba wananchi wawe na hadhari ya maisha yao kwa kufuata kanuni za afya. Ahsante.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Ahsante Mhe. Spika. Pia, namshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Viongozi wa Jimbo la Chumbuni wanajitahidi sana na wanakiendeleza Kituo kile cha Chumbuni kwa ujenzi mbali mbali ukiwemo uzio, ili kutegemea huduma hii kuweza kuwasaidia wananchi wao wa jimbo hilo.

Je, serikali haioni kuwa kambi ile kuwepo pale inawanyima haki wananchi wa Jimbo la Chumbuni wanaoletewa maendeleo na viongozi wao katika jimbo lao?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza napenda nieleze kwamba wananchi wa Jimbo la Chumbuni ni wananchi ambao wamepata bahati kubwa sana, uwepo wa Kituo kile katika Jimbo la Chumbuni, umeifanya mpaka Umoja wa Mataifa kukielewa Kituo cha Chumbuni, umeifanya mpaka dunia nzima kukifahamu Kituo cha Chumbuni kwa kukipatia misaada mbali mbali, kwa kukipatia huduma mbali mbali na kwa kudumisha na kukiboresha kituo kile.

Pia, kituo kile kuwepo pale wananchi wa Chumbuni ni nafasi yao nzuri ya kuepukana na maambukizo ya aina yoyote, kwa sababu wakati kituo

kinapohudumia wagonjwa wa kipindupindu, serikali ina uhakika wa usalama wa wananchi wa Jimbo la Chumbuni, kwa sababu dawa ambayo inasaidia watu wasipate maambukizo hayo, basi inasikika harufu kwa Chumbuni nzima. Hii ni njia moja ya kinga na ni njia moja ambayo inasaidia kuhakikisha usalama wa wananchi wa Chumbuni. Nawaomba wananchi wa Chumbuni pamoja na wawakilishi wake musiwe na wasi wasi na hili, hii ni nafasi kwa kweli mmepewa na naomba muitumie.

Mhe. Spika: Mhe. Miraji Khamis, mwenye jimbo nimekuona kwa swali la nyongeza.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, katika majibu yake alisema serikali ina mpango, nashukuru sana na mara zote serikali ina mipango mingi. Mipango ya serikali huwa tunaiona kwenye vitabu, ikikiwemo kitabu kikuu cha bajeti ya serikali. Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

(a) Mpango huo aliousema unaonekana wapi ili wananchi wa Jimbo la Chumbuni waweze kwenda kuupitia na kuuona, ili kuhakikisha serikali inataka kujega kituo chengine kwa ajili ya kipindupindu ili kituo hiki kiendelee na huduma.

(b) Ulitaja umbali wa vituo vya karibu ambavyo kikifungwa hiki kwa ajili ya kipindupindu wanakwenda karibu. Lakini naomba unithibitishie, ni kituo kipi katika ulivyovitaja kipo chini ya umbali ya kilomita mbili, ili ile jamii ya Chumbuni wakifuate hicho kituo kilichokuwa na ukaribu, kama maelezo yako, ambapo pale kinapofungwa kituo kuna vituo vya karibu anapata. Lakini ni kituo kipi kwa wananchi wa Chumbuni chenye umbali chini ya kilomita mbili waweze kukifuata hicho, maana vyote vilivyobakia navifahamu viko kilomita tatu au na zaidi.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, majibu. Kwanza naomba uwashe kipaza sauti.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya:

(a) Mhe. Spika, serikali kweli ina mpango wa kujenga kituo chengine ili kuchukua nafasi ya kituo cha Chumbuni kwa maradhi yote ya mripuko.Kiwanja hiki kikubwa kimepatikana katika eneo la Tunguu. Wizara imeshakiangalia, imeshakithibitisha na kinachosubiriwa na

kupata uwezo wa kuweza kukijenga. Ni kiwanja kikubwa na kiko mbali na eneo la majumba ya wananchi. Kiwanja hiki kilianza kutafutwa baada ya kuibuka maradhi ya *Ebola* katika mataifa ya wenzetu, kwa tahadhari wizara ikaanza kukitafuta kiwanja hiki na imeshakipata na kiko katika eneo kubwa na mbali ili kuweza kutoa huduma. Mwenyezi Mungu akitujaalia tukipata uwezo basi tunaanza kukijenga.

(b) Mhe. Spika, naomba nimjibu sasa swali lake (b) kwamba, siwezi kukuthibitishia moja kwa moja kwamba ni kilomita ngapi, lakini katika maeneo ya Chumbuni ambao wanahudumiwa katika kituo kile pia wana uwezo mzuri wa kwenda katika kituo cha KMKM, pamoja na umabli uliopo lakini ukilinganisha na wenzetu huduma wanavyosifuata basi pale ni karibu, lakini pia katika kituoa cha Sebleni, pamoja na vituo vyote ambavyo nilivitaja mwanzo.

Nam. 158

Marekebisho ya Mshahara kwa Kada PHNB

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Tunaiponngeza Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa juhudi mbali mbali za kuwaendeleza Watumishi wa Wizara hiyo. Hata hivyo, kuna taarifa kwamba baadhi ya Watumishi wa Wizara hiyo wa kada ya *PHN GRADE B* wenye umri wa kazi wa zaidi ya miaka 15 kwa upande wa Unguja tayari wamesharekebishiwa mishahara yao.

a) Je, ni kwa sasabu gani Watumishi wa ngazi kama hiyo kwa Pemba bado hawajarekebishiwa mishahara yao.

b) Ni lini Serikali itawarekebishia mishahara Watumishi hao na kuwalipa malimbikizo yao ambayo wenzao wa Unguja wameshalipwa kuanzia Februari, 2016.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 158 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, katika mabadiliko yaliyofanywa ya mishahara, wapo baadhi ya wafanyakazi wa kada *PHNB* na

MCHA huko Pemba ambao bado hawajarekebishiwa mafao yao. Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba, Wizara yangu imeshawasilisha maombi ya wafanyakazi hao ya kubadilishiwa mishahara yao huko Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ufuatiliaji wa karibu unafanywa katika kuhakikisha wafanyakazi hao wanapata stahiki zao ikiwemo na malimbikizo yao.

Nam. 140

Kutangazwa kwa Msitu wa Ngezi:

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:-

Pemba tuna msitu mkubwa wa Ngezi kama wa Jozani na ukiwa na vivutio vingi sana. Je, ni lini msitu ule utatangazwa kwa watalii wanaongia nchini na kuimarishwa zaidi.

Mhe: Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 140 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ni kweli kwamba msitu wa Ngezi ulipo Pemba ni msitu wenye hadhi na una vivutio vingi sana kama ulivyo msitu wa Jozani ulopo Unguja. Misitu yote hii miwili inahifadhiwa kisheria na inatambulika kimataifa kutokana na wanyama waliomo na miti ya asili ambayo mingi yao ni ya kipekee duniani.

Mhe. Spika, katika kulijibu suala lake, Mheshimiwa, hivi sasa tayari kuna programu mbali mbali za kuutangaza kiutalii msitu wa Ngezi ambazo ziratibiwa kwa pamoja na Kamisheni ya Utalii Pemba, Shirika la Utangazaji Zanzibar na Idara ya Misitu iliyo chini ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar.

Madhumuni ya Programu hizi ni kuufanya Msitu wa Ngezi uweze kuvitia watalii wengi wanaofikia Kisiwani Pemba.

Mhe. Ali Khamid Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye (a) na(b).

Mara nyingi husika kuna tabia ya kukatwa miti kwa watu ambao wanapitia njia ya panya *road* katika msitu ule ulioko kule kisiwani Pemba.

a) Je, Wizara itatoa elimu gani kwa wahusika wanaokaa katike eneo lile ili kuona miti ile inabakia katika uhalisia wake?.

b) Kwa kuwa msitu ule uko Wilaya ya Micheweni Jimbo la Konde vipi kipindi ambacho msitu ule utaanza kwenye vivutio vyake wananchi wa jimbo lile watapata nafasi za ajira.

Mhe: Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

a) Naomba nimwambie Mhe. Muwakilishi kwamba, Serikali imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara kwa wananchi ambao wanaishi karibu na msitu ule kwa uhifadhi wa mazingira, yakiwemo kutokukata miti ovyo ovyo. Pia niseme kwamba Serikali imechukua juhudi ya kutoa elimu juu ya upandaji wa miti na wakati mwengine tumeshuhudia Serikali imeweka siku maalum ya upandaji miti kitaifa.

b) Kupitia fursa hii wananchi wa Wilaya ya Micheweni na walio karibu na msitu ule akiwemo yeye nimwambie kwamba sasa hivi wananchi wetu wapo vijana ambao wamekaa vikundi na wamejiajiri kupitia msitu ule, ni juzi tu nimetembelea na kuwaona vijana wameweka kikundi na kila gari inayoingia kwa kule Vumawimbi ambayo ni sehemu ya ule msitu wanatoza kodi na wanajipatia mapato kwa ajili ya kuendeleza kijiji chao kilicho karibu ya msitu ule.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali langu moja la nyongeza.

Pamoja na majibu uliyotupa uliyosema kwamba Serikali ina mpango wa kuutangaza msitu huu, ni sababu gani zilizowapa msitu huu kufikia hadi leo haujatangazwa.

Mhe: Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, kama nilivyojibu katika suala mama kwamba msitu huu unajulikana kimataifa, na ndio maana watalii wanapokuja Zanzibar msitu ule wanakwenda na kuangalia hali ya mazingira yaliyomo mle na vivutio vilivyomo mle ikiwemo miti ambayo duniani haipo inapatikana katika msitu ule.

Kwa hivyo, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, msitu huu tayari unajulikana kimataifa na niseme kwamba umeshatangazwa rasmi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu wa maswali umekwisha lakini kwa nguvu niliyopewa na Kanuni ya 39(3) nitazidisha muda usiozidi robo saa ili tuweze kuyakamilisha maswali tuliyonayo kwenye *order paper* leo kwa sababu ya kipindi kilichopita muda mwingi sana tuliutumia kwa kutokujibu maswali. Kwa hivyo, katika kufidia hali hiyo nitatumia hiyo Kanuni ya 39(3) ili kuweza kuhakikisha na baada ya hapo Wizara inayofuata katibu tafadhali.

Nam. 71

Barabara za Mradi wa Miva

Mhe. Machano Othman Said - Aliuliza:-

Katika kuimarisha juhudi za wananchi katika maeneo ya vijijini hasa yale ya Kilimo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, iliamua kujenga barabara kupitia mradi wa Miva. Hata hivyo, barabara hizo zimejengwa kwa kiwango cha kifusi.

(a) Kwa kuwa ujenzi wa barabara za kifusi hutupatia barabara ambazo hazidumu kwa muda mrefu. Je, Serikali ina mpango wowote wa kuzitia lami barabara hizo.

(b) Je, barabara ngapi Unguja na Pemba zimejengwa kupitia mradi huo.

(c) Gharama za mradi huo zilikuwa kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Barabara imedhamiria kuziimarisha barabara hizo kwa kuziwekea lami kwa kadri uwezo utakavyoruhusu, viongozi wa mfuko huo ulitembelea barabara hizo mwaka jana na kuahidi kulifanyia kazi suala hilo kwa awamu kwa kuanza na barabara za Pemba ambapo lengo kuu ilikuwa ni kutoa fursa kwa wakulima kuwezesha kupitisha mazao yao katika masoko hasa zao la karafuu.

Mhe. Spika, kuhusiana na suali la idadi ya barabara zilizojengwa hadi sasa zipo barabara 32 zenye urefu wa kilomita 148. (Unguja barabara 13 zenye kilomita 68 na Pemba barabara 19 zenye urefu wa kilomita 80). Kuhusiana na kipengele cha gharama za mradi wa ukarabati wa barabara kwa Unguja na Pemba ni shilingi bilioni tisa na milioni mia tano (9,500,000,000/=) Unguja bilioni 3.1 na Pemba bilioni 6.4.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza suala moja lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Katika majibu mama Mhe. Naibu Waziri, amesema kwamba kipaumbele za matengenezo wameweka kwa barabara za Pemba, lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri. Je, anaelewa kwamba barabara kutoka Mwakaje ambayo imeenda Mwachealale na Bumbwisudi tayari imebomoka sehemu mbili na karibu itakuwa gari haziwezi kupita.

a) Je, Serikali nayo imeweza kuweka uzito kwa barabara hii.

Inasemakana wakati wa ujenzi wa barabara hii Wizara ya Kilimo haikuwatafuta wataalam wa Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi katika hatua ya awali ambayo wangesaidia kuweka uimara wa barabara, hali ambayo imepelekea barabara zile kutokuwa imara.

b) Je, kuna *guarantee* yoyote iliyowekwa kati ya Wizara ya Kilimo na Mjenzi katika kushughulikia barabara hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Suala lake la nyongeza.

a) Mhe. Spika, ni kweli maneno ya Mhe. Machano kama alivyosema hatuna taarifa ya barabara hiyo kama imeachana, lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano tutaifanyia ukarabati wa kifusi kama kawaida.

b) Kama anavyosema tumetumia na tulikuwa tunao wakandarasi ambao walikuwa wapo kwa muda wa miezi mitatu kuzitizama barabara zile, bahati mbaya kwa vile muda ule umekwisha na tulichelewa kuzikabidhi katika Wizara ya Mawasiliano ndio yametokezea haya, lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano tutazitengeneza tena vile vile kwa kuwakabidhi wao kwa ajili ya hatua ya lami.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha leo hii kutukutanisha hapa leo hii tukiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Spika, kuna barabara hizi ambazo kuwa zimejengwa na mradi huo kwa kupitia Wizara ya Kilimo, barabara hizi hazikujengwa mitaro, kwa hivyo, zinasababisha wakati wa mvua kuingiza maji kwenye majumba ya wananchi.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuzifanyia mitaro barabara hizi ambazo kuwa zinawasumbua wananchi wakati wa kipindi cha mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi na Miundombinu: Kusema ukweli kama alivyosema mwanzo hizi barabara zimejengwa kupitia mradi huu, lakini zimejengwa kwa sababu ya lengo kuu la kurahisisha usafiri kuelekea katika masoko yale yaliyokuweko kule na bidhaa zinazotoka kule, imeonekana wazi kweli si barabara hiyo tu aliyosema Mhe.Viwe, kuna barabara nyingi Mhe. Mihayo Juma N'hunga alisema, Mhe. Machano amesema, sisi tumeshazipitia na tumezitizama kweli zina kasoro na tutakaa na wataalam wetu baadae baada ya kukabidhiwa hizo barabara tutazifanyia matengenezo. Na hapo uwezo utakaporuhusu kama nilivyojibu masuala yaliyopita tutaziwekea lami. Ahsante sana.

Nam. 85

Kujengwa kwa Daraja Kitope Mto Mchanga

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Kutokana na uchakavu wa madaraja ya Kitope Mto Mchanga, yapo katika hali hatarishi ya ukosefu wa vyuma vya kinga katika daraja hizo, kwa kuwa tatizo hilo lipo hadi leo.

Je, Wizara kupitia Mfuko wa Barabara imejiandaa vipi kuyajenga madaraja hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 85 kama ifuatavyo;-

Mhe. Spika, Madaraja ya Kitope, Mchangani, Kinyasini, Mto Mchanga na mengineyo yaliyoko kwenye barabara inayotoka Bububu - Mahonda –

Mkokotoni kupitia Kinyasini yatajengwa upya pamoja na ujenzi wa barabara kuanzia Kwanyanya kupitia maeneo niliyoyataja kwa mkopo wa Fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfBD).* Ujenzi huo utaanza mwakani (2017) na Serikali imeshaanza kutoa fidia kwa nyumba zinazostahili kulipwa ili Mkandarasi akichaguliwa aanze kazi mara moja. Hivyo, si busara kutumia fedha za Mfuko wa barabara kwa muda huu kwa kuwa hakujajitokeza athari kubwa sana ambayo itatufanya kuyatengeneza upya madaraja hayo.

Mhe. Ali Suleimani Ali (Shihata): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, jibu lake Mhe. Waziri, ametwambia kwamba wana mpango mkubwa wa kujenga madaraja yote, hilo halina tatizo, lakini pia amesema kwa kuwa hana mpango wa kufanya lolote kwa kuwa muda wa kujenga barabara utafika baadae. Suala langu liko hapa kwa kuwa barabara ya Kitope meli 13 ya Kitope yenyewe na barabara ya Mto Mchanga zote ziko sambamba tatu hizo, kinga zake zote zimeporomoka ziko chini na hatarishi wakati wowote inaweza kutokea, ana mpango gani wa dharura kutumia pesa chache sana kwa mabomba tu kuyaweka usalama kwa mabarabara yale kwa dereva anayetokea ayaone.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ni kweli kabisa kwamba haya madaraja yanatakiwa kufanyiwa ukarabati, lakini kama nilivyosema hapo mwanzo kwamba, gharama za kujenga kwa daraja lote lile basi uwe na pesa zisizopungua milioni mia mbili, tunaona matatizo na pale ambapo sehemu korofi tunahisi patahatarisha usalama wa wapita njia na wale wanaotumia barabara zile basi sisi huchukua hatua ya kitaalam ya kuifanyia matengenezo ya haraka barabara zile.

Kwa hivyo, mimi namtoa shaka kwamba wataalam wetu na wakandarasi wetu wakati wote wanakuwa wanazipitia hizi barabara na pale watakapohisi hii barabara inahatarisha maisha ya binaadamu na wanaotumia usafiri basi tunaifanyia mtengenezo ya dharura, kwa hivyo, asiwe na wasi wasi kwa hilo tutalikhakikisha kwamba halitotokea athari kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, *inshaallah.*

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, nami niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Mhe.Spika, niipongeze Serikali kwa jitihada yake ya kuweza kuendeleza barabara na kuona kwamba barabara zinapitika hasa katika maeneo ya vijijini.Lakini kwa masikitiko makubwa nataka kusema kwamba Serikali niishauri sana katika

Mkoa wetu wa Kusini kuna kijiji kile cha Miwani na bahati nzuri barabara yake ni mbaya sana, imefikia hatua kwamba hata kwa siku za jua basi pia haipitiki.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa angalau wa kuitia fusi barabara ile ya Miwani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasilino na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni karibuni tu tulikuwa katika ziara na Mhe. Rais, alitembelea barabara hii ya Jendele mpaka Kaebona Ungujaukuu na pale kulitokea malalamiko, mwananchi mmoja alielezea kuhusu hilo suala. Kusema la ukweli ile barabara ilikuwa katika *programme* ya mwanzo ya kujengwa kwa kupitia Mkandarasi wa Dishapria, lakini kutokana na kwamba fedha zilikuwa kidogo ile barabara haikuweza kuwekwa katika huo mpango. Sisi hivi sasa tukishakumaliza kujenga barabara hii ya Jendele mpaka Ungujaukuu Kaebona wale watu waliotupa ule ufadhili *BADEA* wametuahidi kwamba barabara ile ya Miwani mpaka Kizimbani watatafuta mkandarasi wa kuijenga. Kwa hivyo, mimi ninamwambia avute subira, lakini zile sehemu korofi ambazo sisi tunazijua tutahakikisha kwamba tunazifanyia matengenezo. Hilo ni agizo la Mhe. Rais na sisi tumesema kwamba agizo hilo alilolitoa juzi katika ziara yake tutalifanyia kazi ipasavyo. Ahsnate sana Mhe. Spika.

Nam. 149

Malipo ya Fidia kwa Ajili ya Ujenzi wa Barabara

Mhe. Maryam Thani Juma – Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein, alipotembelea katika Jimbo langu la Gando ameahidi kwamba muda mfupi ujao atahakikisha watu ambao hawajalipwa fidia kutokana na majumba yao kubomolewa kwa ajili ya utengenezaji wa barabara.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe.Spika, naomba kumjibu Mhe.Maryam Thani Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Gando swali lake Nam. 149 kama ifuatavyo:-

Mhe.Spika, nyumba zote zilizopisha barabara (*corridor*) tayari zimelipwa hatua inayofuata ni nyumba zilizoharibika baada ya matengenezo ya barabara tunaita

after corridor.Wizara tayari imeshafanya tathmini ya nyumba zilizoharibika baada ya matengenezo ya barabara. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, zimo katika hatua ya mwisho ya mazungumzo ya kutatua tatizo hili na tunamuomba avute subira ni karibuni tu hili suala litatatulika, *inshaallah*.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nataka nimuulize swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Je, ni nyumba ngapi ambazo zimeshatathminiwa na bado mpaka sasa hazijalipwa fidia.

(b) Je, umeshajione hali halisi ya nyumba zenyewe pamoja na tathmini zake husika kulingana na nyumba na hadhi za nyumba ambazo zimewekwa tathmini hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, ni kweli ni karibuni tu sisi wakati wa ziara yetu tulipita tukazikagua zile nyumba, sio nyumba zile tu, vile vile, tulipita Jimbo la Ole ambapo nao karibuni tu pesa zao milioni mia tatu wameshatengewa na wanalipwa. Hiyo alinihakikishia Mhe. Mussa Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Ole. Vile vile, Mhe. Waziri wa Fedha, alizipitia barabara zote tulipokuwa pamoja kule na akatuahidi, pesa pale ambazo sisi tunazifanyia tathmini ni milioni mia moja na thamanini na nne zisipopungua pesa hizo. Lakini kama utaratibu unavyosema tutazifanyia tathmini baadae tutawalipa wahusika kwa mujibu wa uwezo wa Serikali utakapokuwa tayari. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe.Spika, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, nichukuwe fursa hii pia kuipongeza Serikali kwa kuweza kujenga barabara zenye hadhi au zenye kiwango katika Kisiwa cha Pemba hasa katika barabara hiyo ya Gando na Wete/Konde. Mhe. Spika, mbali na ujenzi huo lakini katika majibu yake Mhe. Waziri, amesema tathmini za barabara za Wete/Gando. Lakini kuna barabara ya Wete/Konde je, katika tathmini ya Ole/Konde ni tathmini ngapi ambayo imefanya na wananchi wangapi ambao hawajapata kulipwa fidia yao katika barabara hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwanza kidogo napenda kumuweka sawa Mhe. Nassor Salim Ali Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kikwajuni. Barabara anayokusudia yeye ni Wete/Konde. Barabara ya Wete/Konde tayari tushalipa fidia yote isipokuwa tunadaiwa vipando na hivi vipando kama nilivyosema katika swali langu

nililojibu kipindi kilichopita kwamba, tunavifanyia tathmini. Ninamshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, kwa juhudi alizochukua Wizara kwake katika kukusanya mapato tumekuwa hivi sasa kabla ya kufanya matengenezo ya barabara yote kwanza tunawalipa fidia wahusika.Tumeshaanza kulipa Ole Kengeja na vile vile, tushaanza kulipa Bububu kuelekea mpaka Mkokotoni. Kwa hivyo, na hili kwa sababu yalikuwa ni madeni hapo kabla tunayafanyia tathmini na baadae wahusika tutawalipa kwa mujibu wa haki zao tunazotakiwa tuwalipe. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba kwanza nikutangazieni kwamba mara tutakapoahirisha hizi shughuli mchana wa leo Waheshimiwa Wajumbe, ambao ni kutokea CCM mtakuwa mna kikao na Mwenyekiti wa *Caucus* ya Wawakilishi wa CCM na baada ya hapo naomba sasa nimwite Mhe. Naibu Spika, ili aje achukue kiti kwa ajili ya kuendelea na shughuli zinazoendelea.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na Kuweka Masharti yaliyo Bora kuhusiana na Mambo hayo

(Kusomwa mara ya pili)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha mbele ya Baraza hili Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali pamoja na Kuweka Masharti Bora katika utekelezaji wa Sheria hizo.

Madhumuni ya Mswada huu Mhe. Naibu Spika, ni kupendekeza marekebisho ya sheria mbali mbali ambazo zinaonekana kwa sasa baada ya kupitisha kuna haja ya kufanyia marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, ni utaratibu wa kawaida wa kufanya marekebisho ya sheria kila inapohitajika kufanya hivyo. Marekebisho haya hufanywa kupitia Mswaada wa Sheria ya Marekebisho mbali mbali na kuona kuwa baadhi ya vifungu vya sheria hizo vinahitaji kufanyiwa marekebishao ili ziweze kukidhi haja ya kuanzishwa kwake na kutekelezwa kwa ufanisi.

Kiutaratibu mabadiliko ya sheria ni lazima yafanywe chombo hiki cha kutunga sheria ambacho ni Baraza la Wawakilishi. Hivyo, mswada huu unawasilishwa ili kuweza kukamilisha utaratibu wa kuzifanyia marekebisho sheria mbali mbali zilizoainishwa katika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu kiujumla una jumla ya vifungu 12. Kifungu cha Kwanza, Mhe. Naibu Spika, ni utangulizi ambao unazungumzia jina fupi la sheria na kuanza kutumika kwake.

Sehemu ya Pili, inahusu marekebisho ya sheria ya mahusiano kazini namba 1 ya mwaka 2005.

Sehemu ya Tatu, Mhe. Naibu Spika, inahusu Marekebisho ya Sheria ya Mahkama ya Mahakimu namba 6 ya mwaka 1985.

Sehemu ya Nne, Mhe. Naibu Spika, inahusu Marekebisho ya Mahkama ya Biashara namba 9 ya mwaka 2013.

Sehemu ya Tano, Mhe. Naibu Spika, inahusu Marekebisho ya Sheria ya Usambazaji wa Madawa ya Kulevya namba 9 ya mwaka 2009.

Sehemu ya Sita, Mhe. Naibu Spika, inahusu marekebisho ya Sheria ya Mashauriano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi namba 8 ya mwaka 2013.

Sehemu ya Saba, Mhe. Naibu Spika, inahusu marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma namba 14 ya mwaka 2015.

Sehemu ya Nane, inahusu Marekebisho ya Sheria ya Biashara namba 14 ya mwaka 2013.

Sehemu ya Tisa, Mhe. Naibu Spika, inahusu marekebisho ya sheria ya Chuo cha Kilimo cha Kizimbani namba 5 ya mwaka 2007.

Sehemu ya Kumi, inahusu Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo namba 4 ya mwaka 2012.

Sehemu ya Kumi na Moja, inahusu Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 2014.

Sehemu ya Mwisho, Mhe. Naibu Spika, ambayo ni sehemu ya 12, inahusu Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani namba ya mwaka 1998.

Mhe. Naibu Spika, maelezo ya kina ya ufafanuzi wa marekebisho ya kila sheria yameelezwa kwenye madhumuni na sababu ya mswada husika.

Mhe.Naibu Spika, kufanyika kwa marekebisho yaliyopendekezwa katika sheria hii inakusudiwa kufanya marekebisho kupitia waraka huu, kutaziwezesha taasisi husika na watumiaji wengine wa sheria hizi kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Hii inatokana na ukweli kwamba baadhi ya vifungu vya sheria hizo kwa sasa utekelezaji wake unaleta ukakasi na hivyo ndio dhamira ya kuleta Marekebisho ya Mswada huu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya marekebisho ya sheria yapo yatapitishwa yatawezesha sheria zilizofanyiwa marekebisho kuweza kutekelezeka kwa ufanisi na kukidhi haja iliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa sheria hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushirikiano wao wa dhati waliouonesha katika kutekeleza majukumu yetu, ikiwa ni pamoja na kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu.

Mwisho, Mhe. Naibu Spika, naomba wajumbe wa Baraza lako Tukufu wapiti, wachangie mswada huu na kukubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizi mbali mbali zilizopendekezwa ili marekebisho hayo yaweze kuwa ni sehemu ya sheria zilizopendekezwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante ninakushuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kusoma Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na Kuweka Masharti yaliyo bora kuhusiana na mambo hayo.

Mhe.Naibu Spika, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia afya njema iliyotuwezesha kukutana tena leo hii kujadili Mswada huu muhimu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

Mhe.Naibu Spika, aidha, baada ya kutanguliza shukrani hizo, sasa naomba kusema kuwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuleta Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na Kuweka Masharti yaliyo Bora kuhusiana na mambo hayo mbele ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kufanya marekebisho ya mapungufu yaliyomo katika Sheria hizo na vile vile, kuweka masharti bora ili kuenda sambamba na malengo ya kuwepo kwa sheria husika.

Mhe. Naibu Spika, pia, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wadau mbali mbali ambao Kamati yetu ilikutana nao kwa kuwashirikisha na kuweza kutoa maoni yao katika kuuboresha mswada huu muhimu katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala iliupitia mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka Masharti yaliyo Bora kuhusiana na Mambo hayo ambapo marekebisho mbali mbali yalifanywa na Kamati kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia umuhimu wa Sheria hizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba uwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Mjumbe
6. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Mjumbe
7. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf - Mjumbe
8. Mhe. Ali Khamis Bakar - Mjumbe
9. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
10. Ndg. Ali Alawi Ali - Katibu

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo Kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa

na kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe, tayari mmeshapatiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika Sehemu ya Nne ya Mswada huu inayohusu Marekebisho ya Sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar, Nam. 9 ya 2013, katika kifungu cha 8 cha sheria mama, Kamati inapendekeza kifungu hiki kiruhusu kama ambavyo inasoma katika Sheria Nam. 6 ya mwaka 1986 ya Sheria za Mahkama kiruhusu Mawakili kuweza kuingia katika Mahakama za mwanzo, kwa sababu Mahakimu kwa sasa watakuwa na Shahada na uwezo kwa Mahakama za mwanzo katika thamani ya kesi za madai.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, katika kifungu cha 9, Kamati inashauri neno "Mrajis" liondolewe na liwekwe "Warajis" ili aya hii iweze kusomeka kama nanukuu; "Naibu Mrajis atateuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa Manaibu Warajis wa Mahakama Kuu".

Mhe. Naibu Spika, katika Sehemu ya Kumi ya mswada huu inayohusu marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Nam. 4 ya 2012. Katika mareekebisho kifungu cha 33(c) kinachosomeka nanukuu; "Baraza la Mji litakua ni Chombo kinachojitegemea".

Mhe. Naibu Spika, katika aya hii, kwa kuwa Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zitapewa mamlaka za kujitegemea. Kamati inapendekeza kuzingatiwa mambo yafuatayo:-

i. Wakati Manispaa, Mabaraza au Halmashauri yatakapoona kuna haja ya kuwa na sheria ndogo ndogo zitakazo waongoza na kwa kuwa wameshapewa uwezo wa kujitegemea, basi wazingatie hali halisi za wananchi wa Miji husika na zitangazwe katika jamii ili zitambulike.

ii. Wazingatie kuwa lengo kuu la taasisi hizo ni kuhudumia wananchi na sio kujiendesha kibiashara, hivyo, sheria hii ibainishe shughuli za kimapato ambazo taasisi hizo zinaweza kuzifanya na sio miradi kwa ajili ya faida zao binafsi.

iii. Wahusika wa taasisi hizo wanashughulika na operesheni zote zinazohusiana na wananchi wapatiwe elimu ya kuwaelimisha wananchi na wageni, pia wapatiwe vitambulisho maalum ambavyo vitawabainisha kwa wananchi lakini hata raia wa kigeni wanaoingia nchini.

iv. Pia, katika taasisi hizo ziwepo sheria ambazo zitawabana watendaji wake pale ambapo watatenda makosa ya kinidhamu waweze kuchukuliwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, kamati inapendekeza hivyo ili kuona kwamba baada ya kupita sheria hii, Manispaa, Mabaraza na Halmashauri zitaweza kujiendesha na kupiga hatua katika kukabiliana na changamoto tofauti zilizomo katika jamii na zinazohitaji kuondolewa. Lakini, hata kiuendeshaji zinahitaji ufanisi ili kuweza kwenda sambamba na mfumo mpya tutakaoendana nao wa urasimishaji wa madaraka. (Ugatuzi).

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 36(t), Kamati yetu inashauri wizara husika kuweka utaratibu wa kuwashirikisha wataalam wa fani mbali mbali wanaohusiana na sekta ya mifugo wakati wa operesheni zao za kukabiliana na tatizo la mifugo Mjini. Aidha, serikali kupitia wizara inayohusika itenge maeneo maalum kwa wananchi wanaohitaji kufuga hasa kwa wakaazi wa mijini ambao hawana sehemu za kufugia kisheria.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kamati inashauri kuzingatiwa na kufuatiliwa kwa kina mazingira ya wananchi ambao wanafuga ndani ya majumba yao ambayo wanaishi na wamezungukwa na jamii ili kuepusha uchafuzi wa mazingira kwa usambazaji wa harufu mbaya za mifugo hiyo hasa katika maeneo ya Mjini.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 38(2), kamati inapendekeza kuwa pale endapo waziri atatumia uwezo atakaopewa kwa mujibu wa Sheria hii kulivunja Baraza, basi azingatie maslahi ya watu wa jamii husika na endapo maslahi hayo yamekiukwa basi alazimike kulivunja Baraza hilo. Aidha, kamati inaomba utaratibu wa kuvunja Mabaraza ikiwemo Manispaa wakati wa kuelekea uchaguzi mkuu ni vyema ilingane na muda wa kuvunjwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia tunaiomba serikali kuyazingatia na kuyafanyia kazi yale yote yaliyopendekezwa na kamati na wadau wa taasisi mbali mbali ambao kwa namna moja au nyengine wamesaidia kutoa maoni yao ili kufanikisha sheria hizi ili zitakapotumika ziwe na ubora zaidi. Kufanya hivyo, ni kusaidia serikali na taasisi husika kuepukana na udhaifu wa sheria zilizokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza haya machache, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wenye hekima na busara waweze kutumia uelewa wao wa kuuchangia na kuurekebisha mswada huu kwa kutoa mawazo yatayosaidia

kiutendaji ili kufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha kwa kupata ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kuweka kumbukumbu sawa pamoja na marekebisho ambayo kamati imependekeza katika kifungu cha 36(t) kwenye marekebisho ambayo wajumbe wengi wameyapata hakukuwa na baadhi ya yale mapendekezo ambayo kamati ilikubaliana na wizara, hayakuweza kuanishwa.Tulikubaliana kamati pamoja na wizara kwamba kuna baadhi ya maneno yaondoshwe ili sheria ile kuwa katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunaanza kuchangia na nimepata hapa mchangiaji mmoja tu, sasa kama wako ambao wana nia ya kuchangia walete majina yao ili nikija nikimpa huyu nafasi nijue najipima vipi kwenye muda ambao tulionao. Mkija mkiniletea mwisho msije mkasema Mhe. Naibu Spika, katunyima nafasi ya kuchangia, sijui mmenielewa. Kwa hivyo, naomba wale ambao wana nia ya kuchangia walete sasa hivi nipate kujipanga kwa shughuli nyengine.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kuweza kunipa nafasi hii na mimi nikawa ni mchangiaji wa mwanzo kabisa katika mswada huu wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, pia, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine kwa kuweza kutuamsha tukiwa salama, wazima na tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupa afya njema, lakini na wale wenzetu ambao wako vitandani wagonjwa basi Mwenyezi Mungu awape afueni.

Mhe.Naibu Spika, kwanza kabla sijaanza kuchangia mswada huu, nilikuwa tu naomba ofisi yako, Mhe. Naibu Spika, ofisi yako bado ina kazi kubwa kwa kuweza kutoa taaluma kwa Waheshimiwa Wajumbe. Wajumbe hawa wa Baraza hili bado wengi ni wapya na miswada kama hii ya marekebisho ya sheria mbali mbali kwa kweli inakuwa na mitihani mikubwa, kwa sababu inabidi mtu ahangaike kwenda kutafuta hizo sheria nyengine mbali mbali. Sasa bila ya kuwapa taaluma Waheshimiwa wako hawa inawezekana ukaja ukakuta kuna siku mswada Mhe. Waziri, anasoma mwenyekiti akimaliza na mswada unakuwa umepita. Sasa nilikuwa naomba sana elimu hasa katika miswada kama hii ni muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka moja kwa moja nianze katika ukurasa wa 42 wa mswada huu, Sehemu ya Tatu ya mswada ambayo inazungumzia Marekebisho ya Sheria ya Mahakama wa Mahakimu ya Nam. 6 ya 1985.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza naishukuru sana serikali, naishukuru serikali kwa kuweza kuona baadhi ya mapungufu katika Mahakama zetu na wakaleta miswada ya sheria ili tufanye marekebisho ili Mahakimu wetu wafanye kazi kwa vizuri, lakini vile vile na sisi wananchi pale inapofika pahala tumeteleza basi tuhukumiwe na watu ambao tayari wenye uwezo na wenye taalum na uzoefu wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa naangalia Sheria mama ya 1985, sheria hii Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 5(2), kifungu hiki kama ulivyosema mswada kinarekebishwa katika aya (a) kufuta neno “cheti” iliopo baina ya neno "na sheria" na kuweka badala yake maneno “shahada ya kwanza”. Sasa mimi hapa nilikuwa na maneno kidogo.

Mhe. Naibu Spika, moja katika wajumbe waliokuwa wakichangia sana katika hizi ngazi za Mahakimu ilikuwa ni mimi, nilizungumza sana na nilizungumza kwamba kwa mujibu wa sheria hii Nam. 6 ya 1985 ukienda katika tafsiri Mhe. Naibu Spika, tafsiri imewatambua Mahakimu kwamba labda niisome na hili tu pengine Mhe. Naibu Spika, pia ofisi yako naomba ijaribu kufanya marekebisho katika *library* yetu kupitia kwenye mtandao wetu wa Baraza kwamba, ukiangalia miswada yote ukienda ku-*google* basi unaikuta imeandikwa kwa Kiingereza. Sasa unajua madarasa yenyewe sisi ya tatu ya Mkoloni inakuwa kidogo shida, lakini nitajaribu hivyo hivyo kupitia pitia, kudurufu kidogo alau kutoa tafsiri ya Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia sheria hii ya Mahakama kifungu cha 2 kwenye ufafanuzi, nitasoma kama ilivyotajwa.

"Magistrate include Primary Court Magistrate, District Court Magistrate, Resident Magistrate, a Civil Magistrate and Honorary Magistrate".

Mhe.Naibu Spika, ukiangalia sheria hii Mahakimu imewatambua kuanzia Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo mpaka Mahakimu wa Mahakama za Mikoa pamoja na wale waliotunukiwa. Sasa lakini Mhe. Naibu Spika, ukiangalia sheria imefanyiwa marekebisho, mwanzo sheria ilikuwa inasema, "mtu ambaye atakayetangazwa kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo anatakiwa awe na *certificate* au sifa iliyokuwa inayolingana na hiyo *certificate".*

Kwa hiyo, hata akiwa na *diploma* kwa mujibu wa sheria hii inaonesha alikuwa anaweza kuajiriwa. Lakini ukiangalia *best practice* ambayo mnayozungumza wataalamu wa sheria kwamba, hawa Mahakimu wa Mahakama za mwanzo sasa hivi kwa Zanzibar nzima nadhani tuna kama 25, na hawa wameajiriwa wakiwa na ngazi tofauti, wengine *certificate*, wengine ngazi ya *diploma*. Lakini kutokana na hamu yao ya kufanya kazi wamejisomesha wengine sasa hivi tayari tuna Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo wana *masters*.

Mhe. Naibu Spika, kitu cha kushangaza mpaka leo kama hawa sifa yao ili awe Hakimu wa Mahakama ya mwanzo anatakiwa awe na *certificate*, leo ndio tunakuja kubadilisha awe na *diploma*. Leo tayari hawa wapo wana *masters*, lakini bado wako katika ngazi ya Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi nafikiri hii sio sahihi sana. Sasa mimi napongeza kwa hii hatua ya serikali kuleta haya marekebisho ya sheria kwamba, hawa Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo sasa hivi wawe na ngazi ya *diploma*, lakini pia nina maneno hapa.

Mhe. Naibu Spika, tuna uzoefu katika suala zima la Wizara ya Elimu, Wizara ya Elimu sasa hivi inawaajiri walimu katika ngazi ya *diploma*, lakini hawakuwahi kupitia shule kwenda kusomesha katoka chuo moja kwa moja anaingia kusomesha. Matokezeo yake sasa hivi kuna malalamiko na manung'uniko mengi kabisa na mpaka hivi karibuni Mhe. Naibu Spika, tuliwahi kukaa na chama cha walimu tukawauliza kwa nini leo wanafunzi wetu matokeo yanakuwa sio mazuri. Moja katika jambo walilotwambia kwamba utaratibu ambao uliokuwepo sasa hivi kumuajiri mwanafunzi moja kwa moja kutoka chuoni akawa mwalimu bila ya kwenda kufanya kazi kwanza akapata uzoefu, Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inakuwa ni mtihani. Sasa na hii sifa ambayo tumeiweka hapa ngazi ya *diploma* kwa Mahakimu ya Mahakama ya mwanzo, ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, isiishie hapo sifa hii kwanza alau afanye kazi kidogo, uko utaratibu wao pale anakuwa karani, anajifunza angalau miaka miwili au mitatu halafu baadae ndio anaapishwa anakuwa Hakimu wa Mahakama ya mwanzo. Pia, sio hivyo tu lazima tuweke na sharti katika kipengele hiki awe Mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini nikasema hivyo? Sizungumzi hivyo kwa ajili ya ubaguzi, hivi sasa Mhe. Naibu Spika, tuna tatizo moja kubwa Zanzibar. Kuna Mahakama ya Rufaa, na Mahakama ya Rufaa kwa mujibu wa Katiba ile ni Mahakama ya Muungano. Kwa hiyo, kunatakiwa Majaji zaidi ya wawili kama sikosei kwa mujibu wa sheria watoke Zanzibar, mpaka sasa hivi karibu miaka 15 tuna Jaji mmoja tu nafikiri Mhe. Mbarouk ni peke yake. Sasa hii inatokana

na nini? Kwa sababu kule ili sifa aende nayo kule anatakiwa awe na uzoefu karibu zaidi ya miaka 10, lakini vile vile awe ana *hold diploma*.

Mhe.Naibu Spika, sasa kwa nini tunashindwa kupeleka Majaji wa Mahakama ya Rufaa Zanzibar, kwa sababu hatuna *foundation.* Sasa ndio maana nikasema moja katika hii sifa ambayo iongezwe hapa pamoja na kwamba Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo awe ana *hold degree,* lakini vile vile afanye kazi apate uzoefu karibu miaka miwili mpaka mitatu na vile vile, awe Mzanzibar ili kutengeneza utaratibu wa Mahakimu wetu baadae kuwa Majaji ili waweze ku-*qualify* kuwa Mahakimu wa Mahakama ya Rufaa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele katika hiki kifungu cha 7 cha sheria mama ambacho kinarekebishwa na kuingizwa maneno “Kiingereza” baina ya neno “Kiswahili”. Sasa labda itakuwa pengine kuna tofauti ndogo kwenye mswada wa Kiingereza na Kiswahili, lakini kama nilivyosema kwamba hapa kwenye *Hansard* yetu tuki-*google* kwenye Baraza tunakuta miswada ya Kiingereza, lakini huku lilitangulizwa neno kwamba wanasema. *The language of primary court shall be Swahili*. Sasa hapa inatakiwa iongezwe na neno “Kiingereza”. Sasa sijui litangulie neno lipi hapa; itangulie kama ile ya mwanzo iliyokuwa inasema; "*shall be Swahili and English* au *English and Swahili"*.

Mhe.Naibu Spika, unajua wanasheria hawa Mahakamani pale wanaweza wakakufunga kwa *comma* tu, *comma* tu imekosewa basi hapo hapo ukachezea pingu. Sasa hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu, aje atusaidie tu kwamba je, kipi kitatangulia kwa sababu hii ya Kiingereza imesema "*shall be* Kiswahili", hiyo lugha lakini kimsingi sina matatizo nayo sana.

Mhe.Naibu Spika, lakini ukiangalia kifungu cha 10 ambacho tunakirekebisha (2) cha sheria mama kinarekebishwa na kufuta maneno “stashahada” au “diploma” iliyopo baina ya neno “shahada”.

Mhe. Naibu Spika, hapa tunaongeza ngazi nyengine vile vile katika hiki kifungu cha 10(2) labda kinasema kwamba; "*A person shall be qualified to be appointed a District Magistrate and shall not be qualified unless hold a diploma, hold degree in law and equivalent..."* na hayo mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, sasa na katika eneo hili vile vile, nilikuwa najaribu pia kushauri kwamba pamoja na kuwa huyu Hakimu wa Mahakama ya Wilaya sio tu awe na *hold degree,* lakini vile vile apate *experience* ya kufanya kazi. Hapa narejea lile lile la mwanzo Mhe. Naibu Spika, kwamba tunaweza tukamtoa

mwanafunzi chuoni akawa moja kwa moja ana *degree* yake akenda akawa Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ambapo atakuwa amekosa ile *experience*. Sasa hapa nilikuwa mimi pia Mhe. Mwanasheria Mkuu, aje atufahamishe katika hii kada yao ya taaluma ya sheria.

Kwa nini kusiwe na kigezo cha hawa Mahakimu wa Mahakama za Wilaya, kwa nini kusiwe na utaratibu wawe kama wanapanda daraja kutoka katika Mahakama za Mwanzo kupanda katika Mahakama za Wilaya. Kwa sababu kama nilivyosema mwanzo hawa tayari ile sifa ya kuwa Mahakimu wa Mahakama ya Wilaya wameshakuwanayo, kwa sababu kati ya Mahakimu 25 ni wawili tu mpaka sasa hivi ndio wana *certificate*, lakini wengi wao ni kuanzia *diploma*, *degree* na wengine wana-*masters*. Kwa hiyo, wao tayari wameshakuwa na sifa mpaka za kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mikoa.

Mhe. Naibu Spika, chengine nikirudi katika kile kifungu cha mwanzo kwenye kifungu cha 5(2) tulipokuwa tumezungumzia suala zima la kwamba kunabadilishwa utaratibu kuwa sasa hivi Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo awe na *degree*. Ukiangalia katika kifungu cha 8(1) cha sheria hii kinazungumzia kwamba katika Mahakama za Mahakimu wa Mwanzo hakutokuwa na Mawakili.

Mhe. Naibu Spika, naamini sababu iliyokuwa imewekwa kuwa kusiwe na ma-*advocates* kwa sababu wale mawakili mara nyingi wana taaluma kubwa kuanzia ngazi ya *diploma* na kuendelea. Lakini sasa kwa kuwa tayari umeshafanya marekebisho, kwa hiyo, Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo watakuwa wana *degree*, kuna sababu gani kusiwekwe na mawakili. Kwa sababu na wao watakuwa tayari wako *competent* kuweza kupambana na wale mawakili.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani na hili pia tulifanyie marekebisho ili sasa kufuta kifungu kile kinachosema kwamba kusiwe na mawakili, sasa waruhusiwe kuweko na mawakili. Kwa sababu unajua huko mitaani wakati mwengine ikiwa huna taaluma ya sheria na wengine ukifika Kituo cha Polisi tu futi zinakutetemeka, sasa unapofika pale katika Mahakama ya Mwanzo hakimu tayari ana-*hold a degree*, wana uzoefu kama tulivyoshauri. Sasa angalau akiwepo wakili kidogo anaweza akasaidia kutetea haki za wananchi.

Pia, leo tunarekebisha sheria, tunafanya marekebisho. Je, marekebisho haya yanaendana na hizi *qualifications*?

Mhe. Naibu Spika, nilipiga kelele sana wakati wa bajeti kuhusu stahiki na maslahi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Leo Mhe. Naibu Spika, mwaka 2003 tofauti na stahiki baina ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo na Hakimu wa Wilaya ilikuwa kama shilingi 50,000; lakini Mhe. Naibu Spika, sikufichi sasa hivi wanawapisha zaidi ya karibu shilingi 1,500,000. Hili ni tatizo kubwa, watu wetu, vijana wetu wameshajisomesha sana lakini bado maslahi yao hayaangaliwi. Sasa mimi ushauri wangu au napendekeza, sisi tutakubali tutarekebisha hii sheria kuwa sasa hivi Mahakimu wa Mahakama wa Mwanzo waanze na *diploma*, lakini na stahiki zao vile vile zilingane na hadhi yao vile vile na zile taaluma zao. Kwa hiyo, naamini Mhe. Waziri, ataweza kulisaidia hili kwa sababu bado nilimpa *challenge* katika bajeti labda ataniambia kwamba ile *scheme* imeshafikia vipi kuhusu hawa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa nataka nije katika kifungu cha 9, ukurasa wa 43, kinachofanya marekebisho kinasema kwamba;

"Kifungu cha 37 cha Sheria mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 37 kama hivi ifuatavyo:

"37. Naibu Mrajis atateuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa Manaibu Mrajis wa Mahakama Kuu".

Sasa hapa hatukuweka sifa, nadhani hapa pangelitakiwa pawe na sifa kwa sababu kama kule kwenye Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo tayari ile ngazi ya *certificate* imeshaondoka inakuja *diploma*. Sasa katika hii ngazi ya Manaibu Warajis wa Mahakama Kuu mimi nadhani vile vile kungelikuwa na *qualification* ikajenga ile heshima ya hizi ngazi.

Mhe. Naibu Spika, hapa haikutajwa, basi angalau tungelisema awe na *degree*, maana yake tukisema awe na *diploma* tutakuwa kama tunafananisha na kule kwenye ngazi ya Mahakama za Mwanzo, basi angalau tungesema awe na sifa ya ngazi ya *degree* na hii vile vile itawafanya wafanyakazi wetu wazidi kujisomesha kila siku kwa sababu hizi *posts* zinaambatana na elimu vile vile.

Vile vile, nikija katika kifungu cha 11 katika ukurasa huo huo wa 43 "Kifungu 4(2) cha Sheria mama kinarekebishwa na kufuta aya (a) na badala yake kuweka aya mpya (a) kama ifuatavyo:

"(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais".

Mhe. Naibu Spika, katika marekebisho ya sheria hii ya usambazaji wa madawa haramu ikiwemo madawa ya kulevya, sasa hapa hii nafasi ya mwenyekiti imetajwa tu atateuliwa na Rais. Mimi nadhani lazima tungeweka na *condition* vile vile, basi angalau kuwe na zile sifa kama awe muadilifu, awe hana mambo yanayotofautiana pengine na mambo ya maadili ya jamii.

Mhe.Naibu Spika, hii naizungumza kwa sababu gani, kuna kipindi tulikuwa tuna tatizo la Mahakama hizi za vileo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan, umebakiza dakika nne imeshakuwa muda mrefu sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hee! Haya nitajitahidi. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tuna tatizo kwenye Mahakama za vileo. Mahakama za vileo wananchi wamelalamika maana yake ulevi, lakini sasa yule aliyekwenda kuhukumu mwenyewe jioni anakwenda kuupiga pale pale. Kwa maana hiyo sasa, yeye haoni tatizo zile Mahakama za vileo kuweko mitaani. Sasa hapa ndio maana pamoja na kwamba tunaamini Rais na tukitunga sheria hatumuangalii Rais Dkt. Ali Mohammed Sheni tu, tunaangalia Rais yeyote, isijekuwa mtu pengine ana tuhuma za biashara hii pengine anauza anauza halafu akawa ndio yeye mwenyekiti, Rais akaja akamteuwa mwenyekiti.

Sasa nilikuwa naomba tu basi angalau hii ionekane pamoja na kwamba atateuliwa na Rais, lakini kuwe kuna *conditions* ambazo Mhe. Rais atakaposhauriwa na watu wake anataka kumteuwa bwana fulani, ataambiwa mh! Huyo kidogo alikuwa anaupiga upiga na mambo mengine, Mheshimiwa, ansema aa, huyu kwa mujibu wa sheria hafai. Sasa hiyo nadhani kidogo itaweza kusaidia, lakini vile vile awepo na makamu.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi wananchi wa Pemba wanalalamika sana kwamba, kuna kesi zinachelewa sana kule. Kwa sababu Hakimu mpaka atoke Unguja aende Pemba. Kwa hiyo, na hapa mimi nilikuwa naomba aweko mwenyekiti, lakini vile vile na naibu mwenyekiti ambaye yeye makaazi yake yatakuwa Pemba ili zile kesi za Pemba ziwe zinakwenda bila ya matatizo. Kwa sababu sasa hivi kesi za madawa ya kulevya Pemba zinakaribiana na Unguja na kwa sababu kule unajua maboti yanatoka Tanga, Mombasa, hivyo, hii shughuli kule imeanza kuharibika. Sasa nilikuwa naomba pia awepo naibu mwenyekiti ambaye makaazi yake yatakuwa Pemba.

Mhe.Naibu Spika, kwa haraka haraka, unajua nilikuwa najaribu kuogelea sana nilipoona Wajumbe wengine hawajajiandaa, sasa ndio nilikuwa nawapa muda kidogo waweze kujiandaa.
Mhe. Naibu Spika, naomba nimalize na mambo mawili, Sheria ya Mfuko wa Jimbo. Mheshimiwa, hatuna matatizo kubadilisha hicho kifungu cha kumuondoa yule katibu ambaye atateuliwa na mwenyekiti na baadae kuingia Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani iko haja kupitia marekebisho haya kwa nini tusiwatangaze wawakilishi na wao wakawa madiwani. Kwa sababu leo sisi tunavyojua madiwani wanayo Mifuko ya Wadi zao na wanapata pesa kila mwaka za maendeleo na wala sisi kule hatuingilii, lakini sasa hizi zetu leo tumeanza kuzipata mwaka juzi tunaambiwa sasa hivi Mkurugenzi wa Manispaa awe ndio katibu wetu. Kwa hiyo, ina maana sasa hivi yale mamlaka yetu tayari yameshaingiliwa na Manispaa.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Bara sheria zao za Serikali za Mitaa zimewatambua Wabunge kwamba ni Madiwani na sasa hivi kwa mujibu wa sheria hii tuliyoipitisha, Serikali za Mitaa zimepewa madaraka makubwa sana. Miradi mingi ya maendeleo fedha zitatoka moja kwa moja zitakwenda kwenye Halmashauri.

Mhe. Naibu Spika, sasa iko haja katika sheria hii lazima tuongeze kifungu kwamba Wawakilishi wa Majimbo na wao wawe ni madiwani ili tunapopanga mipango ya maendeleo na sisi tuangalie zile bajeti tunazozipitisha. Mfano kama Mfuko wa Barabara kwa ajili ya ujenzi wa barabara zetu za ndani ili tuweze kushiriki kikamilifu. Sasa hapo mimi nafikiri mambo lazima yaende sawa, isiwe ya kwao wao, na ya kwetu sisi yetu sote. Kwa hivyo, Wawakilishi na wao wawe madiwani katika Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa, mimi nampongeza sana Mheshimiwa mwalimu wangu Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kuleta haya marekebisho ya sheria. Kwa sababu alisikia kilio chetu tulilalamika sana na kunung'unika jinsi lile zoezi lilivyoendeshwa la ukamataji wa ng'ombe katika Mkoa wa Mjini na Magharibi. Sasa mimi nadhani kwa mujibu wa sheria hii kuwekwe mazingira, wenzetu hata nchi za Ulaya ukienda kuna ufugaji unaitwa *zero grassing*, ukienda katika mji mtu anafuga maisha yake anaishi kwa ng'ombe tu katikati ya mji lakini kwa kuwekewa *conditions* maalumu.

Sasa mimi kwa kuleta marekebisho ya sheria hii lakini tu labda lile neno 'kukataza' naona neno lile liko kali sana, maneno ya siku hizi neno 'hasi' kukataza. Mimi nadhani ingelisomeka "kuweka utaratibu wa ufugaji wa ng'ombe, kuku na udhibiti wa uzururaji wa wanyama kiholela", lile neno 'kukataza' tuliache. Kwa sababu unajua katika sheria unaweza kuweka neno moja lile lile watu waka-*violate* sheria kwa kutumia kifungu kile. Mimi nafikiri hapa tuweke *polite language* na tukiweka *polite language* tunawapa nafasi wananchi wetu waendelee kuchukua mikopo kwa ajili ya ufugaji kwa sababu anajua tutawekewa utaratibu na mazingira mazuri ya kuweza kufuga.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani ili usije ukanigongea kengele baada ya hayo machache niliyosema, nakushukuru tena kunipa nafasi hii, lakini naomba sana Mhe. Waziri, hasa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuangalia zaidi yale maslahi ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo hasa baada ya kuongeza na sifa za ku-*hold posts* hizo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii kuchangia kwa kifupi Mswada wetu huu wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali kama ulivyowasilishwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi ni jambo jema sana baada ya kutunga sheria tumeona wapi tunapata matatizo katika utekelezaji wa sheria zile. Kwa hivyo, naipongeza serikali mara kwa mara kuona wapi sheria zinatukwaza haziendi vizuri na kurekebisha ili ziweze kuleta tija katika utendaji wake. Kwa kweli kuna baadhi ya mambo mchangiaji wa kwanza kabisa Mhe. Hamza Hassan Juma, amenifilisi, lakini nitakazia tu hapa na pale, naomba niende moja kwa moja kwenye yale ambayo na mimi nimejikita.

Kwanza kabisa nataka kuchangia kwenye Chuo cha Kilimo Kizimbani, zaidi nasema nakwenda zote mbili Kiingereza na Kiswahili, lakini kwa upande wa Kiswahili ukurasa wa 46, kifungu cha 26(2), kinachosema, Marekebisho ya Kifungu cha 7:

Kifungu 26(2) kinasema kwamba:

"Baraza linaweza kuanzisha Kamati ya Utafiti na kamati nyenginezo kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za kamati".

Ni sawa, lakini nilikuwa naomba kuuliza tu, pale kituoni Kizimbani pana upande wa pili wa kituo wao wanajishughulisha na utafiti wa kilimo na mifugo. Sasa huu utafiti ulioelezwa hapa ambapo Baraza linaweza kuanzisha Kamati ya Utafiti utajishughulisha na mambo hayo tena au upande wa *academy* tu. Nahisi ingewekwa wazi kabisa kuepuka ule wasi wasi mtu ku-*interpret* kwamba wata-*duplicate* kazi za utafiti wa kilimo. Kwa hiyo, nashauri hapo Mhe. Mwanasheria Mkuu angetuwekea wazi hasa anakusudia kamati ile ni kamati gani, utafiti wa nini, naona ingekuwa vizuri pakawekwa wazi.

Halafu kifungu cha 27(a) "kwa kuingiza neno 'Mkuu' baada ya neno 'Mkurugenzi'. Chini kwenye kifungu cha 4, pia Mhe. Rais anaweza kuteuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu. Mimi nilikuwa nina mawazo mengine kuhusu hiki cheo cha Mkurugenzi. Unajua ile ni *institute* kwa Kiswahili ni chuo, lakini kwa hapa tunaposema Mkurugenzi kwa chuo kama kile kidogo naona hai-*fit* vizuri, bora tuseme Mkuu wa Chuo tu, tukisema Mkuu wa Chuo nafikiri inakidhi vizuri na hasa ukilinganisha kwamba vyuo kama vile vya kilimo na kwengineko wanaitwa ma-*principles* tu. Wenzetu Tanzania Bara, Kenya, wote *principle* tu, na halafu tuna lengo letu huko mbele kugeuza vyuo vile katika ile sheria mama ya *University*. Sasa nahisi kusema Mkurugenzi au Naibu Mkurugenzi naona kidogo hai-*fit in* vizuri, naomba Mwanasheria Mkuu hili aliangalie kama litaweza kukidhi haja.

Mhe.Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye sheria nyengine inayozungumzia marekebisho ya Sheria ya madawa na usambazaji haramu wa madawa ya kulevya iko ukurasa wa 43. Mimi nafikiri tulishazungumza sana hili suala kwamba, hakuna madawa ni dawa tu, kama za kutibu, za kulevya. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, naona mpaka kamati kidogo labda hawakuiona hii, nafikiri tuirekebishe ile sio "madawa" ni "dawa" za kulevya, za kutibu na nyenginezo.

Halafu kifungu chengine ni marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo. Mawazo aliyoyatoa Mhe. Hamza Hassan Juma, nakubaliana naye kwa kiwango fulani kwamba iko haja na sisi Wawakilishi tuwe madiwani. Kwa sababu kubwa hatusemi kwamba tunaiga kila kitu, lakini mazuri yanafaa kuigwa. Wenzetu Waheshimiwa Wabunge, nao ni madiwani na wanakwenda sambamba na madiwani katika kuleta maendeleo, wanaingia kwenye vikao vya kuwachagua Meya, Manaibu Meya na sisi iko haja tuingie, lakini kubwa kukaa kwenye vikao vya wenzetu na sisi tupange pamoja maendeleo, tuepuke ile migongano inayotokezea katika majimbo yetu kwenye kuleta maendeleo. Kwa hiyo, nakubaliana na yeye kwamba iko haja kweli na sisi tuingie kwenye vikao vyao.

Mhe.Naibu Spika, lakini kubwa lile lililopendekezwa kwamba Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa husika atakuwa Katibu wa Kamati. Mimi nilikuwa najiuliza tuchukulie mfano Katibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi 'B', sisi tuna majimbo saba, Wabunge karibu sita au saba, kwa hiyo, yeye ni katibu tayari kwa Mfuko wa Jimbo wa Wabunge yeye ndio katibu, na sisi Wawakilishi tunakuja saba, yeye pia atakuwa ndiye katibu wa Mfuko huo wa Majimbo katika majimbo yetu mengine saba. Kwa hiyo, chukulia saba ya Mbunge, saba ya Mwakilishi jumla 14 atafanya kazi vizuri kwa uadilifu huyo? Sasa kwa kweli naona kidogo kuna tatizo, hakutokuwa na uadilifu ila itakuwa tena inapitishwa mipango, yanapitishwa mapesa kwamba yatumike tu, lakini kwa kweli kukaa kwa uadilifu haupo. Kwa hiyo, naomba sana hili tulitizame.

Mimi labda ukiniuliza ushauri wangu mimi ningesema tuongeze kifungu ambacho au mtu yeyote atakayeteuliwa na kamati, bado ile kamati ipewe uwezo wa kumteua. Kwa kusema huyu ahudhurie kwenye vikao tupange kufanya kazi, kwa kweli sio rahisi, hasa ukilinganisha na kazi zake Mkurgenzi katika Manispaa zile au kwa kweli katika Halmashauri *is not practicable,* kwa kweli utendaji haupo. Kwa hiyo, nilikuwa na wazo hilo, ningemuomba sana Mwanasheria Mkuu nalo alitizame kwa undani zaidi hili.

Jengine nije kwenye mswada ule wa marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo kwenye kifungu cha 36 kifungu kidogo (26) yanayohusu suala zima la mifugo. Lakini kwa ufupi ni ile sheria inayozungumza cha Sheria mama ninarekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya (t) kama ifuatavyo:

" (t) kukataza au kuweka utaratibu wa ufugaji wa Ng'ombe, kuku, kudhibiti uzururaji wanyama kiholela...".

Sasa ukiangalia ya Kiingereza Mhe. Naibu Spika, kwa kweli iko *very strong* na naomba niikariri ya Kiingereza:-

"*Prohibition* (yaani unazuia kabisa) *or regulating grazing, poultry keeping,* yaani tunazuia mpaka ufugaji wa kuku, Mhe. Naibu Spika, *out span privileges, keeping animals and the controls of animals of any kind of whatsoever within specified areas of a Local Authority"*

Yaani hapa ilivyo tunampa *Local Authority,* kama Sheha au Diwani au yeyote, tunampa madaraka makubwa na ule ugonganifu utakaotokezea wa matatizo, hii sheria imeipa *room* kubwa sana kwa ninavyotizama kitaalamu kama alivyozungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, ufugaji tunao ule wa *free range* tunawaachia tu kama kuku wa kienyeji warande, wanachokula kutwa nzima

warudi wenyewe nyumbani. Lakini tunao ule *Intensive,* unaodhibiti kuku ndani ya banda unawalisha kila kitu na ng'ombe wa maziwa halikadhalika hivyo hivyo, unamchukua ng'ombe wake mmoja na ana uwezo wa kutoa hata lita 14 kwa siku, wengine wanafika hata lita 20 kadri unavyomlisha mwenyewe. Sasa yule unamuweka hatoki ndani ya banda tunaita *zero grazing*.

Sasa yule tunampiga marufuku aondoke, kwa mfano Fuoni, Kianga au Mwera ni maeneo ya ufugaji, kwa sababu umempa mamlaka huyo *Local Authority* yeye a-*regulate,* itakuwa ni ugomvi. Lakini mimi nataka kushauri kwa Kiswahili pale "kukataza au kuweka utaratibu wa ufugaji ng'ombe kuku" iondoke yote tuanze "kudhibiti uzururaji wa wanyama kiholela".

Tunaitaka ni ule uzururaji kiholela usiwepo, wale ndio tuwadhibiti, lakini sio tuzuie ufugaji. Leo mkulima wetu Fuoni au Mwera ana kuku 5 unamwambia asifuge, si tunatafuta ugomvi na wananchi wetu Mhe. Naibu Spika.

Kwa hiyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, hili alitizame kwa makini sana. Lazima tuangalie hali za wananchi wetu wanavyojitahidi kufanya kazi na ndio kama ninavyosema kupunguza umasikini mwengine anataka mayai mawili matatu kula ndani ya familia. Sasa leo unaposema unadhibiti, yaani unazuia, naona Mhe. Naibu Spika, hili namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu alitizame.

Kwa kweli mimi nilikuwa na michango hiyo midogo tu, lakini namuomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanasheria aitizame kwa undani zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu na mimi nitoe shukurani hizi za dhati kwa kunipa nafasi na pia niwashukuru Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi kwa pongezi zao nyingi walionipatia leo baada ya kusikia tangazo la kwenye redio kwamba jimbo langu la Tunguu katika maeneo ya Jumbi na Tunguu patakuwa panaitwa Jumbi Mji mpya pamoja na Tunguu mji mpya, kwa hiyo nasema ahsanteni sana.

Mhe. Naibu Spika, nikiri kwamba baada ya kuangalia maelezo mazuri ya kamati pamoja na kamanda wetu Mhe. Hamza Hassan Juma kutoa maelezo mazuri kabisa, na kufafanua mengi pamoja na rafiki yangu, mwalimu wangu, kipenzi cha Baraza hili Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, nikiri kwamba sasa

mengi ambayo nimekusudia kuyasema naona tayari wao wameshayazungumza na mimi sitapenda kurudia.

Lakini ningependa na mimi pia nichangie mawili matatu ambayo nimehisi yataweza kusaidia.

Kwanza tukienda katika hii ya *extra ordinary* ya Kiingereza kwenye ukurasa wa Nam. 196 pale panapozungumza *motor vehicle and other means of transport,* kwenye hiyo *box,* Ukiangalia kwenye *box* namba tatu inaposema *chaises machine number,* naona *spelling* ya *chassis* zimekosewa, kwa hiyo, nafikiri hapa parekebishwe *spelling* yake.

Halafu kwenye *Chart No.* 7 panapozungumza *personal uses\ business.* Ningeshauri hapa baada ya neno la *business* liondoke liwekwe *commercial*.

Lakini nikiendelea kuchangia Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha mabadiliko hichi kwenye sehemu ya 21 ambapo marekebisho ya Sheria, Maadili ya Viongozi wa namba 14. Kwenye hicho hicho kifungu namba (c) nikitizama kwenye mchoro inasema jina la Benki, taasisi za fedha *box* namba 2 nambari ya *account* na kama inavyoendelea.

Mhe. Naibu Spika, hapa tunataka sisi tujaribu kujenga utaratibu bora kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wa umma wanaweza kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na maelekezo kama inavyoeleza. Lakini pia kudhibiti hasa katika masuala ya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia ya Kiingereza na ya Kiswahili inataja jina la benki na tasisi ya fedha, maana yake kama ni benki ni *PBZ* ataandika ni *People's Bank of* Zanzibar, na akaunti yake atajaza na mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna kitu ambacho ni muhimu tukiangalie kwamba kuna suala la *official banking* na kuna suala la watu kufungua *official companies* ambazo hizi pia hazi-*disclose.* Lakini pia tuangalie kwa utaratibu mzima kwamba pia watu wanawekeza pesa kwa kununua *shares* katika makampuni tafauti.

Sasa katika *chart* hili mimi siridhiki kuona kama yule mfanyakazi wa umma akiamua kuwekeza pesa zake katika kampuni fulani utawezaje kujua kwamba Ali Juma, Bakari Joseph, Jesse, James, Silvestre Stalon, Antony Queen ana *shares* kiasi gani katika kampuni fulani. Kwenye *chart* hili haiwezi kuonesha hapa. Sasa hapa lazima upatikane utaratibu ni kwamba kinachoonesha pia

shares ambazo unazipata katika kampuni au usajili ambao yeye mwenyewe binafsi amewekeza katika kampuni ambazo zilizokuwepo ambazo zimo ndani ya nchi, nje ya nje pamoja na ambazo zimekuwa *registered* katika *shares* zake mwenyewe na zile ambazo zitakuwa zipo katika *offshore companies* na pia *offshore Bank accounts,* ikiwa zitakuwa ziko Mauritius, *Isle of Wight*, ambazo kuzigundua kuna utaratibu maalumu hata ikiwa ni Switzerland pia. Kwa hivyo, hapa naomba kidogo Mhe. Waziri atusaidie na kutuweka sawa katika hili.

Lakini nikienda katika marekebisho haya haya kifungu namba 40 juu ya marekebisho ya sheria juu ya kodi ya ongezeko la thamani namba 4 ya mwaka 1998. Katika kifungu namba 40 cha (iii) kinasema kwamba;

"Bila ya kuathiri masharti ya sheria, waziri ataweka utaratibu wa kanuni ya malipo ya *VAT* kwa manunuzi ya bidhaa kutoka Tanzania Bara" Ambayo pia kwa Kiingereza inasema kwamba';

(2) *Notwithstanding the provisions of this Act, the Minister shall provide procedures and regulations for payment of Value Added Tax for the supply of goods imported from Tanzania Mainland"*.

Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu wa kila Kampuni ya biashara mwisho wa mwezi wanatakiwa wao wapeleke kodi yao ambayo ya *VAT* ndani ya siku 14 kwa mujibu wa sheria ambayo imewekwa kwa nchi yetu.

Pia kampuni hizi zinatakiwa pia ziwasilishe katika hayo kwenye mauzo yao katika hiyo *VAT* wanakuwa na *input* na *output tax* yao. Hapa waziri anachotaka yeye kutuonesha na kumsaidia kwamba anataka zile kampuni ambazo zitakuwa zinanunua bidhaa au kupata huduma kutoka Tanzania Bara ambapo wale wanapokuja Zanzibar waweze ku-*claim* hiyo *tax* yao ya *VAT returns* mwisho wa mwezi ili aweze kuhakikisha kwamba halali inatumika na wao hawaibiwi au wanafaidika na hizo utaratibu mzima.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna kampuni ambazo ziko zinafanya biashara hapa Zanzibar, lakini pana *double standards* kuna kampuni zipo chini ya *Hotel Levy* wanalipa 18% na kuna kampuni hawa wamesajiliwa chini ya *VAT* ambayo wanalipa *VAT*. Lakini hizi kampuni ambazo zimewekwa kwenye *Hotel Levy* wao wanakuwa hawawezi kulalamikia ile *VAT* yao, ina maana hata kwa bidhaa ambazo na huduma ambazo wanachukua kutoka Tanzania Bara kuja hapa kwa manunuzi yao wanakuwa hawapati. Lakini ukiangalia katika marekebisho haya pia kuna kampuni zitakuwa zinatoka Tanzania Bara na kufanya manunuzi ya hapa Zanzibar, sasa ni utaratibu gani kwa hawa kampuni ambao watakuwa

kisheria watakaotoka kwenda zao moja kwa moja kupeleka mwisho wa mwezi wanapo-*submit* hizo *returns* zao za *taxes*, na kama wamefanya manunuzi Zanzibar kule wao watakuwepo *security* kwa upande gani.

Pia katika hapa anapozungumza Waziri kama ataweka utaratibu wa kanuni ya malipo ya *VAT* kwa manunuzi ya bidhaa kutoka Tanzania Bara, lakini tayari kuna makampuni hapa Zanzibar wanashindwa kupata kodi yao ya marudisho kwa ajili ya suala la *VAT*, kwa sababu wao wapo katika *Hotel Levy*, sasa hapa pana *double standard,* leo mmoja analipa 18% kupitia *VAT* na tayari anastahiki kulipa *VAT* na mwengine yeye halipii *VAT.*

Sasa mimi nataka Mhe. Waziri akija hapa kidogo atuwekee sawa juu ya suala hili, ili tuhakikishe kwamba tunapoondoka hapa wote hawa watafaidika kwa pamoja, na ili suala la *double standard* tuweze kulihakikisha kwamba halipo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo niliyozungumza, niseme tu kwamba mimi sikuwa na mengi, nadhani wenzangu wameshayachangia kabla na nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, na nitaomba sana Waheshimiwa Mawaziri watakapokuja watazweza kunijibu vizuri kabisa ili waweze kuniridhisha.

Ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nawashukuru Wajumbe na Mawaziri kwa kunisikiliza.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia mswada wa Marekebisho ya Sheria sheria mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza sana Mwanasheria Mkuu kwa kuleta mswada huu muhimu, na hasa tukizingatia kwamba lolote linalotaka kufanywa ili liende vizuri basi lipangie mambo mazuri au shughuli nzuri ili lifanikishe katika utekelezaji wake bila ya matatizo.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu una mambo mbali mbali ambayo yanafanyiwa marekebisho. Lakini mimi nitakuwa na machache sana hasa tukizingatia kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma aliyazungumza mengi na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame aliyazungumza mengi, na ndugu yangu Mhe. Simai Mohammed Said mazuri tu ambayo yote ya kuunganisha ubora wa mswada wetu huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitazungumzia mfuko wa jimbo. Mfuko wa Maendeleo ya jimbo ndio roho ya maendeleo kwa Mwakilishi, na usimamizi wake utaheshimiwa kwa pale atoyatekeleza ambayo yatajulikana na kuonekana. Lakini mfuko huu kwa bahati nzuri katika muundo wake wa sasa hivi katika kufanyiwa marekebisho haya naomba sana yapite. Tunasema tu kwamba utaelekezwa katika Manispaa au Halmashauri kuwa Wakurungenzi wetu ndio Makatibu wa kamati zetu ambazo tutaziunda.

Mhe. Naibu Spika, mimi hili sina tatizo nalo, hasa tukizungatia ili tufanye vizuri na serikali yetu iondekane na hasara ambazo hatuzitaki zitokee ni vyema pakawa na mkakati mzuri wa kusimamia hizi fedha kwa ajili ya utekelezaji katika majimbo yetu. Hii naipongeza sana sina tatizo nalo.

Ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, naungana na wenzangu, naomba sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa tunategemea sana kuwa sisi ni wasimamizi kama wenyeviti wa kamati hizi, na litakalofanyika lolote wewe ndio utajibu hoja baadaye, naomba na mimi niungane na wenzangu hapa tufikiriwe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuingie katika Kamati za Madiwani ili linalopangwa lolote twende sambamba kwa ajili ya hatima yetu ya huko mbele tunakokwenda.

Dhamana kubwa Mwenyekiti ndie unayehusika na Katibu ni mtendaji. Kwa hivyo ili kwenda vizuri kwa kuwa fedha zetu itakuwa iko katika Manispaa au Halmashauri, basi ni vyema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakafikiriwa kuingia katika kamati za madiwani ili twende sambamba katika kupanga mipango yetu tufanikiwe katika shughuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine na uzoefu nimeona katika mfuko wa wabunge. Mfuko wa Bunge mzuri unaenda vizuri lakini baadhi ya wakurugenzi wetu lazima wapewe taaluma nzuri, ili kuharakisha zile pesa zinapokuja zitoke ili zifanye kazi kwa maslahi ya wananchi wetu.

Kuna maeneo unaweza kwenda kwa Mkurugenzi ukatimiza siku tatu, nne, tano, mwezi au wiki mbili mpaka tatu humpati, leo kazongwa huku kesho yuko huku, na lengo na madhumuni yetu kuwa fedha hizi zikiingia zitolewe zipate nyaraka zake zinazokubalika kisheria ili kazi yetu ifanyike haraka, ili kuwaondolea shida wananchi wetu katika maeneo yetu.

Kwa hivyo, Mheshimiwa hili nalo namuomba sana Mwanasheria Mkuu aliangalie, kwamba wakurugenzi wetu wa Halmashauri na Manispaa wao ndio watendaji wetu wakuu katika shughuli hizi, wawe karibu na wawe haraka

haraka kufanya tathmini ya pesa zinazotaka kufanyiwa jambo lifanywe, ili tuendelee katika matumizi yetu ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nitalolizungumza hapa nakubaliana na ushauri wa wenzangu Mhe. Mwinyihaji Makame bado mimi niko kwa wafugaji.

Mimi naiunga mkono serikali, tena nasema hadharani hapa wafugaji wetu katika maeneo yetu wawekewe utaratibu mzuri wa kupata maisha yao, lakini si vyema tukaamua haraka kusema kwamba kuku asifugwe mjini, mbuzi, kondoo, ng'ombe hayo yanakubalika, kwa sababu mji wetu tukitizama katika ndani ya mji hata katika Manispaa yetu ya Mjini, mimi Mheshimiwa ninaunga sana mkono kuwa ng'ombe wasiwepo. Kondoo, mbuzi wote, lakini kuku bahati nzuri Mheshimiwa mtu anaweza kufuga nyumbani kwake kwa sababu anatafuta maslahi yake maskini ya Mungu ni kitoweo au wa kuuza mayai. Kama kuku hawa hawamuudhi mtu, hapo ninafikiria sheria tuiangalie tena, tuwaachie watu wetu hawa wenye kufuga ndani ya nyumba zao wafuge kuku wao wasiwabughudhi watu wetu.

Lakini Mheshimiwa ninaunga mkono ng'ombe. Ng'ombe, mbuzi na kondoo mjini wasiruhusiwe hata kidogo, yaani kuwemo katika maeneno yetu haya kwa sababu ya usalama wa gari zetu, wanaotembea kwa miguu na vyombo vya moto vidogo vidogo. Kwa sababu tulikuwa tunaiona huku nyuma tunakotoka na ilikuwa tafrani kubwa. Unaweza kupita *round about* ya Amani pale au kwa Marehemu Mzee Thabit Kombo ukakuta ng'ombe wamelala pale, anapita Makamu wa Pili wa Rais au anapita Rais mpaka waondoshwe, na siyo jambo zuri kwa tulikotoka. (*Makofi*)

Kwa hivyo hapa naipongeza sana Serikali, naipongeza Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kazi nzuri waliyosimamia kipindi hichi chote kwa kuondoa ng'ombe katika maeneo yetu ya mjini. Lakini maeneo ambayo tunasema kwamba bado wananchi wetu wapewe taaluma, naomba wapewe taaluma sana. Mimi siridhiki hata siku moja ng'ombe wale kuchukua magari ya ng'ombe, kwa kuchukua mchanga kwenye maeneo yetu mbali mbali.

Hapa ningeomba hii sheria ikawekwa sheria ya kumdhibiti atakayefanya kosa hili. Na ubaya uliokuwepo sasa hivi vijana wetu hawa wanaochukua magari ya ng'ombe ikiwa usiku ikiwa jioni wanajificha lakini wanakuwa na silaha za hatari, wanawatisha watu wetu na wanatumia mbwa wakati mwengine kuwa-*harass* watu wetu pindi wanapowaona. Naiomba Serikali hii sheria tungeongeza kifungu kwa yeyote atakayeruhusiwa kufuga ng'ombe wake katika

maeneo ambayo hawatakiwi ng'ombe wale wahangaike mitaani, kama kawafunga nyumbani kwake, katika uwa wake lakini akionekana ng'ombe na gari la aina yoyote akamatwe. Akamatwe ng'ombe yule na apewe adhabu kali mwenye ng'ombe yule, kama atataifishwa aende kule Hanyegwamchana akamkomboe huko, sheria ile bora iwekwe. Kwa sababu bado inawapa adha wananchi wetu, na inawapa usumbufu mkubwa katika maeneo, wachimba mchanga usiku na mchana. (*Makofi*)

Ningemuomba Mhe. Waziri anayehusika bado tuna vyombo vyetu vya Dola. Hivi vyombo vya Dola vipelekwe katika maeneo, mimi ninatangaza rasmi kwangu Kwarara. Kwarara bado kuna adha ya ng'ombe, yaani hawa vijana hata hawaeleweki wanatoka wapi. Kwa hivyo ningeomba magari ya ng'ombe sheria hii ikaweka kifungu ambacho kitatoa adhabu kali kwa mwenye gari la ng'ombe atakayechukua mchanga, atakayeharibu mazingira kwa njia yoyote achukuliwe hatua au atakayeingiza ng'ombe kwenye mashamba ya watu. Pia ni suala ambalo litatusaidia katika kuondoa adha hii.

Lakini kwa wale watu wasikivu ambao ninaamini Mhe. Naibu Spika, wamo watu watiifu kwa Serikali yetu hii, hawana matatizo katika ufugaji wao, hawana madhara katika ufugaji wa ng'ombe wao, wale wapewe taaluma zaidi juu ya kufanya shughuli zao za kila siku, hasa tukizingatia kwamba watu wetu ni wanyonge. Kama kuna msemo mmoja Mhe. Hassan huwa anapenda kusema "*Wakwezi na Wakulima*", maana wakwezi na wakulima pamoja na wafugaji ndiyo wakulima wenyewe. Changamoto hii hata Serikali imejitahidi sana kutafuta ng'ombe wa kupandishia mbegu fulani kwa ajili ya kupata watu maziwa na mambo mengine, lakini sikubali ng'ombe kuzurura mjini, hilo na mimi ninaunga mkono hata siku moja sikubaliani nalo.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, jengine ili tuendelee tunahitaji mambo mbali mbali ya makusanyo ya fedha zetu na kuwa salama katika fedha zetu. Kwa hivyo sheria imesema tu kwamba kuna watu watakaohusika ambao wengine wana fedha zao katika mabenki ya nje, wana mambo ambayo wamejiwekea nje. Hii itakuwa shughuli ambayo Serikali ikisimamia vyema na kuwekeza vizuri tutajua hatma ya fedha zetu na utumiaji wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande wangu nilisema mapema tu kwamba naiunga mkono sheria hii na ninaiomba ifanye kazi vizuri, lakini nimesema tu ninamuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu tuje suala la Kamati zetu za Maendeleo au Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo utakuwa chini ya Mwenyekiti wake Mwakilishi, lakini Katibu ni Mkurugenzi wa Manispaa, wenzetu wajumbe wataingia Madiwani, basi na sisi tuunganishwe kwenye vikao hivyo,

ikiwa tutakuwa wajumbe ama tunaingia kwa kazi maalumu ya kupanga maendeleo yetu kwenye maeneo yetu.

Baada ya hayo naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja na naomba ng'ombe wanaozurura wachukuliwe hatua, ng'ombe wanaoachiwa mashambani mwa watu wachukuliwe hatua. Anayekutwa kachukua mchanga popote pale katika maeneo hasa kwangu Kwarara, ninazungumzia sana kwangu mimi kwenye jimbo langu akamatwe mtu huyo mara moja na adhabu aipate.

Ninashukuru ahsante sana na ninaunga mkono Mswada huu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata sasa hivi ni Mhe. Miraji Khamis Mussa na baada ya hapo nitampisha Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Said Soud Said, na atakayefuata mchangiaji wa mwisho ni Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa Mswada huu.

Kwanza niipongeze Kamati na niipongeze Serikali pia kwa kuuleta Mswada huu kwenye Kikao hichi cha Baraza lakini pia niipongeze zaidi Serikali.

Katika eneo hili la marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo, ninaipongeza Serikali kwa sababu kwa azma yao njema ya kulinda pesa za wananchi.

Mhe. Naibu Spika, hapa Serikali imetafuta dawa nzuri ya kuzitumia pesa vizuri na kufika kwa wananchi tuliowakusudia. Ninayasema haya kwenye eneo hili la marekebisho haya na kutilia mkazo zaidi, ili wenzangu washawishike zaidi kupitisha hapa katika kifungu hichi bila ya tatizo lolote na marekebisho yoyote. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tukifuata katika kitabu cha 2013/2014 cha matumizi ya Mfuko wa Jimbo ambao kila Mhe. Mwakilishi alipewa lakini sisi Kamati ya *PAC* ndiyo tulipewa zaidi, kwa sababu tunataka kuzifanyia kazi. Karibu majimbo hamsini basi wana sehemu ya kujibu hoja. Na hoja iliopo mbele ni matumizi yasiyoridhisha ya pesa hizi, ambazo lengo kuu ni kufikia kwa wananchi wetu. Hivyo niipongeze Serikali katika eneo hili kwa kutafuta njia mbadala ambapo sasa hivi tukienda katika Serikali za Mitaa, kama sisi kule mjini tutakwenda Manispaa, tutapewa sheria za manunuzi kwa pamoja tutazifuata ili miradi yetu ifuate utaratibu mzuri na iidhinishwe kisheria.

Kwa hivyo mimi hapa ninapenda sana kuwaambia wenzangu, ili kupunguza kuja kuwakagua, pengine nitakuwa ni Mwenyekiti wa *PAC* hapo, basi ni vyema tukaridhia kifungu kikawekwa kule ili matumizi haya yaende kwa mujibu wa sheria na utaratibu utakaopangwa kwa kushirikiana na taasisi zetu za Halmashauri na Mabaraza ya Miji.

Kwa hivyo ninawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi dawa hii iwe inatumika kwa sote na tuifute ili tuisaidie Serikali, lakini tutawasaidia zaidi wananchi wetu katika kufikia malengo mazuri ya matumizi ya fedha hizi. (*Makofi*).

Lakini baada ya hapo naomba niungane na wenzangu pia kwenye wasi wasi wangu kidogo, lakini akiinuka Mwanasheria Mkuu anaweza akatupatia ufafanuzi wa ziada kwenye marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, hasa pale kwenye Rais anaweza kuteua Naibu Mkurugenzi. Kwa kuwa Serikali ina Mswada ambao upo mbele yetu wa SUZA ule wa kuja kuviunganisha hivi vyuo, sijui leo tukipitisha marekebisho haya na keshokutwa tunakuja kuviunganisha, ninajua vyuo vyote vitakuwa chini ya Makamu Mkuu wa Chuo na Mkuu wa Chuo ambaye ni Rais. Sasa hawa wengine *levels* za Wakurugenzi au Manaibu Wakurugenzi kule huwa hawateuliwi tena. Sasa sijui ufafanuzi huu tukishapitisha hili litasimama vipi kisheria.

Sasa nilikuwa ninamuomba Mwanasheria Mkuu kunako maeneo haya mawili Kifungu hichi cha 27 (a) na (b), na namba 4 ile chini pale aje atusaidie.

Baada ya hayo huku kote sina mashaka na Mswada huu na ninaomba niuchangie kwa ufupi na niunge mkono kuwepo kwa Mswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ahsante ninakushukuru sana. Sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Said Soud Said) na baada ya hapo atakuja Mhe. Sheha Hamad Mattar na baadae atachangia Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, Serikali inapotengeneza utaratibu wa marekebisho ya sheria huwa inaelekeza faida kwa wananchi ili waondokane na zile shida mbali mbali. Kwa maana hiyo ni kwamba marekebisho haya yamelenga kuwafanya Wazanzibari watambue umuhimu wa Serikali yao na kuelewa hoja ya afya, kwamba ni muhimu zaidi katika kuendeleza harakati za maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi hoja ya wafugaji wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kuendelea kufuga ng'ombe kati kati ya miji, punda, mbuzi na hata kuku walio wengi kama wale walio ndani ya mabanda.

Ningeshauri tu kwamba waelewe kuwa wakati huo umepitwa na wakati, na sasa ni wakati muafaka wa kuelewa kwamba Serikali iliopo madarakani ina nia nzuri ya kuwafanya watu wawe na afya kwa kuepukana na maradhi mbali mbali yanayosababishwa na mifugo hii.

Mhe. Naibu Spika, wakati nikiwa skuli niliwahi kusomeshwa kwamba ng'ombe anasababisha maradhi ya *tuberculosis.* Hata hivyo dunia leo inatangaza mafua ya ndege, licha ile ya *TB* lakini pia kuna mafua ya ndege. Sasa unapoweka ng'ombe wa maziwa katikati ya mji, halafu ng'ombe yule akawa ana *smell* ya mambo mbali mbali ya vyakula vyake, haja zake anazokwenda nazo na hatimaye na hewa yake.

Pia inaweza kuchangia kuleta matatizo ya majirani pamoja na kwamba wewe unajipatia maziwa na kupata faida, lakini inaonekana wazi kwamba faida yako ni hasara kwa jamii.(*Makofi*)

Kwa hivyo ni vizuri sasa wananchi wakakubali utaratibu wa kufuga ng'ombe, kuku, mbuzi na yale yote ambayo wenyewe wanahitaji, lakini nje ya miji na siyo ndani ya mji. Kwa sababu haya yanafanywa na mataifa mbali mbali duniani. Watu wanaweka maeneo mbali mbali kwa ajili ya kufuga mifugo yao ili isiwe karibu na jamii, na kuepusha yale maradhi ambayo yanaweza yaka-*spread* na wananchi wengi wakapoteza maisha kutokana na hoja hii. Na pia ni wakati muafaka sasa hivi Mhe. Naibu Spika, kwamba mifugo hiyo nayo pale itakapowekwa basi ni vizuri watu wakawa tayari kugharamia namna ya kutengeneza majosho, madawa na chanjo ili kuepuka ku-s*pread* maradhi ya wanyama wale kwa wananchi wasio na hatia.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo ni vizuri pia wananchi wakaelewa kwamba hoja ya kuondoa mifugo ndani ya miji, serikali inaendelea na utaratibu wa kutangaza sekta yake ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, katika Miji yetu ya Chake Chake, Wete na Mkoani basi huwezi ukaenda hatua ishirini bado hujaruka kinyesi cha ng'ombe au cha punda, mbuzi, jambo ambalo lilikuwa linailetea tabu sekta hii ya utalii Kisiwani Pemba. Lakini baada ya sheria hii kuzuka na utaratibu mzima ukapangwa juu ya hoja hii, leo hata ile gari ya ng'ombe pale Chake Chake imekuwa ni historia haiingii mjini. Kwa nini haiingii mjini, kwa sababu ni

jambo la ajabu kwamba wewe una ng'ombe umempakia mchele, sukari na vitu vyengine, lakini ng'ombe huyo unamzuia asimgonge mtalii anayepita barabarani. Kwa hivyo mambo haya yalikuwa yanakwenda kienyejienyeji, tulikuwa tumebeba ule utaratibu wetu wa kufanya kazi kwa mazoea na tukashindwa kuiwekea *discipline* Serikali, tukashindwa kuweka *discipline* ya vile ambavyo vinafanya Serikali yetu kupata mapato. Kwa hivyo mambo haya ndani ya utaratibu huu yamejenga sifa ya kwamba umefika ule wakati wa kutembea pale katika miji yetu bila ya kuruka vitu kama hivi ambavyo nimevitaja.

Hata hivyo Mhe. Naibu Spika, umefika wakati sasa wale wafugaji na wao kuwa tayari kutumia vitu vile kwa kipimo, ili visiwe tayari vitu vile wanavyovifanya wao kuenea kwa maradhi katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuja kwa ng'ombe wa maziwa katika Visiwa vya Unguja na Pemba, kulikuwa hakuna maradhi yaliyoongezeka zaidi na zaidi ya kisukari kabla ya kuja ng'ombe wa maziwa katika nchi hii. Hawa machotara, sijui jazi sijui kitu gani, kulikuwa hakuna maradhi ya sukari yaliyozidi sasa hivi.
Sasa hivi kila mtu anayetembea ni mtarajiwa wa maradhi ya sukari baadae, na kwa sababu gani basi. Wafugaji wetu wamekuwa hawana *discipline* ya utumiaji wa *molasses* inayotiwa katika majani, katika maji juu ya ng'ombe wa maziwa.

Mhe. Naibu Spika, ng'ombe yule hali majani makavu kwa kupenda bali majani yale hurovya sukari, tena sukari iliyo nzito, iliyokataa kuganda katika viwanda. Matokeo yake imekuwa ni biashara kubwa inayoletwa hapa Zanzibar. Wafugaji wanaichukua wanaitumia kwenye maji, wanaitumia kwa kuimwagia katika majani, ng'ombe anakula bila ya kipimo. Matokeo yake basi ng'ombe anakunywa maji inakuwa bila ya *limit*. Wewe unakamua lita ishirini, lita arobaini lakini kumbe umesababisha yule ng'ombe anywe maji mengi yaliyojaa sukari na wewe maziwa yako unayoyatoa yana sukari na mnywaji anapokwenda pale anapiga jagi; mchana jagi, jioni jagi, nyumbani jagi.

Mhe. Naibu Spika, sukari imezagaa kwa kutokuwa na utaratibu mzuri wa ufugaji wa ng'ombe hawa. Mhe. Naibu Spika, nipo tayari ku-*challenge* kwa hoja hiyo kama atatokea mfugaji yeyote atapinga. Anatumia sukari kulisha ng'ombe, anatumia sukari kuwapa ng'ombe wa maziwa na matokeo yake ng'ombe ndiyo wanakuwa sasa ndiyo chanzo cha kuongezeka kwa maradhi ya sukari.

Sasa ni vizuri wakawa tayari wafugaji kutumia uwezo huu wa kutoa vipimo maalumu kwa ajili ya maji, vipimo maalumu kwa ajili ya majani ili ile sukari isizagae.

Mhe. Naibu Spika, ninakwambia hivyo kwa sababu gani. Wenzetu katika nchi mbali mbali waliokuwa nao wale ng'ombe maziwa, lakini ng'ombe wakishakamuliwa maziwa yale yanakuwa tayari yanapelekwa pahala yanatolewa ile *fats* yote, *fats* ile inatumika kwa kutengeneza siagi, watu wanapata *cream* ya maziwa. Hivyo watu wanatumia maziwa bila ya matatizo, maziwa yanauzwa katika nchi mbali mbali wala hayamu- *affect* mtu, lakini ng'ombe wetu sisi akitoka pale mkamuaji anakutilia kwenye chupa, wewe unakwenda unayapiga *full protein sugar*, na ndio maana sukari ikaenea.

Sasa mimi kwa sababu hili jambo nalijua, na ndio maana nikalitangaza makusudi ndani ya Baraza hili, ili serikali yetu hili jambo walifanyie namna ya kuzungumza na wafugaji. Tayari nataka nikwambie Mhe. Naibu Spika, nimeshazungumza suala hili katika kikao husika, lakini watu wakawa bado wana utata. Kila siku idadi ya watu wenye sukari nchi hii wanaongezeka kwa sababu ya ng'ombe hawa wa maziwa, jinsi gani tumeshindwa kuwa-*maintain* wafugaji wetu na matokeo yake yamekuwa haya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nataka niseme kwamba Zanzibar ina uwezo wa kutunga sheria mbali mbali tena zenye maslahi kwa wananchi wake. Kwa vile yale yanayotengenezwa kwa mujibu wa maslahi ya sheria za nchi hii, ni vyema yakazingatiwa sana ili wanaoepuka kuzitumia sheria zile, wanaozivuruga sheria zile kwa makusudi, basi ule wakati wa kufanyakazi kwa mazoea umekwisha, na sasa ni lazima tufanye kazi kwa ufanisi, hatua kali zichukuliwe ili kulinda sheria zinazotengenezwa na chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Shehe Hamad Mattar, baadae atakuja Dkt. Khalid Salum Mohamed; Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia angalau machache katika mswada huu wa kurekebisha sheria mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze serikali yetu kwa kupitia Mwanasheria Mkuu kwamba kuona serikali yetu ni sikivu na inajua matatizo ya wananchi wake, ndio maana ikaweza kufanya marekebisho haya baada ya kusikia vilio au mawazo mbali mbali kupitia kwa wananchi.

Na mimi niungane na wenzangu kwamba mtanguliaji aliyetangulia kuchangia mswada huu, kwa kweli wengi alitufilisi. Mimi nasema ni hivyo hivyo, lakini nitaongezea kidogo tu pale inapozungumza katika sehemu ya Mahakama ya Mwanzo.

Kifungu hiki kilichozungumzia Mahakama ya Mwanzo, marekebisho yake na mimi nayakubali, lakini kuna mambo yaongezwe katika Mahakama ya Mwanzo. Tulisema kwamba Mahakama ya Mwanzo sasa iwe na watu ambao wamemaliza *degree*, ni sawa. Lakini na wale mawakili vile vile nakubaliana nao kwamba waingie katika Mahakama ya Mwanzo ambayo zamani ilikuwa hawezi kuingia.

Vile vile katika Mahakama hii ya Mwanzo turekebishe katika ile sehemu ya uwezo ya Mahakama ya Mwanzo. Kwa sababu Mahakama ya Mwanzo zamani uwezo wao ulikuwa ni mdogo katika nafasi ya kufunga mtu na kutoa faini. Vile vile sehemu hii ilikuwa imewabana sana ni ndogo sana, kwa hivyo watu ambao wameshawekwa hapa ni watu wenye ujuzi mkubwa, kwa hivyo iongezwe nafasi ile ili ionekane ni kiwango gani kitakuwa ni wastani wa nafasi yao badala ya kubakia pale pale walipokuwepo. Kama vile sehemu ya kufunga ilikuwa mwisho ni miezi sita, basi sasa iongezwe kuanzia miaka miwili mpaka mitatu waongezewe katika uwezo wa kumfunga mtu na asibakie pale pale.

Mhe. Naibu Spika, pia Mahakama hii ya Mwanzo ambayo tunaizungumza kwamba waangaliwe maslahi yao, maslahi ni muhimu sana. Tumewaweka watu hapo katika nafasi kama hiyo, lakini na maslahi nayo tuyaone yabadilishwe. Kwa sababu hivi sasa ukitizama kama alivyozungumza Mhe. Hamza Hassan hapa mapishano ni makubwa sana, kwa kweli inavunja moyo. Mtu kama huyo anayeanza na *degree*, lakini ukimtizama maslahi yake na yule wa wilaya wana sifa karibu ni moja, lakini mshahara wao wanapishana sehemu kubwa sana. Sitaki niutaje hapa, lakini inaeleweka kwamba watu wa Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Wilaya yamepishana sana. Kwa hivyo, naiomba serikali na hili iliangalie.

Mhe. Naibu Spika, tutakuwa tunayatekeleza yale maagizo ya Mhe. Rais anaposema kwamba unapompa mtu dhamana, mpe na haki yake, usiwe unampa

cheo kikubwa, lakini ukimtizama maslahi ya cheo kile humpi, suala hili naomba sana lifanyiwe kazi.

Vile vile sheria hii inayorekebishwa isiwabane wale Mahakimu wa Mwanzo ambao wapo, na maslahi haya na wao pia waweze kupata, bali iwabane wale wapya, lazima wawe na sifa hizi, kwa sababu hawa wameshawatumikia wananchi kwa muda mrefu. Pengine wengine inawezekana hata wako karibu ya kustaafu umri wao. Kwa hivyo, naomba sana watu hawa waangaliwe.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane katika suala la lugha inayotumika katika Mahakama hizi, bado na mimi nasisitiza kwamba lugha ya Kiswahili nayo iendelee kutumika kama tunataka kutunza kilicho chetu. Tusiendelee kutawaliwa tu na kila lugha za kigeni tukaona ndio lugha ambazo tunaweza kuzitumia, kwani utakapokuwa unamzungumza mtu pale mnajadiliana kwa lugha anayoifahamu, basi anaweza kupata uwezo wa kujitetea, lakini kama lugha inayotumika pale katika Mahakama basi atabakia kufumba macho, na hatimaye ataonekana ni mkosa kumbe ana uwezo wa kujitetea, kama itazungumzwa lugha ambayo anaielewa. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili na Kiingereza na mimi nakubaliana nayo sana itumike.

Vile vile niende kwenye masuala ya wale ma-*assessors*, waingie ma-*assessors* wale wawili katika kutoa maamuzi, ambao wanaingia katika kutoa maamuzi. Lakini wawe ni washauri tu, kwa hivyo Mahakimu sasa hapa watakuwa na uwezo mkubwa nao, wasiwe ni miongoni mwa wapiga kura katika kutoa maamuzi yale wawe ni washauri, na ushauri unaweza ukakubaliwa au usikubaliwe, suala hili nalo liangaliwe sana.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ibara ya 36 yenye marekebisho ya kifungu cha 26 cha kuhusu wanyama. Mimi nakubaliana nayo kwamba hili neno la kukataza lisiwepo, pamoja na maelezo yote yaliyokwishatolewa kukataza mifugo, bali iwekwe utaratibu. Naungana na suala hili kwamba utaratibu uwekwe katika hali yoyote ambayo itakuwa salama kwa wafugaji na wananchi. Bado tunahitaji mifugo iwepo kwa utaratibu, na hili linawezekana. Mimi nakubaliana nacho kifungu hiki kirekebishwe lakini isikataze moja kwa moja, hasa ukizingatia mazingira yetu na wananchi wetu ndio sisi, na sisi tunatokea huko huko kwa wakulima na wafugaji. Kwa hivyo, leo uko hapa usitunge sheria kesho na wewe mwenyewe ikakubana wakati haina madhara kiasi hicho.

Kwa hivyo, tuweke nafasi ambayo itaweza kutuweka salama sote na wale waliopo na mazingira yaangaliwe, ni wapi yataweza kukubaliwa hapa yasikubaliwe, yapo mazingira ambayo yanaruhusu, hilo nalikubali sana.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwambia mchango wangu ni mdogo, lakini na mimi nasema lazima nichangie kwenye mfuko wa majimbo.

Mfuko wa Majimbo unatugusa sote na ni muhimu sana kufanyiwa marekebisho, na mimi sitaki niongeze lolote isipokuwa marekebisho tu kama walivyozungumza wenzangu waliotangulia, nayaunga mkono hayo marekebisho ya kuwa na sisi Wawakilishi tuwe tunahusika katika mabaraza yale ambayo yanaanzishwa.

Jengine la mwisho, naunga mkono hoja hii kama ilivyoletwa na mule ambamo mutaweza kuleta faida kwa nchi yetu na wananchi wake.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumpisha Mhe. Dk. Khalid Salum; Waziri wa Fedha na Mipango kuchangia, kama tunavyoelewa tumebakiza nusu saa ambayo haitatutosha kwa ajili ya kumaliza hii shughuli yetu ya leo.

Kwa maana hiyo namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutengua kifungu, ili tuweze kuendelea na shughuli yetu hadi tutakapomaliza. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu, na kwa kuwa tunao mswada wa marekebisho ya sheria mbali mbali hapa ambao una umuhimu tuweze kuumaliza. Kwa hivyo, niliombe Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, naomba kutoa hoja ili tuweke kanuni ya muda kando tupate muda wa kumaliza shughuli zilizo mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja iko mezani wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

Tunaendelea, sasa ni zamu ya Mhe. Dk. Khalid Salum, baada ya Dk. Khalid Salum atapata nafasi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, na baada ya hapo tutampisha Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwasilisha kwa vizuri kabisa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali.

Mimi nilitaka nitoe ufafanuzi mdogo Mheshimiwa katika kuchangia hoja ya marekebisho ya sheria ya ongezeko la thamani, kwa maana ya *value added tax*.

Mhe. Naibu Spika, kilichowasilishwa hapa na Mhe. Mwanasheria Mkuu ni mabadiliko ya kifungu cha 3(a) na (b), niseme tu mabadiliko haya yametokana na marekebisho ya sheria ya fedha yaliyofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 2016.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya hapo baina ya pande zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tulikuwa na sheria zinazofanana za ongezeko la thamani. Katika utaratibu uliokuwepo kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa zilizokuwa zinahaulishwa Zanzibar kutoka Tanzania Bara, kodi hiyo ilikuwa inakusanywa Tanzania Bara kama wakala wa Hazina ya Zanzibar. Vile vile kwa bidhaa ambazo zilikuwa zinahaulishwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara, kodi hiyo ilikuwa ikikusanywa Zanzibar kama wakala wa Hazina ya Tanzania Bara.

Sasa kutokana na mabadiliko hayo yaliyofanywa kwa upande wa wenzetu, utaratibu huo sasa umeondoka, na badala yake sasa uko utaratibu wa *zero rating*, kwa maana bidhaa zinazohaulishwa Zanzibar, zilizozalishwa Tanzania Bara kule wana-*charge zero rate*, na kwa namna hiyo kodi ile tunapaswa kuikusanya hapa Zanzibar. Kwa sasa hatuna utaratibu huo kwa sababu tulikuwa na utaratibu ule wa zamani. Kwa hivyo, na sisi sasa tumelazimika kuleta marekebisho haya, kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kuweza kukusanya kodi hiyo kwa bidhaa zinazotoka Tanzania Bara zinazohaulishwa kuja Zanzibar.

Kwa hivyo, hayo ni ndio marekebisho yaliyokusudiwa, na sheria hii imempa nguvu waziri anayehusika na masuala ya fedha kuweka utaratibu, na tumeweka

hivyo makusudi ili kuepuka kwamba kila itakapotokea marekebisho kwa upande wa wenzetu wa Tanzania Bara, na sisi tulazimike kufanya marekebisho hayo.

Kwa hivyo, utaratibu huo sisi tutauweka kwenye kanuni, pale inapotokea kufanyika marekebisho kwa upande wa wenzetu, basi sisi tutakuwa hatuna ulazima wa kuleta marekebisho ya sheria, kwa sababu tutabadilisha katika kanuni.

Mhe. Simai Mohammed Said, alizungumzia masuala mengine yanayohusiana na sheria ya kodi ya hoteli, kwa maana ya *hotel levy*. Sasa hii niseme tu kwamba kuna sheria mbili, ambayo ni sheria ya kodi ya hoteli namba 1 ya mwaka 1963, ambayo hiyo haikuwa sehemu ya marekebisho yaliyowasilishwa hapa. Lakini kwa ufafanuzi tu Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kuna tofauti baina ya yale makampuni ambayo yamekuwa *VAT registered* na makampuni ambayo yanatakiwa yatozwe *hotel levy*, na mabadiliko hayo yako kwenye Sekta ya Utalii peke yake.

Tofauti iliopo kwa zile hoteli ambazo zinalipisha malipo ya malazi yaliyoanzia dola 100 na kuzidi haya yanatakiwa yalipe asilimia 18 ya *VAT*. Lakini kwa yale mahoteli ambayo kiwango chake wanacho-*charge* hakifiki dola 100, kwa maana kiko baina ya ziro mpaka dola 95 wanatakiwa walipe *levy* kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa. Utaratibu huo ni kwamba kwa zile hoteli ambazo zina-*charge* baina ya dola ziro mpaka dola 25 hawa wanatakiwa walipe dola 5 kwa mgeni, yaani anaye- *charge* baina ya dola 26 mpaka dola 45 anatakiwa alipe dola 8 kwa mgeni, na yule anaye- *charge* baina ya dola 46 mpaka 96 huyu anatakiwa alipe asilimia 18 kwa mgeni, ile *value* ambayo inatozwa na ile kodi.

Sasa hili nilitaka nilieleze kwa ufafanuzi tu Mhe. Naibu Spika, lakini hoja ya msingi iliyowasilishwa hapa ni marekebisho ya sheria ya ongezeko la thamani.

Hii kama nilivyosema tumeileta ili kuleta utaratibu mzuri unaofanana na ule wa wenzetu, wa kwamba tutakuwa na *zero rate* kwa bidhaa zilizozalishwa Zanzibar na zinazohaulishwa upande wa Tanzania Bara. Kwa hivyo, ni utaratibu wa kawaida na wenzetu wa *TRA* pamoja na *ZRB* tumewaagiza wakae ili kuhakikisha kwamba mabadiliko haya hayatoleta athari katika makusanyo ya kodi tunazostahili. Mhe. Naibu Spika, nilitaka niseme hayo tu.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha.

Sasa ni zamu ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Baada ya hapo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuwa miongoni mwa wajumbe wako tunaochangia hoja hii ambayo imeletwa mbele yetu na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, juu ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwashukuru wale wote ambao wametoa maoni yao juu ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na mimi sitaki kwenda sana katika ufafanuzi bali nitamuachia mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini wajumbe wengi wamezungumzia juu ya suala la kifungu cha 39(t) kinachohusu katazo la ufugaji wa wanyama.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba nadhani maoni ya Waheshimiwa Wajumbe na maoni ya serikali au mapendekezo ya serikali hatuko mbali sana.

Mhe. Naibu Spika, nia ya kifungu hiki cha 39(t) ni kuweka mazingira yatakayowezesha serikali kuweza kuweka mazingira mazuri ya wafugaji wetu kufuata utaratibu wa kufuga, na pale itakapobidi basi kuweka katazo la kukataza katika maeneo maalumu yasiyoruhusiwa kuweza kufuga wanyama, ndio hasa madhumuni ya kifungu hiki.

Sasa mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wakubaliane na kifungu hiki, kwa sababu lengo ni kuweka kifungu hiki na hatimaye kutunga kanuni ambazo zitaweka utaratibu wa kufuga.

Uko utaratibu wa kufuga hasa ng'ombe wa maziwa katika maeneo yaliyoruhusiwa na kutokufuga wanyama wengine katika maeneo yasiyoruhusiwa. Sasa ningewaomba sana Wajumbe waelewe kwamba nia yetu sio kuwakataza kabisa wananchi. Lakini kama nilivyosema ni kuweka utaratibu na mazingira kwa nini Serikali imefanya hivyo, ni kwa sababu yamejitokeza matatizo katika maeneo hayo ya ufugaji.

Kwa hivyo hatuna nia kabisa Serikali ya kukataza kabisa wananchi wasiweze kufuga, lakini kuna utaratibu utakaowekwa wa kuweza kufuga hasa ng'ombe wa maziwa katika maeneo maalumu, na Serikali inaweka utaratibu wa kutafuta eneo maalumu katika Manispaa hasa hizi mbili za Magharibi (A) na Magharibi (B) kwamba hili litakuwa ni eneo la wafugaji wale wanyama wengine.

Jengine ambalo nataka niliseme ambalo nichangie hoja hii ya Mhe. Mwanasheria Mkuu ni pale Wajumbe walipoiomba sana Serikali sasa ifanye marekebisho kutufanya sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa Madiwani, na hoja yao inakuja zaidi hasa kwanye ule utaratibu wa zile fedha ambazo zinasimamiwa sasa na Halmashauri.

Katika hili nataka nichukue nafasi ya kumpongeza sana Mhe. Miraji kwa nini Serikali imefikiria kuja na haya marekebisho ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na fedha hizi sasa badala ya kuingia kwenye *accounts* zetu moja kwa moja za mifuko ya jimbo kwenda kwenye *accounts* za Halmashauri kutokana na kasoro ambazo zimejitokeza katika kipindi kilichopita. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais atakuja kufafanua zaidi.

Mkurugenzi wa Halmashauri kuwa katibu wa kamati ya Maendeleo hakumfanyi mfuko huu kuupeleka kwenye Baraza la Madiwani na kuamuliwa, ni vitu viwili tofauti, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo una Sheria yake isipokuwa marekebisho yanayofanywa ni kumfanya Mkurugenzi kuwa katibu wa ile kamati, lakini katu hakuna utaratibu wa mfuko huu kuupeleka kwenda kuamuliwa na Baraza la Madiwani. Kwanza hilo lazima tulielewe, hakipo kitu hicho. Baraza la Madiwani kazi zao ni nyengine kabisa, kilichopo pale kwamba zile fedha zinapitia pale kwenye Manispaa au Halmashauri au kwenye Baraza la Mji na Mkurugenzi ndiye atakuwa katibu wa zile kamati.

Sasa kama suala atakuwa peke yake taratibu vipi hii mifuko, sasa hilo namuachia mwenyewe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais atakuja kulifafanua zaidi na Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini nataka niwatoe hofu kwamba fedha hizi hazitakwenda kabisa kwenye Baraza la Madiwani, kwa msingi huu Madiwani ukiacha wale waliotajwa ndani ya sheria ya mfuko wa jimbo ambao nakumbuka katika kila kamati ya Mfuko wa Jimbo kuna Madiwani wawili; mmoja awe mwanamke mmoja awe mwanamme. Mmoja awe wa kuchaguliwa, mmoja kwa ufupi awe mwanamke mmoja awe mwanamme. Sasa wanaingia kwenye ile kamati lakini hayaamuliwi mambo yale kwenye Baraza la Madiwani, sasa hoja na sisi tuwe madiwani.

Sasa hoja na sisi tuwe Madiwani mimi niwasihi Waheshimiwa wajumbe bado suala hili tuliache, kwa sababu sheria mbili ambazo tulikuja nazo mwaka juzi, Sheria No. 7 hii ya Serikali za Mitaa na Sheria No.8 ya Tawala za Mikoa. Sheria hii ya Serikali za Mitaa inaweka utaratibu wa kuwa na Baraza la ushauri la shehia ambapo ndiko mambo yanaanza kuibuliwa na wananchi wenyewe, kwa sababu ndio maana ya madaraka kuyapeleka kwa wananchi wenyewe, yakitoka kwenye Baraza la Ushauri la Shehiya yanakuja kwenye Baraza la

Maendeleo ya Wadi ambalo Mwenyekiti wake anakuwa Mhe. Diwani na pale kutaajiriwa katibu wa Wadi na watu watakaochaguliwa katika lile Baraza la Wadi.

Mambo haya yakitoka ndio yanakuja sasa kwenye Baraza zima la Madiwani kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya au Manispaa au Baraza la Mji, yakishakujadiliwa mambo haya yanakwenda kwenye *Secretariat* ya mkoa ambayo itaongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa, baada ya hapo mipango yote itakayoamuliwa iatakuja kwenye kamati ya Maendeleo ya Mkoa, kwenye Kamati ya Maendeleo ya Mkoa humkuti tena Diwani pale unamkuta Mbunge na Mwakilishi ni Wajumbe katika lile Baraza la Maendeleo la Mkoa ambalo linakuwa chini ya Mkuu wa Mkoa. Mipango ile sasa ikitoka pale inakuja Wizarani inakwenda kwenye Tume ya Taifa ya Mipango kwa kujadiliwa.

Sasa sisi tukianza kuwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani nadhani itakuwa tunajiwekea mazingira ambayo nahisi kwa sasa hivi yatakuwa sio sahihi sana, kwa hivyo niwasihi ni jambo ambalo linazungumzika Waheshimiwa Wawakilishi, lakini hebu kwanza tu- *practice* na hili ambalo lipo.

Najua tunaweka mfano wa Waheshimiwa Wabunge Bara, lakini tuelewe vile vile hata Waheshimiwa Wabunge kwa Sheria ile ile ya Bara si Wajumbe wa Baraza la Madiwani kwa hapa, kwa hivyo niwasihi Waheshimiwa Wajumbe kwa hili tusubiri kwanza, angalau tufanye mapitio ya hizi sheria ambazo tumezipitisha, halafu kama kuna uwezekano huko usoni basi kama tulivyoleta sasa tunaweza tukaja tukaamua wakati huo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kwisha kusema hayo naomba niunge mkono kwa asilimia mia moja hoja hii ya Mwanasheria Mkuu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Aidha niwashukuru wasemaji wenzangu walionitangulia kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zinazohusu sekta zao.

Vile vile nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuwasilisha hoja hii muhimu ya marekebisho ya sheria mbali mbali na kuweka masharti yaliyo bora kuhusiana na mambo hayo, nampongeza sana kwa uamuzi huo.

Aidha niwapongeze Waheshimiwa wajumbe ambao wameuchangia sana Mswada huu kwa kina, maelezo yao mazuri yametupa mwanga mkubwa sana vipi tufanye marekebisho pale panapohitaji marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe mimi eneo langu hasa linahusu mfuko wa jimbo na umeelezwa vizuri hapa katika Mswada wenyewe, kuna kifungu hapa ambacho ndio kimezungumzwa sana kifungu cha 29(e) Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa husika ambaye atakuwa Katibu, hapa sasa wajumbe wengi walizungumzia mtu mmoja huyu atawezaje kuwakilisha kamati mbali mbali za majimbo.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe hii imetokana na uzoefu tulioupata kwa upande wa mfuko wa jimbo, ukitizama miradi mingi ambayo imeanzishwa na mfuko wa jimbo kwa upande wa Wawakilishi haikufanya vizuri kama ambavyo kwa mfuko wa jimbo kwa upande wa Wabunge, na hii ilitokana na tathmini kubwa ambayo tumeifanya na tukaona yako maeneo Waheshimiwa wamefanya vizuri kwa jimbo, lakini yako maeneo kumefanyika vibaya sana, kwa hivyo moja lililoonekana pale ni usimamizi wa yale matumizi ya mfuko wa jimbo.

Kwa hivyo Serikali ikaona ili kutekeleza lengo lililokusudiwa ambalo ni kusaidia miradi ya wananchi katika maeneo husika lengo lile lifanyike, kwa sababu fedha zinatoka mradi haufanyiki, lile lengo linakuwa halifikiwi. Lengo ni kuunga mkono hali za wananchi katika eneo hilo, na yanayofanyika hapa ni kuweka mazingira mazuri zaidi kwa Mhe. Mwakilishi mwenyewe kukubalika kwa wananchi wake, kwa sababu sasa ile miradi inakwenda vizuri zaidi.

Sasa kwa kuwa mfuko wa jimbo katika sheria yake ilipoonesha Afisa Mipango wa Halmashauri ndio alikuwa Katibu, na Katibu mmoja huyo aliweza kusimamia vizuri sana mifuko yote ile katika kamati zile za Maendeleo za jimbo, na si lazima kwamba atakuja yeye moja kwa moja, yeye anaweza kuwakilishwa kwa niaba yake na Afisa mwengine ambaye atateuliwa na Mkurugenzi fedha, kwa hivyo inawezekana siku moja hiyo kukawa na Kamati ya Maendeleo imekaa katika Jimbo hili na jimbo lile alimradi atakuwa ametaarifiwa kwamba kuna siku hii kuna kamati inakaa, ikiwa ni zaidi ya moja yeye atachukua Afisa mwenyewe kutoka Ofisini kwake atakayempeleka pale kumuwakilisha, ilimradi utekelezaji ufanyike bila ya kuchelewa. Na kwa sababu uzoefu umefanyika vizuri kwa upande wa mfuko wa Jimbo na upande wa ubunge, tukaona ni vizuri kufanya hivyo kuliko utaratibu tuliokuwa nao sisi ambao ulikuwa haumjumlishi Afisa kutoka Halmashauri, na matokeo yake tuliona kwamba miradi haikwenda vizuri ndio asili ya kumuweka huyu

Mkurugenzi wa Halmashauri katika Serikali za Mitaa awe Katibu wetu wa Kamati.

Kwa hivyo nataka niwahakikishie Waheshimiwa kwamba wapo maafisa wengi wa Serikali wanaoweza kwenda kwa niaba yake shughuli zikafanyika, na bado yeye atakuwa dhamana wa kuhakikisha kwamba matumizi yamefuata utaratibu, mradi umefanyika na wewe Mwenyekiti utapata unafuu kutoka katika jimbo lako kwamba mradi umekwenda vizuri, naamini nyote mutaona kwamba pale ambapo usimamizi umekwenda vizuri na miradi ikafanyika utapata *compliment* kwa wananchi. Lakini na wewe mwenyewe unapata fakhari kwamba fedha zimetumika vizuri, mradi ule kupatikana ndio asili ya kufanya Mkurugenzi awe Katibu, naamini sana hilo jambo litapunguka.

Mheshimiwa amelielezea vizuri sana, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ suala la sisi kutokuwa madiwani amelieleza, nataka mimi nimshukuru sana. Lakini tujue kwamba sisi wenyewe ndio wenyeviti wa Kamati ya Maendeleo katika Jimbo, kwa msingi huo kama alivyosema yeye Madiwani watakaokuwemo pale kwenye kamati ndio watakuwa na mchango, lakini kama hayupo kwenye kamati ile maana yake hana mchango na hawezi kuingia kwenye ile kamati. Kwa hivyo bado Mwakilishi ni Mwenyekiti na ndiye atakayeendesha shughuli nyingi za vikao hivyo, na ndio hasa hasa atakayeshauriana na wananchi katika eneo katika kuinua miradi yao, kwa hivyo mimi sina shaka yoyote Mhe. Mwakilishi una nafasi pana zaidi ya kusimamia wananchi wako ili kukidhi kiu ya maendeleo katika jimbo husika.

Kwa hivyo mtazamo hapa marekebisho yanayofanywa nia na dhamira yake ni miradi ifanyike vizuri na kuwaondolea lawama Waheshimiwa Wawakilishi ya kulaumiwa kwamba matumizi hayakwenda vizuri, kama ambavyo ripoti ya *CAG* ilivyokuja ikaonesha kwamba miradi mingi mambo hayakuwa mazuri, hii yote ni kuwaondoshea dhima hiyo na kuweka utaratibu mzuri ambao utawajengea mustakbali mwema kwa wananchi na kuleta maendeleo katika majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nashkuru na nawashukuru Wajumbe kwa kunisikiliza. Ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kukushukuru kwanza kwa kunipa nafasi ya kuja kutoa ufafanuzi mbali ya ule ambao tayari Waheshimiwa Mawaziri wamesaidia katika kutoa ufafanuzi.

Pia Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru wajumbe wote ambao wamechangia hoja hii iliyokuwa mbele yetu, hoja hii Mhe. Naibu Spika, imepata wachangiaji karibu 12 naomba kwa heshima kubwa niwatambue.

1. Mhe. Mihayo Juma N'hunga ambaye amechangia kwa niaba ya Kamati.
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
4. Mhe. Simai Mohammed Said
5. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
6. Mhe. Miraji Khamis Mussa.
7. Mhe. Said Soud Said
8. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, yeye alichangia kwa maandishi
9. Mhe. Shehe Hamad Mattar
10. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
11. Mhe. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za mitaa na Idara Maalum za SMZ.
12. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza, wengine wametoa mawazo yao, lakini kwa yale ambayo yalitaka majibu *specific* ya Sheria ambazo zipi, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao na wao wameweza kutoa ufafanuzi…

Mhe. Naibu Spika: Kama sikosei sijawasikia waliochangia kwa maandishi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Niliyepata aliyechangia kwa maandishi ni Mhe. Mtumwa Peya Yussuf ambaye nimemtaja, sasa wengine nimepata vikaratasi lakini havina majina.

Mhe. Naibu Spika: Kuna kimoja nimekileta nimeandika Mhe. Hassan *Diaspora*.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Na Mhe. Hassan Khamis Hafidh naomba radhi naye amechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mengi ambayo waheshimiwa Wawakilishi wameyauliza yamegawika katika sehemu tatu au nne. Moja ni lile ambalo alilianza Mhe. Mihayo na pia akalizungumzia Mhe. Hamza, la kutoa fursa kwa Mawakili kuweza kuingia kwenye Mahakama za mwanzo, ukisoma sheria kifungu cha 8 kinakataza Mawakili hao kuanza kuingia kwenye Mahakama za Mwanzo, lakini mawazo ya Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba kwa sababu sasa

tumebadilisha sheria, na kwamba sasa Mahakimu hawa waanze kuwa na Digirii ya kwanza. Sasa ni vyema na Mahakimu tuwaruhusu sasa kuingia na kuweza kuwatetea wateja wao kwenye Mahakama hizi, wazo ni zuri, wazo linazungumzika.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwenye Mahakama hizi tunapoanza kusikiliza tunakwenda na uwezo, kila Mahakama imepewa uwezo wa kusikiliza kesi, na kila Mahakama imepewa uwezo wa kutoa hukumu. Sasa kwa mfano kwenye Mahakama ya mwanzo ambayo uwezo wake ni mdogo lakini leo unamwambia aingie wakili ambaye gharama zake za kuchaji ni kubwa kuliko zile gharama ambazo Mahakama ile ina uwezo wa kusikiliza na kutoa maamuzi, nalo inabidi pia tulitizame, kama kuna maeneo inabidi tuyatizame.

Kwanza ni kuzidisha sasa uwezo wa ile Mahakama kama sasa ina uwezo gani wa kuweza kusikiliza, na uwezo huu Mhe. Naibu Spika unakwenda sasa kwa mahakama zote, unapoanza Mahakama ya mwanzo maana yake pia ubadilishe sasa uwezo wa Mahakama inayofuatia juu yake, lakini pia ubadilishe uwezo wa Mahakama inayofuatia juu yake. Mahakama ambayo uwezo wake ni mkubwa na hauna kipimo ni Mahakama Kuu. Sasa hili niwaombe Waheshimiwa Wajumbe linazungumzika lakini tulitizame vizuri.

Pia, kwa kipindi hichi ni vyema kutoa fursa kwa sababu ishapita sheria hii maana yake hata na wale waliokuwepo sasa Mahakimu wanasema sasa uwa-*phase out* waje hawa wengine, lakini pia itoe fursa kama sasa Mahakama nayo ianze kuajiri wale ambao tayari wana vyeti waanze kuondoka pamoja na kwamba Mhe. Hamza amesema wengi wa hawa wana *masters degrees.* Ni sawa lakini pia kuna wengi ambao bado wamebaki wana vyeti hivi ambavyo vimetajwa. Sasa kwenye hili ni vyema tulitizame vizuri, na sisi tumelichukua tutazungumza na Mhe. Jaji Mkuu ambaye ndiye anayetoa sasa uwezo wa kila Mahkama kusikiliza kesi ili sasa hivi viwango viweze kurekebishwa kulingana na mabadiliko ambayo tumeyafanya katika sheria hii.

La pili, mengi ambayo yamezungumzwa kipi kinaanza mwanzo alisema Mhe. Hamza kinakuja Kiswahili au Kiingereza, nadhani kinakuja mwanzo Kiswahili halafu kifuate Kiingereza. Kwa sababu Kiswahili bado kitabaki ni lugha ya kwetu na ni lugha ambayo tunatumia, kwa hivyo kitumiwe Kiswahili na ikibidi basi itumike Kiingereza, ndio dhamira ambayo tumekusudia.

Chengine ambacho Mhe. Hamza pia alizungumza ni sifa ya Mrajis kama ameona humu kuna Warajis tumewazungumza lakini hatukutaja sifa zake. Ni kweli kwa sababu sheria ambayo imetengeneza nafasi ya Mrajis ni ile Sheria ya

Mahkama Kuu, Sheria Namba 2 ya mwaka 1985, ile ndio ambayo imetaja sasa na kuweka nafasi ya Mrajis.

Sasa wazo lako hili ni zuri, tutapoanza sasa kurekebisha ile sheria ya Mahkama Kuu sasa na haya mawazo ambayo mumeyatoa, sasa nayo pia tutayachukua ili yajumuishwe katika kuyafanyia marekebisho.
Mengine yalikuwa mawazo, sifa hizi za Mwenyekiti wa Tume ya Madawa ya Kulevya tuweke, *any way* wazo zuri lakini ukitizama asili yake Mhe. Naibu Spika, kama tumekuwa tukifanya mabadiliko ya nafasi hii kutokana na ile idara inapokwenda.

Kama mtakumbuka Waheshimiwa tulianza na Ofisi ya Waziri Kiongozi ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa ile Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya, baadae ili idara yake ilivyobadilishwa kuwepo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ikabidi tuje kubadilisha tena sheria tumuweke Makamu wa Kwanza wa Rais ndio Mwenyekiti wa ile Kamati. Sasa hivi Idara ile iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hatuwezi kuja tena kubadilisha sheria tukairudisha sasa kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Dhamira yetu sasa ni kumwachia Mhe. Rais uwezo mpana sasa wa kuchagua bila ya kujali ile idara sasa ataipeleka wapi, ama akiamua kuipeleka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais sawa, akiamua kuipeleka Ofisi yake ya Ikulu kwa Mhe. Gavu sawa, yeye tumwachie nafasi ya kuteua Mwenyekiti. Ukitizama muundo wa lile Baraza karibu wote wajumbe ni Mawaziri. Sasa tunaamini hekma za Waheshimiwa Marais hawa ni pana, na watapochagua watu watachagua watu kulingana na wale ambao anaowaongoza. Sasa ningewaomba kwenye hili tusitie sifa kwa sababu ambazo nimezieleza Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Dkt. Mwinyi amezungumzia sana kuhusu Chuo cha Kizimbani na akauliza kuhusu hii kamati, hii ni Kamati ya Utafiti. Ukitizama kwenye sheria sasa hivi hakuna kamati ambayo imeanzishwa. Sasa lengo letu ni kutoa fursa sasa kwa Baraza lile la Chuo kuanzisha hizi Kamati, na Kamati ya kwanza ambayo tumependekeza iwe ni hii ya utafiti. Ukisoma kile kifungu kinaelezea kama sasa Baraza litakuwa na uwezo mwengine wa kuteua Kamati mbali ya hii ya Utafiti ambayo imeanzishwa ndani ya sheria.

Jina la Mkurugenzi ni kweli sasa hivi anaitwa Mkurugenzi na ukweli ukitizama Vyuo vyengine tunawaita *Principals*, sasa hatuna *consistency* kwenye kuwaita hawa Wakuu wa Vyuo, wazo ni zuri. Sasa hivi lakini dhamira iliyokuwepo ni kumpandisha hadhi yule Mkurugenzi ambaye yupo na kumpa sasa hadhi ya Ukurugenzi Ukuu. Lengo letu baadae Chuo hichi nacho kukitia katika orodha ya vile Vyuo ambavyo vitakwenda SUZA. Sasa tukivitia kule angalau tukianza

kukiimarisha tokea sasa hivi ili na Mkurugenzi wake huyu Mkuu awe na hadhi ile ambayo inalingana na wale ambao watakwenda nao kule watapojiunga na SUZA. Haya mengine nadhani Waheshimiwa Mawaziri wameyajibu; ya kufuga.

Mhe. Simai amezungumzia *spelling mistake* nadhani hili tunalichukua ni sawa, VAT Mhe.Waziri wa Fedha amelijibu.

Mhe. Ali Suleiman amezungumzia mambo ya Mfuko wa Jimbo nadhani haya yamejibiwa na pia kifungu cha kukataza kufuga ng'ombe nadhani yamejibiwa vizuri na Mhe. Waziri na hata marekebisho tumeyafanya ya kuzungumzia jinsi gani kile kifungu kizungumzike, kwa sababu pia hili tulizungumzia kwenye Kamati.

Mhe. Miraji nimshukuru ametambua dhamira ya Serikali ya kubadilisha vifungu hivi vya Sheria ya Mfuko wa Jimbo kwa hivyo ninamshukuru lakini pia nimjibu ameuliza kama leo tunabadilisha Sheria ya Chuo cha Kizimbani, lakini kuna mswada wa SUZA ambao unakuja unaunganisha baadhi ya vyuo.

Nimwambie tu Mhe. Miraji Chuo cha Kizimbani hakimo kwenye ule mswada wa SUZA, kwenye mswada wa SUZA kuna vyuo vitatu. Kuna Chuo cha Afya, kuna Chuo cha Taasisi ya Maendeleo ya Utalii na Chuo cha Fedha cha Chwaka. Hivyo ndio vyuo kwa mara hii tunaanza navyo kuvi-*up grade* na kuvitia SUZA, hiki cha Kilimo cha Kizimbani kitakuja baadae.

Mengine Mhe. Mwenyekiti, ni majibu ambayo yametolewa na Waheshimiwa Mawaziri, kwa hivyo kiujumla niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mawazo ambayo wametupatia lakini pia kwa michango ambayo wameitoa, na sisi haya ya kamati tunayachukua na tunakubaliana nayo yote mia kwa mia.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Mwanasheria Mkuu ametoa hoja sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, naona hawa Makatibu wameona *AG* ni mzoefu kwa hivyo mara nyingi vile vikaratasi vinavyopelekwa

kwa Mawaziri kusema ukishamaliza kutoa hoja *stage* inayofuata ni nini hawakumletea *AG*, kwa sababu wanadhani ni mzoefu.

Mhe. Naibu Spika: Nilidhani umeletewa makatibu, niliona kama alipelekewa pale, naomba ufuate ya 11 na utasoma kile kilichopo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nadhani nimeiona, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na Kuweka Masharti yaliyo Bora kuhusiana na Mambo hayo

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na Kuanza Kutumika

Sehemu ya Pili

Marekebisho ya Sheria ya Mahusiano Kazini Namba 1 ya 2015

Kifungu 2 Kusomwa
Kifungu 3 Marekebisho ya Kifungu cha 81

Sehemu ya Tatu

Marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Nam. 6 ya 1985

Kifungu 4 Kusomwa
Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha 5

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii nikataka ufafanuzi zaidi kwa mkufunzi wangu wa sheria Mhe. Mwanasheria Mkuu. Unajua ule mswada wa mafuta ule sasa hivi tumepata utaalamu sana wa sheria hasa kutokana kuwa mkufunzi wetu Mwanasheria Mkuu pamoja na msaidizi wake Sheikh Saleh.

Mhe. Mwenyekiti, nilishauri katika kufanyiwa marekebisho ya hiki kifungu pamoja na zile sifa za Hakimu wa Mahkama ya Mwanzo kwamba sasa hivi ili awe na sifa hiyo awe na *degree* kutoka *certificate* lakini kuna suala zima la *experience*.

Sasa hili Mhe. Mwanasheria Mkuu sikumsikia kulitaja, kwa sababu unajua mtu anaweza akatoka na Diploma Chuoni moja kwa moja akafika pale akawa ndio Hakimu wa Mahkama ya Mwanzo kwa sababu tayari amesha-*qualify* kwenye hii sifa. Lakini sasa tatizo linalokuwepo Mhe. Naibu Spika, kwamba suala la kutoa haki ni suala zito sana, na huku mara nyingi kesi hizi zinazoendeshwa wale ambao kesi zao zinaendeshwa na kuwa hawana uwezo wala ufahamu wa sheria yoyote, wizi wa kuku, waiba nazi, waiba mihogo, wanaodhalilisha ng'ombe, punda. Sasa kama hakuna *experience at least* ya kufanya kazi alau miaka 2 au miaka 3 pamoja na hiyo sifa yake ya kuwa na diploma au *degree*, lakini *at least* ile *experience* ya kazi hapa Mwanasheria Mkuu hakulitolea ufafanuzi. Hebu naomba atusaidie katika hilo.

Vile vile, hapo hapo kuna suala jengine nilizungumza awe Mzanzibari, na nilizungumza awe na sifa hiyo kwa sababu tunakosa wale Majaji wa Mahkama ya Rufaa kwa sababu tunakuwa hatuna Majaji ambao wana *experience* ya muda mrefu ambapo kama hapa hatukuweka wazanzibari ina maana ndio baadae tunakuja kuwakosa.

Sasa labda haya mambo mawili anisaidie hapa. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda nianze hili la sifa la kuwa Mzanzibari. Kwa hivyo Mhe. Hamza anakumbuka kama Sheria ya Utumishi wa Umma sasa hivi inaelezea vizuri kama kwenye nafasi zote ambazo zinatangazwa na Serikali, moja ya sifa ambayo inawekwa kwamba waombaji wawe ni wazanzibari kwenye nafasi za Utumishi wa Umma.

Moja ya sifa ni watumishi hawa wawe wazanzibari, sasa wazanzibari hawa lina- *cut across* kwenye nafasi zote hizi Mhe. Mwenyekiti.

Sasa kwenye hili nadhani Mhe. Hamza atafahamu kama tayari kuna sheria inayoongoza, ambayo inazungumzia masuala mazima ya ajira ndani ya utumishi wa Serikali.

Kwa hivyo tayari imeshatajwa sifa, sifa ni kuwa mzanzibari. Lakini hili la uzoefu ukilitizama ni gumu kidogo Mhe. Mwenyekiti, kwamba nafasi hizi zinawezekana sasa kama hutaki kuajiri watu, utampata mzoefu gani ambaye

sasa ameshaanza kufanya kazi hizi za uhakimu mlete umuajiri hapo hapo. Linalofanyika sasa hivi Mhe. Mwenyekiti ni kwamba hawa wote ambao wanahitimu mafunzo ya sheria, kabla ya kupata ajira maana inabidi sasa wafanye *internship*. Sasa hivi kuna *internship* ambayo inafanywa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia kuna *Law School* ambayo imeanzishwa na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia kuna sheria ambayo tutaileta baadaye, Sheria ya Mawakili hawa nayo pia inaanzisha utaratibu sasa wa mafunzo kwa hawa *graduates* wa sheria ambao wataingia na wao pia kwenye utaratibu huo huo. Sasa kwa sasa hivi kumuwekea mtu uwezo useme mtu asiajiriwe kwenye nafasi ya uhakimu mpaka awe na sifa za miaka 7 za kuwa ametekeleza kazi za uhakimu itakuwa ngumu.

Jengine kubwa Mhe. Mwenyekiti, lililofanywa ni kwamba kwa mageuzi haya ambayo yamefanywa sasa hivi ya muundo na mifumo, uajiri sasa hivi wa Mahakimu inavyotakiwa uanzwe kwanza kwa kutizama wanasheria wazoefu waliokuwepo nchini. Kwa sababu maslahi sasa yameongezwa na zile nafasi sasa zimekuwa zimepewa hadhi baada ya marekebisho ambayo tumefanya. Sasa badala ya kutumia utaratibu ule ule wa kawaida tuliouzoea, inavyotakiwa sasa hivi Tume ya Utumishi ya Mahkama inapotoa matangazo ya ajira, kwanza ianze kutizama Serikalini tunao wanasheria wangapi ambao tayari wana uzoefu wa kazi, ili sasa wao ndio wapewe kipaumbele cha kwanza cha kuomba hizi ajira, halafu baadae ndio unafuata sasa huu utaratibu mwengine.

Sasa utaratibu upo mzuri Mhe. Mwenyekiti umewekwa, sasa niombe Mhe. Hamza atukubalie kwenye hilo kama kuna utaratibu mzuri ambao umewekwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kuendelea kupata darasa kwamba kumbe sasa hivi tukipitisha hizi sheria si lazima itaje mzanzibari kwa sababu tayari kuna ile sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa hivyo tunashukuru kwa hilo mimi ninafikiri litakuwa liko sawa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini alipokuwa akitoa ufafanuzi Mhe. Mwanasheria Mkuu alizungumzia kwamba sasa hivi tayari kuna haya masuala ya miongozo na miundo ya utumishi, na wanapoajiriwa hawa wanatakiwa kwanza waangaliwe wale watu ambao tayari wenye *experience* lakini vile vile na lile suala analozungumza kwamba katika *experience* kumbe kuna *internship* sasa hivi mimi nafikiri hoja yangu hapo itakuwa iko sawa. Sasa labda tu anisaidie kwa sababu Waziri wa Katiba na Sheria hakuwepo, tuliongezea kitu pale ilikuwa kuhusu maslahi ya hawa Mahakimu wa Mahkama ya mwanzo ambao sasa hivi watakuwa wanaajiriwa kwa ile sifa sio ya *certificate* tena, lakini kuanzia ngazi

ya *diploma* kwenda *degree,* sasa je, ina maana hii sifa ya sasa hivi baada ya kupitisha sheria hii itaendana na yale maslahi yao kama hivyo walivyoizungumza. Kwa sababu sasa hivi katika suala zima la maslahi wako mbali sana, yaani kama *astaghfiru llahu laadhim* basi nikisema mbingu na ardhi nitakuwa nimekufuru lakini nisha-*staghfiru*, labda ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ninajua Mhe. Hamza anatetea Mahakimu na hiyo ndio kazi ambayo imekuwa ikifanywa na Serikali ya awamu hii tokea mwaka 2010. Sasa hilo alilosema nadhani ni jambo ambalo la kiutumishi, nadhani Serikali inasikia na kuna maelezo na majibu tofauti yamekuwa yakitolewa. Sasa nimuombe tu Mhe. Hamza majibu kwenye hili tayari nadhani yameshatolewa muda mrefu, lakini akitaka majibu zaidi basi alete swali kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma atamjibu tena vizuri zaidi. Lakini haya ya kiutumishi ambayo hayamo ndani ya sheria hii kwa hivyo naomba atuachie tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nishajua anakonipelekea na nitakwenda huko.

Kifungu 5	Marekebisho ya Kifungu cha Tano
Kifungu 6	Marekebisho ya Kifungu cha Saba
Kifungu 7	Marekebisho ya Kifungu cha Kumi

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho ya kifungu cha 10(2) nilielezea wale Mahakimu wa Wilaya sasa hivi nao pia sifa zao zimetoka kwenye stashhada na kutajwa kwamba itakuwa ni shahada. Vile vile nilijaribu kushauri kwamba kama nilivyosema mwanzo kwamba hawa Mahakimu wa Mahkama ya Mwanzo ambao Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba bado wapo ambao wana zile *certificates*, mimi nataka nimthibitishie nimefanya *research*, wamebakia wawili tu Mahakimu wa Mahkama za Mwanzo ndio ambao wana *certificates*. Lakini wengi wao sasa hivi wana ngazi sio ya *diploma* kuanzia *degree* kwenda *masters,* sasa ndio maana nikajaribu kushauri, je, katika kupandisha madaraja wakati wa kuteua Mahakimu wa Mahakama za Wilaya kwa nini kusiwe na haja kwamba wale Mahakimu wa Mahakama za mwanzo ambao tayari wamejisomesha na wameshakuwa na uzoefu, kwa nini wasipandishwe hapa na ikawezekana kukatoka *loophole* ya kuteuliwa Mahakimu wa Mahakama za Wilaya kutoka nje ya wale Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo. Labda anisaidie ufafanuzi katika hapo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Hamza anajua utaratibu wa kupandisha hawa Mahakimu daraja, kazi hiyo imeachiwa Tume ya

Utumishi wa Mahakama ndio yenye dhamana ya kupandisha hawa Mahakimu na wao ndio *appointing authority*. Sasa hatuwezi ukaandika hapa Mhe. Mwenyekiti wakati tayari kuna Tume ile ambayo moja ya kazi yake ni hiyo na ambayo imeelezwa vizuri kwenye Katiba na sheria. Nimuombe kama aache ile Tume ifanye utaratibu wake ambao umeelezwa wa kisheria wa kupandisha madaraja hawa Mahakimu. Sasa hivi nadhani wana utaratibu mzuri ambao umewekwa na ambao wanataka kuubadilisha zaidi, kwa hiyo, asubiri tu mambo mazuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba sasa hivi anasema wameweka utaratibu huo mzuri, lakini bado nilikuwa nataka kumthibitishia Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ameingia hapa hayo maboresho ambayo ameyasema kwamba yamefanywa lakini bado katika ile ngazi ya Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo bado hakujafanyika chochote. Sasa hilo tu hiki kifungu nakiruhusu, lakini nafikiri Mhe. Waziri kwa kuwa anatikisa kichwa najua atafanya hiyo kazi, na kwa sababu mwezi Machi hapa tutakuwa tunawasilisha ripoti za kamati, moja katika masuala yangu nitakuja kumuuliza masuala hayo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 7 Marekebisho ya kifungu cha 10

Sehemu ya Nne

Marekebisho ya Sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar Nam. 9 ya 2013

Kifungu 8 Kusomwa
Kifungu 9 Marekebisho ya kifungu cha 37 pamoja na marekebisho yake

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilimsikia vizuri sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kuhusu suala la Naibu Mrajis kuteuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa Warajis wa Mahakama Kuu.

Sasa unajua kwa bahati mbaya sijaipitia hiyo miongozo ya uteuzi wa hawa Warajis, lakini sijui Mhe. Mwanasheria Mkuu hakuona kwamba lazima tuweke sifa, kwa sababu inawezekana anao lakini pengine hawaendani hasa na ile elimu ambayo iliyokuwepo sasa hivi. Mimi nadhani ili kuwafanya na wao wajifunze zaidi hatuoni haja hapa kwamba kuwekwa hii sifa, maana yake unajua vyeo hivi mheshimiwa unaweza ukawa na cheo kikubwa lakini elimu yako ndogo. Sasa lakini wako Warajis hizi elimu zinatofautiana, sasa ndio

maana nikasema hatuoni haja tukaweka sifa, maana yake unaweza ukamkuta Naibu Mrajis pengine ana *diploma* lakini kuna watu wana *masters* pale. Anaweza akaachwa mwenye *masters* akawekwa mwenye *diploma* wale wengine ikawa kama wanavunjika moyo, hebu kidogo atusaidie bado hajaona umuhimu wa kuweka sifa hapo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikifanya majumuisho nilimfahamisha Mhe. Hamza kwamba sheria Nam. 2 ya 1985 *High Court Act* juu ya sheria ya Mahakama Kuu, ndio sheria ambayo imeanzisha nafasi ya Mrajis wa Mahakama Kuu. Sasa sifa zake na utaratibu wake umetajwa kwenye ile sheria Nam. 2 ya 1985, kwa sababu hawa tayari wameshaajiriwa na tayari wanafanya kazi. Anachofanya Jaji Mkuu hapa ni kuwapeleka kwenye hizi Mahakama ambazo zinaanzishwa, kama sasa hivi tumeanzisha Mahakama ya Biashara, tukianzisha na Mahakama nyengine. Kwa hiyo, kazi ya Jaji Mkuu ni kuwatoa wale ambao tayari wameshaajiriwa kufanya kazi za Warajis na kuwapeleka kwenye hizi Mahakama kuwa kama Warajis na kufanya kazi hizi katika Mahakama hizi nyengine. Sifa hatuwezi kutaja hapa, sifa lazima itajwe kwenye sheria yake mama ambayo ndio sheria Nam. 2 ya 1985.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 9 Marekebisho ya kifungu cha 37 pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano

Marekebisho ya Sheria ya Madawa na Usambazaji Haramu wa Madawa ya Kulevya Nam. 9 ya 2009

Kifungu 10 Kusomwa
Kifungu 11 Marekebisho ya kifungu cha 4

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa tuna sheria hii *very sensitive* inayohusu madawa ya kulevya, kifungu (a) uteuzi wa Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, unaonaje pakawekwa sifa za huyu Mwenyekiti hasa ukizingatia hii taasisi anayokwenda kuiongoza ni *very sensitive* inayohusu madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru Mwenyezi Mungu sisi Zanzibar tumepata bahati ya kuwa na Rais msikivu, Rais muaminifu na Rais anayekubali kushauriwa, anayefuata sheria na Katiba, lakini hatujui Rais ajae kesho na kesho kutwa anaweza hapa kwa sababu sifa hizi hazijatajwa Rais ajae kesho na kesho kutwa akaja akamtafuta rafiki yake akampa hii nafasi kwa sababu fulani fulani. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba ziwekwe sifa za mtu huyu ambaye anatakiwa kuteuliwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kama utaratibu wa kanuni unavyotueleza wakati wa kuchangia mswada kama kuna Mjumbe anataka kufanya mabadiliko kwenye kifungu inahitaji pale alete hayo mabadiliko ya kifungu kisomekaje. Sasa wote waliochangia wamesema tuweke sifa, sisi utaratibu tuliokuja nao ni huu lakini hakuna mtu ambaye ameleta sasa mabadiliko ya kifungu hiki akasema sasa hizo sifa za Mwenyekiti ziweje. Kwa hiyo, wakati huu wa kupitisha kifungu kwa kifungu ukisema turudi nyuma kwenye mijadala tuanze kuweka sifa, nadhani kule tumeshatoka Mhe. Mwenyekiti.

Utaratibu ilikuwa ni kule mtu aje na marekebisho yake aseme kwenye kifungu hiki nataka sasa sifa za Mwenyekiti ziwe hizi, ila anaposimama hapa kupiga buti aeleze kama mimi nimeshaleta kifungu changu na nilieleza kiwe hivi. Kwa hiyo, sasa hivi ukisema tuanze kutaja sifa hapa tumeshapita kule, mimi nadhani hatutokuwa tunafanya sawa.

Mimi nimuombe Mhe. Hassan kama kwenye hili tulishalitolea ufafanuzi na tumelieleza vizuri, kwa hiyo atukubalie tuendelee, lakini pia ajipange vizuri wakati tunapochangia hoja hizi Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile ni Mwanasheria Mkuu lakini hakutaja kanuni inayonibana mimi kusema hapa sasa hivi, lakini naomba tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, leo tumekutana na bingwa hapa, maana yake hoja yetu ilikuwa ya msingi kutaja sifa na inaonesha yeye aliikubali lakini tumekosea hapo pa kutaja hizo sifa zenyewe. Labda tu kwa kusaidia kwamba pale tulikuwa kwenye Baraza sasa hivi tuko kwenye kamati, sasa imekula kwetu. Sasa sitaki kukuomba Mhe. Mwenyekiti turudi tena kwenye Baraza lakini hoja yangu mimi nilikwishaieleza ukiacha hii ya sifa ambayo ninaisamehe kwa sababu tumekosea utaratibu, lakini nilipendekeza kuweko na Naibu Mwenyekiti. Sasa hili nililitaja pale na nilizungumza kwamba mara nyingi Pemba kesi zinachelewa na zinachelewa kwa sababu

anasubiriwa Jaji atoke Unguja. Sasa hili suala la mwenyekiti nilizungumza kwamba angalau na zile kesi zinazohusu masuala ya dawa kuna Naibu Mwenyekiti ambaye atasaidiana na mwenyekiti kwa upande wa Pemba. Sasa hili sikulisikia naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naona waheshimiwa hawa wamejipanga vizuri kwenye mabuti. Kwa hiyo, ukisoma ile sheria mama Mhe. Mwenyekiti mbali ya nafasi hii ya Mwenyekiti, lakini wale wajumbe miongoni mwao wamepewa pia fursa ya kuchagua Makamu Mwenyekiti. Nadhani iko vizuri na nimesema ukitizama muundo wa ile sheria wengi waliokuwemo mule ni mawaziri wajumbe wa ile Tume ya Madawa ya Kulevya. Sasa utaratibu umewekwa kwenye ile sheria mama, sidhani kama tuna haja ya kuweka tena Makamu Mwenyekiti mwengine wakati utaratibu wa kisheria upo ambao sheria nyingi tunapozitunga tunaandika hivyo, kama wajumbe miongoni mwao watakuwa na uwezo wa kuchagua Makamu Mwenyekiti, ningeomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu ninaiona lakini hebu anisaidie ufafanuzi katika kushughulikia hasa zile kesi ambazo kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Upande upi umesema Mheshimiwa?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Yaani katika kifungu hiki hiki tunaposema kwamba yule Makamu Mwenyekiti maana yake hata huyo waziri hawezi akasimamia zaidi yale masuala ya madawa ya kulevya kwa upande wa Pemba awe Mwenyekiti lazima awe ana *overall* ya Zanzibar nzima katika haya masuala ya madawa ya kulevya labda nipate ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hii ni Kamati ya Kitaifa inayosimamia mambo haya na inasimamia pande zote, inasimamia Unguja na inasimamia Pemba ni kamati inayoratibu na kusimamia mambo haya kwa Unguja nzima haibagui kwa Zanzibar nzima, wala haibagui maeneo tukasema hili la Pemba na hili la Unguja, wajibu wao ni kusimamia kwa Zanzibar nzima. Kwa hiyo, nadhani Mhe. Hamza angekwenda kwanza akazisoma zile sifa na kazi ambazo zimewekwa za Tume hii, kazi zake ni nini, wajibu wake ni nini, mipaka yake ni mpaka wapi, angeitazama vizuri nadhani angekuwa na hoja nzuri ya kujenga hapo baadae, lakini kwa sasa nimuombe kwa sababu ni ya kitaifa hii ina-*cover* sehemu zote na wala hakuna haja sasa ya kuanza kubagua maeneo ukasema hili lisimamiwe eneo la Unguja na hili lisimamiwe eneo la Pemba.

Kifungu 11 Marekebisho ya kifungu cha 4
Kifungu 12 Marekebisho ya kifungu cha 5
Kifungu 13 Marekebisho ya kifungu cha 63

Sehemu ya Sita

Marekebisho ya Sheria ya Mashirikiano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Nam. Ya 2015

Kifungu 14 Kusomwa
Kifungu 15 Marekebisho ya kifungu cha 2
Kifungu 16 Marekebisho ya kifungu cha 21

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 16 marekebisho (c) kuna maneno yamesema kwamba kurejesha fedha zilizotumika kutokana na taratibu. Sasa hapa nilishauri katika mchango wangu niliochangia kwa maandishi, kurejesha fedha zilizotumika au kurejesha risiti au vielelezo vya fedha zilizotumika?

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ukitizama asili yake ya kifungu hiki hapo awali kilivyokuwepo ilikuwa kikizungumzia utaratibu wa kurejesha fedha kabla ya kutia saini mikataba ya *PPP*, kwa sababu kabla haukufika huko kuna kazi nyingi zinafanywa; kutayarisha *feasibility study*, kutoa maoni, kuna kazi nyingi zinakuwa zinafanywa hapa kati kati.

Sasa mwanzo sheria hii ilikuwa inasema kabla ya kufika kutia saini kwa mikataba mnaweza kuweka utaratibu wa kurudishiana hizi fedha. Sasa hivi pendekezo lilokuwepo ni kwamba ziachwe taratibu zote zimalizike mpaka mkataba ule wa mashirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma utiwe saini ndio baadae sasa pande hizi mbili zikae zitafute huo utaratibu wa kurudishiana fedha. Hivi ilivyo ni nzuri zaidi kuliko ilivyokuwepo hapo awali kabla hatukuleta marekebisho haya Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Naomba tuendelee Mheshimiwa.

Kifungu 16 Marekebisho ya kifungu cha 21
Kifungu 17 Marekebisho ya kifungu cha 35
Kifungu 18 Marekebisho ya kifungu cha 38
Kifungu 19 Marekebisho ya kifungu cha 46

Sehemu ya Saba

Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 14 ya 2015

Kifungu 20 Kusomwa
Kifungu 21 Marekebisho

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi wakati nachangia Mhe. Waziri wa Fedha alichangia katika eneo moja nililoligusa, lakini katika suala la kisheria nilipozungumza niliangalia katika *spelling* ya Kiingereza neno la "*chasses"* ukurasa Nam. 196(g) *motor vehicle and other means of transport*, *spelling* ya *chassis* ilikuwa imekosewa.

Halafu nilishauri kwenye boksi la mwisho *chart* Nam. 7 *personal use* baada ya *business* kama waangalie kuweka *commercial*, hilo la kwanza.

Pia nilizungumza katika suala la msingi kabisa juu ya kuongeza *chart* pale kama ingewezekana kwamba kwenye hicho kifungu 21(c) kinataja fedha katika *account* ya *bank*, taasisi ya fedha iliyopo nje ya Zanzibar taja nchi ambazo unamiliki *account* ya *bank*. Nikataja kwamba kuna benki za biashara ambazo ni *Commercial Bank*, lakini nikazungumzia pia kuna *Official Bank* na pia nikataja kwamba mtu anapomiliki hisa katika kampuni, ambaye ni *shareholder*. Sasa haya yote pia nina-*result* mtu kupata fedha, hapa nikasema nitahitaji maelezo na hakuna mtu aliyesimama upande wa serikali kulieleza hilo nikaridhika, kwa hiyo naomba majibu juu ya hilo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hili la *spelling* nadhani tulilikubali tukasema hili halina matatizo tutarekebisha. Lakini hili jengine ambalo Mhe. Simai amelizungumza la biashara, watu kuwa na *shares* haya yote yamo kwenye ile sheria mama. Nimetizama ile sheria mama kuna *tables* nyingi ambazo zimeelezwa, hii ya sasa hivi tunayozungumzia ni ya benki na hii ya pili ni ya vyombo, lakini kuna ya makampuni kama unamiliki kampuni imeelezwa utaje hisa ngapi unamiliki. Sasa imetaja majadweli mengi lakini baada ya kupitia tumeona majadweli haya mawili ndio yana matatizo, ndio maana tumeleta marekebisho.

Kwa hiyo, nimuhakikishie Mhe. Simai akitizama ile sheria na akitazama yale majadweli yaliyokuwemo basi yote haya ambayo ameyazungumza yametajwa. Lakini kwenye hii tunachorekebisha ni hili ambalo linazungumzia benki yako na hili ambalo linazungumzia aina ya vyombo ambavyo tutakuwa tunamiliki,

maana yake hii inatuhusu sisi sote tukiwemo na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa hiyo hata yeye yumo Mhe. Simai.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante unajua sijamsikia vizuri lakini kama nimemsikia kwamba suala la *Official Bank* amelipokea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, unapotaja jina lako la benki, unapotaja aina yako ya *account*, kiwango, haya yote kwenye ile fomu yameelezwa inabidi uyataje hiyo benki yako iko hapa, hiyo benki yako kama kafungua juzi Mauritius alipokwenda itabidi aitaje, na hiyo *Official Bank* yake aliyofungua huko. Kwa hiyo, upo utaratibu mzuri umeelezwa kwenye ile sheria Mhe. Mwenyekiti asiwe na wasi wasi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu nimepokea hayo maelezo yako ni kwamba katika hizo fomu zitakapokuwepo itaonesha kwamba kuna *Commercial Bank* na pia kuna hizo *Official Banking*, kwa hiyo mimi nimeridhika na hilo. Kwa hiyo, mimi namshukuru na kama zile *account* zake pia na yeye aendelee pia. Ahsante.

Kifungu 21 Marekebisho ya jadweli la 2 pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nane

Marekebisho ya Sheria ya Biashara Nam. 14 ya 2013

Kifungu 22 Kusomwa
Kifungu 23 Marekebisho ya Kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24 Marekebisho ya Kifungu cha 23

Sehemu ya Tisa
Marekebisho ya Sheria Chuo cha Kilimo cha Kizimbani Nam. 5 ya mwaka 2007

Kifungu 25 Kusomwa
Kifungu 26 Marekebisho ya Kifungu cha 7 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27 Marekebisho ya Kifungu cha 9

Sehemu ya Kumi

Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo
Nam. 4 ya mwaka 2012

Kifungu 28 Kusomwa
Kifungu 29 Marekebisho ya Kifungu cha 9

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka ufafanuzi na hasa baada ya ile hoja yangu kupanguliwa ya kuambiwa kwamba, hakuna umuhimu wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutajwa na wao kwenye sheria wakawa kama ni sehemu ya madiwani, hasa baada ya kuambiwa Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa sasa hivi kwamba atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Maendeleo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa akitoa ufafanuzi alielezea, kwa sababu hoja za Wajumbe zilikuwa kwamba huyu mkurugenzi mjumbe na sisi tuna Kamati za Maendeleo mbali mbali katika maeneo yetu. Sasa tunataka kupitisha miradi yeye ana shughuli zake na huku kamati nyengine za maendeleo zinataka kupitisha shughuli zake, tukapata ufafanuzi kwamba anaweza akamteua afisa akaja akashikilia kile kikao. Je, kama hatukuweza kuweka hapa kifungu kidogo ambacho kinafanya kuwa Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa ambaye atakuwa katibu au mjumbe wake, maana yake hapa tumemfunga moja kwa moja ni Mkurugenzi tu wa Manispaa. Sasa hapa labda atusaidie Mhe. Mwanasheria Mkuu itakaa vipi? Je, hapa kwa kuwa ametajwa mkurugenzi akimuwakilisha mjumbe wake ataweza ku-*fit* katika hiyo nafasi? Tunaomba atusaidie ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka hasa jibu hili lijibiwe na Mwanasheria Mkuu, lakini Mwanasheria Mkuu ameniridhia niseme chochote.

Mhe. Mwenyekiti, nia ni kwamba mkurugenzi ni taasisi, kwa maana sio yeye kama yeye ni taasisi. Kwa hiyo, mkurugenzi ana mamlaka ya kumteua afisa yeyote yule pale ambapo hizi shughuli zitakuwa zinaingiliana. Kwa mfano, leo kuna Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Tumbatu, wakati huo huo iko ya Jimbo la Nungwi na wakati huo huo iko ya Jimbo la Chaani. Kwa utaratibu wa sasa ni kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa ana timu nzuri sana ya wataalamu, ambapo kwa mujibu wa sheria hii ya ugatuzi wa madaraka sio muda mrefu tunategemea serikali kuwatoa wataalamu katika sekta/wizara mbali mbali kuwa chini ya Mkurugenzi wa Manispaa au Halmashauri au Baraza.

Kwa hiyo, miongoni mwa wale wataalamu watakaokuwepo pale ama anaweza akenda yeye ama atamuwakilisha mtu kwa niaba, lakini sheria inamtambua kwamba mkurugenzi ndiye katibu wa kamati. Sasa kwa nia ya utekelezaji wa zile shughuli za Kamati za Maendeleo sio lazima mkurugenzi awe yeye tu mkurugenzi kama yule mkurugenzi, lakini mkurugenzi ni taasisi na ana uwezo wa kuteua afisa yeyote akamuwakilisha katika kamati hiyo na atakapokuja kule atakuja kwa niaba ya mkurugenzi. Nilitaka niseme hivyo ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana namshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake huo mzuri. Sasa hapa labda pia atusaidie kwamba huyu Mkurugenzi au yeyote kama sheria inavyosema. Kwa sababu kama alivyosema mkurugenzi sio mtu tu, mkurugenzi ni taasisi. Hilo nafikiri hatuna tatizo nalo, sasa je, hawa watasimamia tu zile fedha za Mfuko wa Jimbo ambazo tunapewa na serikali au watasimamia na shughuli nyengine tunazozifanya katika jimbo? Kwa sababu katika hii miradi ukiangalia mfano kama sasa hivi, ukienda jimboni utakuta tayari kuna ma-*grader* yanafanya kazi lakini Mfuko wa Jimbo bado hatujapata.

Je, hawa wakurugenzi ambao ndio watakuwa makatibu wetu wa kamati ina maana chochote tutakachokifanya wao ndio wataendelea kuwa makatibu wetu wa kamati au watasimamia zile fedha tu za Mfuko wa Majimbo. Kwa sababu sasa hivi tayari nafikiri Waheshimiwa wengi wameshateua makatibu na shughuli zinaendelea, maana sisi huwa hatusubiri pesa za Mfuko wa Jimbo tukiona jimbo kidogo linalegalega mzee unajitutumua uonekane upo.

Sasa mimi nafikiri Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pia yupo keshafahamu ujumbe wangu, labda tupate ufafanuzi Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi, lakini pia nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma na niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi kwa kazi nzuri ambazo wamekusudia kuzifanya majimboni, na hilo hasa ndio lengo la wananchi kuwachagua viongozi wetu hawa ili kutekeleza wajibu wao kwa kuwatumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hii ninayozungumzia humu ni fedha za Mfuko wa Jimbo ambazo zimetolewa na serikali, ndizo ambazo zinatakiwa ziwekewe mahitaji yake sawa na utekelezaji wake uonekane. *CAG* anapofika pale anakwenda kukagua kuona ule utekelezaji wa fedha za serikali namna zilivyotumika na fedha nyengine zozote zile, ambapo naamini waheshimiwa wanazitumia kwa wingi katika majimbo yao na waendelee kuzitoa na kuzifanyia uamuzi ni wao

wenyewe katika kusimamia mambo yao na kuwatekelezea wananchi matakwa yao. Haitahusiana na miradi mingine ambayo Mwakilishi mwenyewe anaianzisha kwa fedha zake binafsi au kwa fedha ambazo kwa njia nyengine yoyote atazipata kwa ajili ya kufanyia miradi katika eneo lake. Hapa nazungumzia zile *specific,* fedha kutolewa na serikali kwa ajili ya Mfuko wa Jimbo. Huyu katibu atakuwa dhamana kwa sababu ya mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa mfuko wa ubunge. Mhe. Mwenyekiti ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua tunauliza hivi kwa sababu tayari waheshimiwa tunanong'ona, kwani kuna baadhi yao tayari kuna kazi ambazo wameshazifanya na pengine wengine wameshakubaliana na kamati zao kwamba acha tunafanya shughuli hizi zikija zikipatikana zitarejeshwa.

Sasa huku tulikuwa hatujapitisha sheria, huyu Katibu wa Halmashauri anayekuja hayo ya huko nyuma hayajui, sijui tutatumia utaratibu gani hapo katika kuona ni namna gani haya mambo huyu Katibu wa Halmashauri atatambua yale mengine ambayo waheshimiwa tayari wameshaanza kuyafanya.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea naona ulikuwa unazungumza zaidi, hayo naona kama ni mambo ya baadae katika utekelezaji. Mhe. Hamza Hassan Juma umeshajibiwa tuache tuendelee.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri sana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mimi nilikuwa nataka kumuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwenye sheria humu najaribu kuangalia ile sheria mama kazi za huyu katibu hasa wa hii kamati, najaribu kuzitafuta sizioni pengine sioni vizuri. Kwa sababu unajua pamejitokeza ile haja ya *accountability* ya fedha, imezungumzwa humu kwamba ile kamati itakuwa na wajibu huo, lakini hizi ni kazi za Mhasibu Mkuu. Sasa kuepuka muingiliano na kumpa kazi yake inayostahiki yule mhasibu ningeshauri sana hili suala la hizi kazi za katibu, kwa sababu najua tuna *practical example* huko kwenye Halmashauri. Kuna mambo yanafanyika haidhuru wewe mwenyewe ndiye mwenyekiti wa kamati, lakini yule katibu mnakaa naye, mnapanga lakini ule utendaji na zile pesa zinavyotumika kidogo kuna shaghala baghala. Sasa hizi kazi za katibu ningetaka kumshauri sana Mhe. Mwanasheria Mkuu tumechelewa lakini vizuri zikawa *defined* hasa. Ahsante ni ushauri tu.

Kifungu 29 Marekebisho ya Kifungu cha 9

Kifungu 30	Kusomwa
Kifungu 31	Marekebisho ya Kifungu cha 4
Kifungu 32	Marekebisho ya Kifungu cha 10
Kifungu 33	Marekebisho ya Kifungu cha 11
Kifungu 34	Marekebisho ya Kifungu cha 12
Kifungu 35	Marekebisho ya Kifungu cha 22
Kifungu 36	Marekebisho ya Kifungu cha 26

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kifungu kinachotaka kukataza sasa kimeanza kukataza. Zanzibar ni nchi ya Kimapinduzi, Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964 yalikuja kwa lengo la kuwaletea maendeleo wakulima na wakwezi, miongoni mwa shughuli moja ya ukulima moja ni ufugaji na uvuvi, natambua ndani ya Baraza hili muna wengine ni wavuvi lakini wengi wetu ni wakulima ambao ndani yake muna ufugaji. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Welezo, wananchi wangu wengi ni wafugaji, naheshimu agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar alilolitoa si chini ya mara nne kumsikia hataki kuwaona ng'ombe mjini, ni agizo zuri ingawaje limechelewa kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, agizo hili lilipotekelezwa limetekelezwa kwa kutukomoa, na wananchi wetu wengi wanapata shida kwa sababu watekelezaji wa agizo hili wengine walikuwa wanawanyang'anya pesa wananchi wetu. Sasa leo tunarekebisha sheria hapa ya kuwakataza.

Mheshimiwa mimi naomba kusema Dkt. Mwinyihaji Makame alisema lianze kudhibiti kama alivyoliagiza mwenyewe Mhe. Rais kwamba hataki kuwaona ng'ombe mjini sikukataa, lakini wananchi wetu wengi ni wafugaji tunapowakataza tumewaondoshea *livelihood* yao ya kimaisha, tukatae kuwaona ng'ombe mjini tusiwakataze kufuga, tukataze kuzurura ng'ombe mjini. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ alilizungumza hili na akalijibu vizuri kwamba nini dhamira yake. Ni kwamba sio dhamira ya serikali kukataza kwenye maeneo yote lakini kwenye maeneo ambayo inabidi yakatazwe lazima uwe na *instrument* itayokufanya wewe sasa utoe tangazo la kukataza. Kwa mfano, unaposema mjini haparuhusiwi kulisha mifugo lazima uwe na sheria ambayo inakuruhusu kusema hivyo kwamba mjini hairuhusiwi kulisha mifugo, lakini sheria haikuishia hapo ikasema kwamba itaweka utaratibu wa maeneo hayo mengine ambayo sasa itabidi yaruhusiwe. Mhe.

Waziri alieleza vizuri kwa utaratibu na kwa ufasaha, akaeleza vizuri dhamira ambayo imekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya pia yanatokea, unasikia ukitizama televisheni huko Mhe. Hassan Hafidh Uingereza maradhi ya ng'ombe, *bird flu*, yote haya inabidi na sisi tuwe na uwezo wa kuweza kutoa makatazo kwenye maeneo haya ya kutokea. Sasa dhamira sio kukataza maeneo yote, lakini dhamira ni kuratibu vizuri kwenye maeneo ambayo yataruhusiwa na kwenye maeneo ambayo hayataruhusiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili nadhani *spirit* iwe hiyo, na nimuombe Mhe. Hassan Hafidh tuendelee na wananchi wake wamemsikia wa Jimbo la Welezo kama kawapigia debe, lakini kwenye hili dhamira iwe ni hiyo na sio kukataza.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa mara ya kwanza leo kukubali kwamba hapa kakosea, na alipotamka ninanukuu maneno yake kasema: "dhamira sio kukataza", bali maandishi yameandika kukataza. Kwa hiyo, kama Mhe. Mwanasheria Mkuu amekubali kuwa hapa maneno yaliyoandikwa sio dhamira na haya tunayoyafanyia kazi hapa leo ni maandishi ambayo yameandikwa kisheria, na Mwanasheria Mkuu kakubali kwamba dhamira sio hiyo. Kwa hivyo hapa kuna matatizo ya maandishi, ningeliomba Baraza lako tukufu likae kama Baraza twende kwa mujibu wa kanuni ili tuendane na dhamira ya Mwanasheria Mkuu tutengue haya maneno.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri sisi sote tumefahamu alichokusudia Mhe. Mwanasheria Mkuu, ni kwamba kwa yale maeneo ambayo yanatakiwa kukatazwa yatakatazwa, na kwa yale maeneo ambayo yatapangiwa utaratibu maana yake yatapangiwa utaratibu, *simple as that*. Nafikiri inaeleweka Mheshimiwa tunakuomba tuendelee hii isiwe hoja ya kushindana, nakuomba sana. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, si mshindani wala sishindani na kiti chako, bali nilikuwa naeleza yale maneno aliyoyasema Mwanasheria Mkuu na yaliyoandikwa. Nakubali uliyoyasema wewe ndiye Mwenyekiti lakini dhamira sio maandishi ya hapa, na mimi ni mtetezi wa wananchi, nimechaguliwa na wananchi na ninaogopa sheria hii ikipita wananchi wangu kesho watendaji wa Mhe. Waziri watasema ng'ombe hawatakiwi waonekane kwa sababu sheria ishawakataza, naogopa, na mimi ndio walionipa kura na wanaonituma. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka busara yako lakini nasema ukweli wangu maandishi haya yananitisha, yako vibaya na

makali; silo agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Agizo la Rais hataki kuwaona ng'ombe mjini, ambalo mimi nakubaliana nalo na nililisema waziwazi wizara imechelewa kulitekeleza, lakini maandishi yananitisha, yakipita haya yatakuja kutekelezwa kama yalivyopita tutakuja kuambiwa ndio yameshapita Barazani. Sasa Mwenyekiti kiti chako nakiheshimu na ninakiogopa, hivyo naomba busara yako katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri busara yangu ni kwamba tuendelee. Naomba sana tuendelee na Mhe. Hassan Khamis Hafidh kifungu kinajieleza hayo maneno aliyoyasema ikiwa kama kasema, ikiwa hakusema lakini sheria imo ndani ya karatasi.

Leo Mwanasheria yupo, kesho hayupo lakini hii itabakia kuwa hivi hivi. Kwa hiyo, hayo aliyoyasema pengine inawezekana ulimi umeteleza lakini tunayafuata haya yaliyokuwemo ndani ya maandishi sasa tunaendelea kutokana na haya maandishi kwa sababu tumeyakubali au vipi?

Wajumbe: Ndiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifungu 36	Marekebisho ya Kifungu cha 26
Kifungu 37	Marekebisho ya Kifungu cha 30
Kifungu 38	Marekebisho ya Kifungu cha 88

Sehemu ya Kumi na Mbili
Marekebisho ya Sheria ya Kodi, Ongezeko la thamani
Nam. 4 ya mwaka 1998

Kifungu 39	Kusomwa
Kifungu 40	Marekebisho ya Kifungu...

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kwanza nataka nisikitike kwamba waziri husika mwenye dhamana na aliyetoa maelezo haya hayupo, lakini katika maelezo yake alipozungumza alitaja juu ya utaratibu mzima wa ukusanyaji wa kodi na mapato yaliyopangwa.

Lakini kifungu hichi kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, katika sheria za kodi zetu za mwaka 1998 tuliondoa suala la *sales tax*, na tukaenda moja kwa moja kwenye *VAT,* na tulianza kutoka milioni 10 tukaenda 15 na tukafika hadi sasa milioni

30. Ina maana kampuni yoyote kwa mujibu wa sheria za kodi na ile *principle* ya *VAT* na katika *spirit* ya Utawala Bora wa nchi yetu kwamba kampuni yoyote ambayo inafanya biashara zaidi juu ya milioni 30 anatakiwa akajisajili na *VAT*. Hapa kuna taratibu mbili inatumika hasa katika mahoteli; kuna *hotel levy* na kuna *VAT*. *Hotel levy* kwa wenzetu Tanzania Bara wanakusanya hawa *local* ***government***, hapa Zanzibar mtu anawekewa kiwango cha U$ 100 lazima afikie ndio katika hicho kiwango anatakiwa akalipie hiyo *VAT* ya 10%.

Sasa hoja ambayo niliyozungumza hapa kwa mujibu wa kifungu hichi bila ya kuathiri masharti ya sheria hii Waziri ataweka utaratibu wa kanuni ya malipo ya *VAT* kwa manunuzi ya bidhaa kutoka Tanzania Bara. Kifungu hichi kitawasaidia wale ambao wako *VAT registered*, wale ambao wako wanalipia *hotel levy* ambayo pia wanafanya mauzo zaidi ya milioni thalathini kifungu hichi hakiwezi kuwasaidia, na hawa pia watakuwa wanachukua hizi huduma na manunuzi kutoka Tanzania Bara, na kwa mujibu wa sheria za kwetu za kodi utaratibu huo wa kuweka *double standards* yaani Ali analipa *VAT*, Juma analipa *hotel levy* tukienda mitaani huko kwenye mahoteli watu watashindwa kutuelewa. Leo hoteli fulani inalipa *VAT* hoteli hii inalipa *hotel levy* huyu mwenye *VAT* yeye ndiye atafaidika na kifungu hichi. Sasa huyu mwenye *hotel levy* Mhe. Waziri anatakiwa anijibu wanawawekea utaratibu gani, kwa sababu na yeye pia analaza wageni, anatoa huduma ya vyakula, ananunua umeme...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hoja sasa unatoa *speech*, nenda kwenye hoja yako sema hoja yako ujibiwe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Hoja yangu nataka nifahamu katika kifungu hichi wale ambao wanatumia *hotel levy* na manunuzi yao yapo zaidi ya milioni thalathini na kwenda juu, sasa hawa watafaidikaje na kifungu hichi mwisho wa mwezi wanapopeleka *returns* zao za fedha.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kama nimemfahamu Mhe. Simai Mohammed Said anazungumzia utaratibu wa malipo ya zile ada za kwenye mahoteli na nilimsikiliza kwa makini sana Mhe. Waziri wa Fedha, na alisema mambo haya ya mahoteli yanaratibiwa na Sheria Namba 1 ya mwaka 1995 nadhani ndiyo aliyosema. Hapa utaratibu unaowekwa Mhe. Mwenyekiti ni ule wa kurudishiana *VAT* baina yetu na wenzetu wa Tanzania Bara.

Zamani ilikuwa wao ni mawakala wetu na sisi ni mawakala wao, wanakusanya kwa niaba yetu baadae wanaturudishia na sisi tunakusanya kwa niaba yao baadae tunawarudishia. Lakini kwa sababu ya marekebisho ambayo yametokea

kwenye sheria ya fedha iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utaratibu huu umeondoshwa. Sasa kama umeondoshwa inatulazimu na sisi turekebishe sheria zetu ili ziendane kama vile ambavyo wenzetu wamerekebisha, ndio utaratibu unaozungumziwa hapa Mhe. Mwenyekiti.

La sivyo itakuwa sisi wenzetu hawaturejeshei lakini tukusanye tuwarejeshee, haitowezekana hivyo, na ndio maana tumeweka kifungu hichi kama hata mwaka ujao wa fedha wenzetu wakija na utaratibu mwengine sisi tusiwe na haja tena ya kuleta marekebisho, hapa tumuachie sasa fursa Mhe. Waziri dhamana wa fedha afanye marekebisho haya kwa kupitia kanuni ambazo wanazitengeneza.

Sasa utaratibu huu uliowekwa ni ule ambao ulikuwepo wa kisheria kwa kurudishiana *VAT* baina ya Tanzania Bara na sisi Zanzibar, na haizungumzii Mhe. Mwenyekiti utaratibu wa *hotel levy* kama ambavyo Mhe. Simai Mohammed Said alivyozungumzia.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina hoja tena ya msingi kabisa. Hoja yangu ni kitu kimoja ...

Mhe. Mwenyekiti: Sasa kama una hoja binafsi uilete mezani kwanza halafu baadae utaileta ndani ya Baraza hili au unasemaje. Endelea.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, au unataka nikae.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ninayekuruhusu ni mimi, kwa hiyo mimi nimesema endelea naomba uendelee kusema, sawa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hapa hichi kifungu kilipokaa naomba nifahamike vizuri na nimerudia tena kukizungumza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu hajajibu hoja yangu ambayo niliyozungumza, na Mhe. Waziri anazungumza kuhusu mapato ya hoteli. Kifungu hichi kama tunataka tukipitishe hapa basi ilikuwa iandikwe hapa:

"Bila ya kuathiri masharti ya sheria hii waziri ataweka utaratibu wa kanuni ya malipo ya *VAT* kwa manunuzi ya bidhaa kutoka Tanzania Bara hasa kwa kampuni ambazo zilikuwa ziko *registered* Zanzibar na zile zilizokuwa zinalipa *hotel levy* hazimo kwa sababu tayari kuna kampuni zinalipa, zinakuwa *registered in Zanzibar*, wao wanalipa zaidi ya kiwango cha *VAT* kilichowekwa. Sasa hawa wenye *hotel levy* wanakwenda wapi jamani.

Sasa hapa mimi nahisi labda kwa kusaidia Baraza hili jambo kwa sababu ni pevu, na hichi kifungu lazima kipite ili waziri aweze kukifanyia kazi. Kwa sababu tayari kuna makampuni ambapo *VAT registered Zanzibar* wanahitaji kifungu hichi wanatimiza vigezo vyao.

Sasa ili kusaidia Mwanasheria Mkuu alichukue hili alipeleke, kwa sababu kwa vile anachokijibu yeye sicho ninachokizungumza mimi hapa. Kwa hivyo, tukubaliane, na kwa ajili ya Baraza tunataka liendelee hichi kifungu lazima kipite kwa sababu hawa ambao wako *VAT registered* wanahitaji hichi .

Mimi nataka kujua na hawa wanaolipa mabilioni ya pesa hapa Zanzibar wako kwenye *hotel levy*, hasa hayo manunuzi yao watakaopata watafaidika vipi, na Mwanasheria Mkuu ndiye anayetakiwa anijibu hapa, hiyo ndiyo hoja yangu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza sana kwa makini Mhe. Simai Mohammed inawezekana anayo hoja lakini amezungumza sana sasa akawa anachanganya na mengine.

Mimi ninachotaka kusema ni kwamba, ninamfahamu anachotaka kuzungumza, ukisoma sheria kodi kuna sheria nyingi za kutoza kodi, moja aliyoizungumza ni hii ya *hotel levy* ambayo inatoa utaratibu wa ukusanyaji wa kodi kwenye mahoteli.

Hoja yetu hapa tuliyokuja nayo Mhe. Mwenyekiti, ni kuondoa ule utaratibu uliokuwepo wa kukusanyiana kodi na kurudishiana tena kodi yenyewe kwenye *VAT,* ile ya 10% ambayo tunakusanyiana kwenye bidhaa umekwenda kununua saruji Dar-es-Salam umekwenda kununua nondo umekwenda kununua sigara wenzetu wale wanatukusanyia halafu baadae wanaturudishia, wanasema kwa mwezi huu watu walionunua ni hawa kwa hiyo na nyinyi leteni risiti zenu ziwiane halafu wanaturudishia. Sasa hivi wenzetu utaratibu huo wameuondoa. Wamesema sasa hivi hakuna utaratibu huo.

Sasa na sisi kodi ile tunaihitaji lazima na tuweke utaratibu ambao tutahakikisha na sisi kwa upande wa kwetu tunakusanya hii kodi ndio hoja iliopo hapa Mhe. Mwenyekiti, hii ya *hotel levy*, sheria yake ni namba 1 ya mwaka 1995, na iko vile vile utaratibu umeelezwa vizuri mtu gani anatakiwa alipe kiwango gani, mtu akiwa na biashara ya milioni ngapi anatakiwa awe wapi, utaratibu upo mzuri tu umeelezwa.

Lakini hapa hoja ya Mhe. Simai Mohammed Said haitoweza kusimama, kwa sababu tunachozungumzia ni utaratibu wa *VAT* wa bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara na bidhaa zinazonunuliwa Zanzibar kupelekwa Tanzania Bara. Huo ndio ufafanuzi ambao tunaweza kuutoa kwa upande wetu Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria ya *VAT* sheria ya kodi ya mwaka ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohammed Said ningekuomba jambo moja, hayo yote yameshaelezwa wewe umeeleza kwa upande wako na Mwanasheria Mkuu kaeleza kwa upande wake.

Nafikiri tumwachie Mwanasheria Mkuu aichukue hoja yako tupitishe kifungu halafu hiyo hoja sasa Mwanasheria Mkuu watakaa pamoja na Waziri wa Fedha na wewe kufahamishana vizuri zaidi. Kwa sababu Mwanasheria Mkuu amekusudia kupitisha au nipigishe kura sasa watu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ikipigishwa kura nitashindwa. Mhe. Mwenyekiti, ninachoomba tu nimalizie mimi hichi kifungu napitisha wala sina lengo la kupiga kura. Lakini ninachokitaka kwamba maelezo yachukuliwe ya zaidi, kwa sababu kuna watu hapa watafaidika na kuna watu hawatafaidika. Sasa hawa wanaolipa *hotel levy* ambao tayari wao wanatimiza vigezo wako chini ya *VAT* kwa sababu mauzo yao yako zaidi ya milioni thalathini na kuendelea juu. Sasa katika kifungu hichi wao hawataweza kufaidika ndio maana utaratibu uunganike. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 40 Marekebisho ya kifungu cha tatu

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya kutunga sheria imeupitia mswada kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali hoja.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mwanasheria Mkuu ametoa hoja, wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mkono, wale wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya sheria mbali mbali ya mwaka 2016

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya sheria mbali mbali ya mwaka 2016 sasa usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mimi nichukuwe fursa hii adhimu kuwashukuru sana kwa siku hii ya leo kwa utulivu wenu na kwa wale ambao wamechangia lakini hasa wale ambao wamepiga buti niwashukuru wote kwa sababu wamefanya wajibu wao uliowaleta hapa.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuahirisha kikao naomba niwatangazie kwamba ile *caucus* ya Chama cha Mapinduzi iliyokuwa ifanyike baada tu ya kikao hichi imeahirishwa hadi Jumatatu, lakini ile semina iliyokuwepo leo itakuwepo, kwa hiyo mnaombwa Waheshimiwa wote muhudhurie katika semina baada tu ya kutoka hapa.

Baada ya kusema hayo naahirisha kikao hichi hadi siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi. Nawashukuru sana.

(Saa 8:16 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/09/2016 saa 3:00 asubuhi)